Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Sita – Tarehe 10 DESEMBA, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (*Mhe. Job Y. Ndugai*) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 54

Sekondari za Masasi Girls na Ndanda Boys

MHE. MARIAM R. KASEMBE aliuliza:-

Shule za Sekondari za Masasi *Girls* na Ndanda *Boys* zilikuwa zikuchukua wanafunzi wa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne lakini sasa zimefanywa za Kidato cha Tano na Sita na hivyo kutumia sehemu ndogo sana ya majengo na mengine yakibaki bila kutumika:-

(a) Je, Serikali haioni ni vema kuzifanya shule hizo zichukue wanafunzi kuanzia Kidato cha Kwanza hadi cha Sita ili kunusuru rasilimalli za majengo yaliyobaki bila kutumika?

(b) Shule ya Masasi *Girls* haina uzio, gari hata moja, haina vyoo kwenye mabweni hali ambayo ni hatari kwa afya za wanafunzi.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutatua matatizo hayo ambayo ni ya msingi sana hasa katika mchakato wa Bajeti ya mwaka huu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a) na (b|) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilizibadilisha baadhi ya shule za sekondari za bweni kuwa Kidato cha Tano na Sita tu ili kutoa fursa zaidi kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha Tano kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaohitimu kidato cha Nne na kujiunga na Kidato cha Tano.

Baada ya kubainika kuwa baadhi ya shule zinasajili wanafunzi wa kidato cha tano wachache kuliko uwezo wa shule, tarehe 12 Februari, 2013 Serikali ilitoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa wote nchini kufanya tathmini na kuona uwezekano wa kupeleka wanafunzi wa Kidato cha Kwanza katika shule za bweni ambazo zimebainika kuwa wanafunzi wachache wa Kidato cha Tano na Sita ikiwemo shule ya sekondari ya wasichana Masasi na Wavulana Ndanda.

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, shule ya sekondari ya wasichana Masasi ni moja kati ya shule kongwe hapa nchini. Serikali imeanzisha mkakati maalumu wa kuziboresha kwa awamu shule zote kongwe nchini ambapo kila mwaka hutoa fedha kwa ajili ya ukarabati na kuimarisha miundombinu mingine ikiwemo uzio, mifumo ya maji na umeme.

Mwezi Oktoba, 2013 jumla ya bilioni 3 zimetumwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya shule za Sekondari kongwe 59 ikiwemo shule ya Sekondari ya wasichana Masasi iliyopewa shilingi milioni 50.

(c) Aidha, Serikali kupitia mipango na Bajeti za Halmashauri inatenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo kuboresha miundombinu ya shule na ununuzi wa magari.

Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Halmashauri ya Mji wa Masasi imetengewa shilingi bilioni 117 kwa ajili ya kukamilisha miradi hadi sasa shilingi bilioni 85 zimeshapokelewa.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza ya maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri amesema Kwamba Halmashauri pia zimekuwa zikitenga fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwaka huu mwanzoni maafa makubwa yametokea katika Wilaya yetu ya Masasi kwa kuchomwa Maofisi moto, magari na vifaa mbalimbali vya Halmashauri hivyo kupelekea Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na Halmashauri ya Mji kuingia katika umaskini mkubwa.

Je, Serikali haioni ipo haja ya ununuzi wa gari kwa ajili ya sekondari ya Masasi na ujenzi wa uzio ikabeba jukumu hili Serikali Kuu?

La pili, kwa kuwa utekelezaji wa kupeleka tena wasichana katika shule ya wasichana Masasi pamoja na Ndanda limetekelezwa kwa kiwango kidogo sana katika Sekondari ya Masasi.

Je, Serikali ipo tayari katika matokeo ya darasa la saba mwaka huu kuongeza idadi kubwa ya wasichana na kupeleka katika shule ya sekondari ya Masasi na sekondari ya Ndanda?

NAIBU SPIKA: Majibu ya uhakika Mheshimiwa Waziri kuhusiana na Sekondari ya Masasi. Kumbukumbu zinaniambia Mheshimiwa Spika amesoma katika shule hiyo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ilipata maafa makubwa sana kutokana kuchomwa moto kwa magari yake mengine yakiwemo magari ya wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili lilipelekwa Idara ya Maafa nina imani kabisa kwamba linashughulikiwa. Lakini kwa masuala kwa maana Bajeti zinazokuja pia tutaangalia kwa namna ya pekee Halmashauri ya Wilaya na Mji wa Masasi.

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kupeleka wanafunzi katika shule ambazo zilikuwa kidato cha tano na sita kama nilivyosema katika jibu la msingi tayari tumewaandikia Makatibu Tawala na tuna imani kabisa katika mwaka 2014 yaani kuanzia Januari, katika hizo shule Tanzania nzima ambazo nafasi zake nyingi sana zinaachwa wazi watapelekwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Hawa jamaa wanachoma mpaka gari la wagonjwa. Bado tupo Kusini, swali linaulizwa na Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, kwa niaba yake.

Na. 55

Ubovu wa Barabara ya Singino – Mkocho – Kivinje

MHE. RASHID ALI ABDALLAH (K.n.y. MHE. SELEMANI S. BUNGARA) aliuliza:-

Kwa muda murefu sasa kipande cha barabara cha kutoka Singino - Mkocho- Kivinje yenye urefu wa kilomita 2.5 kimekuwa kibovu sana na kuleta kero na adha kubwa kwa watumiaji wa barabara hiyo na tarehe 18 Oktoba, 2010 Mheshimiwa Rais aliahidi kutengeneza kipande hicho kwa lami:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu ahadi hiyo?

(b) Je, ni lini ujenzi wa kipande hicho cha barabara utaanza?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiw Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliahidi kutengeneza barabara hiii kwa kiwango cha lami wakati wa kampeni za Uchaguzi wa Rais mwaka 2010. Barabara ya Singino-Mkocho- Kivinje, ina urefu wa kilomita 4.5 ambayo inaanzia kijiji cha Singino, Kitongo cha Mkocho kilichopo kilomita 5 kutoka Nangurukuru hadi mji wa kihistoria wa Kilwa Kivinje ambako kuna hospitali ya Wilaya ya Kilwa (Kinyonga Hospitali)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya ujenzi wa barabara ya Singino-Mkocho – Kivinje kwa kiwango cha lami imeanza mwezi Oktoba, 2013 na inatazamiwa kukamilika mwezi Aprili, 2014 kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Aidha, kupitia Bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013 Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ilipewa milioni 350 kwa ajili ya kuweka lami kilometa moja eneo korofi la barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ili barabara hii iweze kutengeneza na kukamilika kwa kiwango cha lami Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa inatakiwa kutenga fedha katika Bajeti yake ya mwaka wa fedha 2014/2015 na iendelee kuipa kipaumbele kwenye mipango ya Halmashauri mpaka itakapokamilika.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Hatma ya jibu ya suala hili imepewa Halmashauri.

[MHE. RASHID ALI ABDALLAH]

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, toka mwaka 2010. Suala la kupewa Halmashauri kukamilisha suala hili si sahihi. Mheshimiwa Waziri atueleze sasa ni lini barabara hii itamalizika kwa agizo la Mheshimiwa Rais? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ahadi hii ni ya Mheshimiwa Rais. Lakini kinachotakiwa ni Halmashauri husika iweke katika mipango yake na kukumbushia ahadi hii. Ndiyo maana tukasema waweke katika Bajeti ya mwaka 2014 haina maana kwamba wakiweka ni kwa fedha zao wanaiweka ili Serikali tuone na tuweze kupatia fedha.

Kama ambavyo walifanya mwaka 2011/2012 ambapo waliomba maombi maalum ya shilingi milioni 800 na sisi tukawapa milioni 350 kwa ajili ya kukamilisha. Kwa hiyo, tunachowaomba tu wao kazi yao, wajibu wao ni kuikumbusha Serikali kupitia Bajeti yao. Lakini sisi tunapenda kuahidi kwamba ahadi ya Rais lazima itekelezwe.

Na. 56

Tatizo sugu la Maji Safi na Salama Mbozi Magharibi

MHE. DAVID E. SILINDE aliuliza:-

Tatizo sugu la maji safi na salama Mbozi Magharibi, limeshindwa kupatiwa ufumbuzi wa kudumu tangu tupate uhuru:-

Je, ni lini tatizo hilo litatatuliwa Jimboni Mbozi Magharibi?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID E. SILINDE]

(a) Je, kwa nini Serikali imeshindwa kufikia lengo la kuwapatia wananchi wa maeneo hayo maji safi na salama angalau kwa asilimia 75 tangu uhuru?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012 Serikali ilitenga kiasi cha milioni 277 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji Namtambalala ambao tayari umekamilika na unahudumia watu wapatao 2,779 wa kijiji cha Namtambalala, mradi huu una tanki lenye ukubwa wa lita za ujazo 90,000 na vituo vya kutochea maji 9.

Aidha, Serikali inaendelea kutekeleza ujenzi wa mradi wa maji katika kijiji cha Itambula, ambapo milioni 251 zilitengwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali ilitenga milioni 233.8 kwa ajili ya mradi wa maji katika kijiji cha Iyendwe ambapo ujenzi wake unaendelea na ilitenga milioni 248.89 kwa ajili ya kijji cha Chilulumo ambao ujenzi wake unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014 Serikali imetenga milioni 571.3 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji katika kijiji cha Mnyuzi ambao kwa sasa upo katika hatua za mwisho za manunuzi na unategemewa kunufaisha wakazi wapatao 2,788.

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji 68 vimeingizwa katika mpango wa kutekeleza Awamu ya Pili ya miaka mitano ya Programu ya Maji na Usafi na Mazingira Vijijini utakaoanza mwaka 2014/2015 hadi 2018/2019 kwa gharama ya bilioni 26 ambapo utanufaisha watu wapatao 354,432 ifikapo 2025. Hivyo, kutatua tatizo la maji Jimboni Mbozi Magharibi.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, swali (b) halijajibiwa. Nilichokuwa nataka kuuliza ni kwa nini Serikali imeshindwa kupatia maji yaani kufikia lengo la asilimia 75 tangu tupate uhuru miaka 52 sasa. Kwa hiyo, ningependa arudie atupate sababu kwa nini wanashindwa? Ndiyo nataka arudie.

(b) Katika mwaka wa fedha 2013/2014 katika Bajeti iliyopita Halmashauri ya Wilaya ya Momba tumetengewa jumla bilioni 9 katika Matokeo Makubwa Sasa. Je, mpaka sasa ni kiasi gani kimetoka?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza natambua sana jinsi Mheshimiwa Silinde anavyofuatilia tatizo la Maji katika Jimbo lake. Lakini nataka kumhakikishia kwamba siyo kweli kwamba Serikali imeshindwa.

Katika jibu langu la msingi nimetamka vilevile vile vilivyoanza kupata maji sasa hivi vya Namtambalala ambavyo nilidhani kwamba kama Mheshimiwa Silinde kwa uungwana tu angeshukuru kwanza kazi iliyofanyika. Hilo la kwanza.

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ni mchakato na kupanga ni kuchagua, yapo mambo mengi ambayo Serikali imeyafanya ambayo sasa hivi tunajivunia. Lakini katika sekta ya maji baada ya kuona kwamba tatizo ni kubwa, Serikali imeamua kwa uamuzi mzuri kabisa kuingiza Sekta ya Maji katika Mpango wa *Big Results Now (BRN)*. Katika sekta sita, maji ni mojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango huu tumejiwekea malengo yafuatayo kwamba mwaka wa kwanza 2013/2014 tuwape Watanzania milioni 7,100,000 wapate maji wakiwemo wa Jimbo la Mbozi Magharibi ambayo itakuwa ni sawasawa na vijiji 1449 na miradi hii ndiyo ambayo nimeitaja inatekelezwa katika hatua mbalimbali.

Mwaka wa pili, 2014/2015 tumepanga kuwapa Watanzania wengine milioni 7 wakiwemo wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi na tumeagiza Halmashauri zote Juni mwaka kesho ziwasilishe vijiji Kata 20 mpaka 30 kwa ajili ya kuanza utekelezaji. Tukifanya vile mwaka wa tatu, tumepanga kuwapa Watanzania milioni 1,300,000 ambapo ukijumlisha miaka yote mitatu hiyo utapata Watanzania milioni 15.4 na *base* tuliyonayo sasa hivi ni milioni 15.2 na hivyo kufikisha Watanzania milioni 30.6 watakaopata maji ambao ni sawasawa na asilimia 74 tutakuwa tumeishafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 74 ni zaidi ya asilimia 65 ya malengo ya millennia, kwa hiyo tutakuwa tumevuka. Kwa hiyo, tuipongeze Serikali ya CCM kwamba itafanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, (b) ni kweli Mheshimiwa Silinde tuliingiza miradi ya *Big Results Now* ikiwemo Jimbo lako la Mbozi Magharibi, Mradi wa Kamsamba, mradi huu utahudumia vijiji vifuatavyo:-

Kamsamba, Muyu, Senda, Msoche, Mnkonko kwenye Bajeti tumetenga milioni 900.3, sasa hivi ninavyoongea umeshapelekewa milioni 63 kwa sababu tayari kazi ya usanifu ilishafanyika pale *DANIDA.*

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

Kwa hiyo, kazi ni ku-*up date* ule usanifu na kusaini Mkataba na Mkandarasi ili kazi iweze kuanza. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Silinde, huna swali tena. Mheshimiwa Laizer, swali la nyongeza.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali ndogo la nyongeza. Kwa kuwa juhudi anazozisemea Mheshimiwa Naibu Waziri ni za kweli. Lakini miradi inahujumiwa na watendaji wabovu walioko vijijini, waliopo katika Halmashauri. Kwa hiyo, suala hili mipango mizuri haiwezi kutekelezeka kwa ajili ya ubovu wa hao watumishi.

Je, Serikali inasema nini kuhusiana na hao watumishi wabovu ambao hawatekelezi miradi iliyopangwa? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni kweli Idara za Maji zina shida kubwa sana ya watumishi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli yapo baadhi ya maeneo ambao miradi haitekelezwi vizuri au inahujumiwa. Lakini ni kweli vilevile kwa sasa hapa tulipo eneo ambalo miradi imetekelezwa vizuri na inaendelea kutekeleza vizuri ni katika Sekta hii ya Maji ambapo miradi hii inatekelezwa kwa kusimamiwa na TAMISEMI kupitia Halmashauri wakishirikiana na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho ninaweza nikamwomba Mheshimiwa Mbunge ni kwamba pale inapoonekana kwamba vipo vitendo vya dhahiri vya kuhujumiwa tupeane taarifa na ndiyo maana tupo hapa ili tuweze kushughulikia mara moja inapoonekana kuna ushahidi wa hujuma inayotolewa. Niwaase wafanyakazi wote hasa kwenye Wizara ya Maji wanaosimamia miradi hii wawe waaminifu wachape kazi ili kuwapatia wananchi Maji. *(Makofi)*

Na. 57

Posho ya Mazingira Magumu kwa Walimu

MHE. ANNE KILANGO MALECELA (K.n.y. MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO) aliuliza:-

Walimu wanafanya kazi kwa mazingira magumu sana hapa nchini, ikizingatiwa kuwa wengi wako vijijini ambako huduma nyingi muhimu kama vile maji, barabara, umeme, matibabiu na kadhalika, hakuna:-

(a) Je, ni lini Walimu wataanza kupata posho ya mazingira magumu ya kazi?

(b) Je, ni lini Serikali itaanza kuwapa mishahara inayoendana na hali halisi ya maisha yao ili waondokane na ugumu wa maisha?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sera ya Malipo ya Mishahara wa Motisha katika Utumishi wa Umma wa Mwaka 2010, Serikali inatambua kuwa wapo baadhi ya watumishi wanaofanya kazi kwenye maeneo yenye mazingira magumu, wakiwemo Walimu, Watumishi wa Kada za Afya, Watumishi wa Kada za Kilimo na kada nyingine. Katika kutekeleza sera hii, Serikali inazielekeza Halmashauri namna ya kuandaa miongozo watayoitumia kutoa motisha kwa watumishi wao wanaofanya kazi kwenye maeneo yenye mazingira magumu.

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]

Aidha, kwa kuwa aina za motisha zinatofautiana kati ya eneo moja na jingine kutegemea aina ya ugumu uliobainishwa, Halmashauri zimeelekezwa kuainisha idadi ya watumishi watakaohusika, aina ya motisha watakazostahili kupewa na utaratibu utakaotumika kutoa motisha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, motisha zitakazotolewa hazitakuwa za kifedha tu (posho), bali zitahusisha mahitaji mbalimbali yatakayosaidia kupunguza ugumu wa maisha katika maeneo husika, kama vile nishati mbadala, nyumba za kuishi na kuhakikisha huduma za jamii zinapatikana kwa urahisi.

Motisha hizo zimeshaanza na zitaendelea kutolewa. Kwa mfano ujenzi wa nyumba za wafanyakazi, ujenzi wa barabara vijijini, ujenzi wa minara ya simu, uwekaji wa nishati mbadala *(solar power)*, ununuzi wa boti katika mazingira yenye visiwa kama vile Rufiji, Kigoma, Muleba, Rudewa, Sengerema na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuzipongeza baadhi ya Halmashauyri za Wilaya kama vile Iramba, ambazo tayari zimeanza kutekeleza utaratibu huu, hususan kwa kada ya afya.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kupanga mishahara kwa watumishi wa Umma, wakiwemo Walimu kwa kuzingatia kuongezeka kwa tija na hali ya uchumi wa nchi, kwani uchumi ukitengemaa na mishahara inaongezeka.

MHE. ANNE KILANGO MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Diana Chilolo, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mwalimu, kwa hiyo nafahamu vizuri hali halisi ya Walimu. *(Makofi)*

[MHE. ANNE KILANGO MALECELA]

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Walimu wote kuanzia Shule za Msingi mpaka Chuo Kikuu, wanafanya kazi muda wa ziada kwa sababu baada ya kazi inabidi wasahihishe madaftari na watayarishe masomo kwa kesho yake. Kwa hiyo, Walimu wanafanya kazi zaidi ya muda ambao unastahili.

Je, Serikali haioni kwamba waliangalie hilo vizuri na kuwapa mshahara kulingana na muda wa kazi wanaotumia kufanya kazi yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kutokana na jibu la Serikali, inaonekana kwamba sasa jukumu hili linatupiwa Halmashauri zetu wakati tunajua ni pesa kiasi gani zinazopelekwa kwenye Halmashauri hizi.

Je, Serikali imepeleka fungu maalum kwenye Halmashauri na kusema kwamba hili ni kwa ajili ya motisha ya Walimu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Walimu wanafanya kazi katika mazingira tofauti na watumishi wengine na wakati wa kupanga mishahara, hayo yote yanazingatiwa. Tunaangalia Madaktari kwa mazingira yao, Wauguzi kwa mazingira yao, Walimu kwa mazingira yao na watumishi wa kada nyingine kwa mazingira yao. Kwa hiyo, suala la kupanga mishahara kutegemea na aina ya kazi linazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuwaachia Halmashauri, mwongozo kwa mujibu wa sera iliyopo, Serikali Kuu inao wajibu wa kutoa motisha na pia Serikali za Mitaa na zenyewe zinao wajibu, zimeelekezwa kutoa motisha kulingana na uwezo wake ilio nao.

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Serikali katika Bajeti ya mwaka huu tumetoa shilingi milioni 500 kwa zaidi ya Halmashauri 38 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Watumishi katika Halmashauri mbalimbali. Hata tulivyozungumzia suala la kununua boti, ni suala la Serikali Kuu. Kwa hiyo, Serikali Kuu na Halmashauri kwa pamoja tushirikiane.

Tunachofanya, tumetoa miongozo. Kwa sababu yapo yale madogo madogo ambayo Halmashauri ina uwezo wa kufanya na zipo Halmashauri kwa mfano Mikoa ya Kigoma na Rukwa wanatoa. Sasa ili kuwazuia wasiwe wanafanya kazi ya kila siku kuomba kibali, tumetoa miongozo ya kuwaelekeza. Pale ambapo hali inawaruhusu, basi watoe motisha.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nimwulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Walimu katika maeneo mbalimbali nchini wanakabiliwa na changamoto zifuatazo:- Wanadai fedha za uhamisho, wanadai hawapandishwi madaraja.

Kutokupandishwa madaraja ni moja ya tatizo ambalo ni sugu ikiwemo Walimu wanaofanya kazi katika Halmashauri yangu (Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu). Lakini pia Walimu wanakabiliwa na tatizo la kupuuzwa na baadhi ya Watendaji (viongozi wao) kama vile Maafisa Elimu. Inaonekana kwamba Serikali wakati mwingine ni kama inawakumbatia.

Ningependa kupata kauli ya Serikali, ni lini Serikali itaacha kuwapuuza Walimu na hatimaye Walimu wamekata tamaa, wanashindwa kuweza kufanya kazi kwa sababu wanaona kama vile wameachwa nyuma? Naomba kauli ya Serikali.

NAIBU SPIKA: Kuwapuuza katika jambo gani hasa?

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza wanapuuzwa. Kwa mfano hawapandishwi madaraja kwa wakati kama ambavyo inavyotakiwa. Ukiangalia fedha za uhamisho, fedha za matibabu; ni matatizo. Na *case study* naomba niseme ni *site* ya Halmashauri yangu ya Wilaya ya Kasulu, maeneo mengine wanaandika *message,* wanapiga simu. Serikali inatoa kauli gani katika kutatua kero hizi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Moses Machali kama ifuavyo:-

Kwanza, si kweli kwamba Serikali inawapuuza Walimu au Watumishi wake. Ni mara nyingi Serikali imekuwa ikilipa madai ya Walimu na mara ya mwisho mwezi wa 8 mwaka huu Madai ya Walimu yamelipwa na pia tumefanya uhakiki mwingine na sasa hivi tuko mbioni kulipa madai ya Walimu. Tena ukiangalia, Madai ya Walimu yamekuwa yakilipwa mara kwa mara kuliko hata Watumishi wengine ambao sio Walimu.

Kama ungekuwa unafuatilia maslahi ya Watumishi wengine ukiachilia Walimu, nadhani ungekubaliana na mimi kwamba Walimu tunawajali zaidi kuliko Watumishi wengine. Kwa sababu tumeshalipa zaidi ya mara 4 madai ya Walimu, wakati Watumishi wengine hatujawalipa hata mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la kwamba Walimu hawapandishwi madaraja na kwamba Maafisa Elimu wanawanyanyasa. Ikumbukwe kwamba Maafisa Elimu na wenyewe pia ni Walimu. Na mara nyingi sisi tumekuwa tukiwasema, na hata mimi nilipokuwa Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) tuliamua kabisa. Kwa sababu hata waliokuwa Maafisa wetu upande wa *TSD* walikuwa ni Walimu, tuliamua kubadilisha na kuwaweka

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]
Maafisa Utumishi kwa sababu baada ya kuona kwamba Walimu walioko ndani wanawagandamiza wenzao.

Labda, Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Machali kwa kuwa yeye ni Mwalimu, kuna siri gani kwa wenzetu huko Ualimu kwamba wenyewe kwa wenyewe wananyanyasana. Kwa sababu Afisa Elimu ni Mwalimu, Mratibu Elimu Kata ni Mwalimu.

Lakini kila Mwalimu anapopanda madaraja unakuta anamkandamiza mwenzake. Labda anisaidie ili tuweze kuwafanya Maafisa Elimu wajione wao wenyewe ni Walimu na watetee maslahi ya Walimu wenzao. (Makofi)

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, nami nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya mwaka jana ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tulipitisha hapa Sh. 500,000/= kwa kila Mwalimu ambaye anakwenda kufanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda ni-*declare interest*, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu huwa inakuja kwetu.

Maelezo ambayo yalitolewa kuhusu zile fedha yamekuwa yakijichanganya. Mara sijui zimekwenda wapi, mara zimejenga nyumba, mara zimenunua fenicha kwenye nyumba za Walimu; wakati hakuna nyumba za Walimu kwenye vijiji au kwenye vijiji au kwenye vijiji ambavyo Walimu wanafanya kazi, nyumba za Walimu hazipo. Sasa nataka kuuliza, hizo laki tano ambazo tulizipitisha hapa kwenye Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa nini zimetumika vinginevyo bila kwanza Wizara kuja kusema hapa imebadilisha matumizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Christowaja Mtinda, kama ifuatavyo:-

Katiba Bajeti ya mwaka 2011/2012 tulipitisha pesa za jumla ya shilingi laki tano kwa Walimu ambao wangeripoti shuleni (Walimu wapya) katika Halmashauri zile ambazo zimetambulika kama Halmashauri zenye mazingira magumu.

Pesa hizi ni za wahisani (Benki ya Dunia). Kwa sababu ya hali halisi iliyokuwa kipindi kile kwamba katika shule zile au Halmashauri zile ambazo zimetambulika kama Halmashauri zenye mazingira magumu, tayari kulikuwa na Walimu ambao wameripoti mwaka uliopita na miaka mingine, ambao hawakupata posho ya kuripoti kwenye mazingira magumu, ikaingia kitendawili au ugumu kwa Serikali kuwapa hao wapya wakati wale waliotangulia hawana posho hiyo. Posho ya mara moja tu imetolewa na wafadhili, hakuna posho ambayo ingeendelea kwa mwaka unaofuatia na mwaka unaofuatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali baada ya kuzingatia kuwa kulikuwa na walimu wengine waliokuwepo pale na watumishi wengine wa Serikali walioko kweye Halmashauri hiyo hiyo.

Kwa kifupi niseme kwamba kutokana na mazingira hayo tofauti ambayo yamekuwepo, Serikali ilishindwa kutumia fedha hizo za mfadhili za mara moja tu. Bali tumependekeza kwa *World Bank* matumizi mengine ambayo yatahusiana katika kurekebisha miundombinu katika Halmashauri zile husika ili tutende haki kwa watumishi wote.

Na. 58

Ukosefu wa Nguvukazi yenye Ujuzi

MHE. JUMA SURURU JUMA (K.n.y. MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA) aliuliza:-

Mojawapo ya vikwazo katika utekelezaji wa malengo ya *Milenis (MDGs)* ni ukosefu wa nguvukazi iliyo na ujuzi *(Skilled Manpower):-*

Je, Serikali ina mipango gani ya muda mfupi, kati na muda mrefu katika kuondokana na kikwazo hiki ambacho pamoja na misaada mingi ya Wajhisani, bado Taifa letu linahesabiwa kuwa maskini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mojawapo ya vikwazo katika utekelezaji wa Malengo ya Milenia ni ukosefu wa nguvukazi iliyo na ujuzi *(Skilled Manpower).* Hata hivyo, ili kuondokana na kikwazo hiki, Serikali imekuwa na mipango mbalimbali ya muda mrefu na muda mfupi ya kuimarisha Elimu na Ujuzi katika maeneo yanayohitajika kutimiza malengo ya milennia. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imekuwa ikitekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari (MMEM na MMES) uliyokusudia kutoa nafasi kwa Watanzania wengi kupata Elimu bora.

Kwa kuzingatia mipango hiyo, uandikishaji wa wanafunzi katika Shule za Msingi uliongezeka kutoka 8,247,172 mwaka 2008 na kufikia 8,410,094 mwaka 2012. Watoto walioandikishwa Elimu ya Sekondari waliongezeka kutoka 1,222,403 hadi 1,884,272 katika kipindi hicho.

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Afya, udahili wa wanafunzi katika Vyuo vya Afya umeongezeka kutoka wanafunzi 7,458 mwaka 2011/2012 hadi 7,956 mwaka 2012/2013. Hadi sasa Wizara imefikia asilimia 80% ya lengo na kudahili wastani wa wanafunzi 10,000 kwa mwaka ifikapo 2017. Kwa hiyo, kati ya malengo ya milennia, nchi yetu imefanya vizuri sana kwa upande wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hatua ya muda mrefu, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, zinafanya uchambuzi wa kubainisha mahitaji ya Watendaji *(Skills Gap Analysis)* katika maeneo ya kipaumbele ya kitaifa yaliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa *(TLTPP)* ili kuiwezesha Serikali kupata wataalam wa kutosha. *(Makofi)*

MHE. JUMA SURURU JUMA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza swali moja tu. Je, ni lini kazi ya uchambuzi itakamilika kutekelezwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) na Tume ya Mipango, inafanya uchambuzi ambao siwezi kusema leo kwamba ni lini; lakini nina uhakika ndani ya mwaka huu utakamilika, ili kuweza sasa kujaza hayo mapengo ambayo yatabainika.

Na. 59

Mawasiliano ya Simu – Kata za Katuma na Sibwesa

MHE. MOSHI SELEMANI KAKOSO aliuliza:-

Mawasiliano ya simu katika Kata za Katuma na Sibwesa ni ya muhimu sana kwa wananchi wa maeneo hayo:-

Je, kwa nini mpaka sasa mipango ya kuweka minara ya Mawasiliano katika Kata hizo imekuwa ya kusuasua?

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa eneo kubwa katika Jimbo la Mpanda Vijijini halina huduma ya mawasiliano ya simu za mkononi zikiwemo Kata za Katuma na Sibwesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo changamoto nyingi zinazosababisha Kampuni za Simu kusita kupeleka mawasiliano katika maeneo mbalimbali ikiwemo mvuto mdogo wa kibiashara katika eneo husika.

Aidha, sababu zinazopunguza mvuto wa kibiashara ni pamoja na hali za kijiografia, yaani wingi wa milima na mabonde, misitu na kuwepo kwa idadi ndogo ya watu katika eneo husika.

Katika kukabiliana na changamoto hizi, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ambao una lengo la kufikisha mawasiliano hususan katika maeneo ya vijijini, umeyaainisha maeneo yenye hali halisi na kuyaweka katika mpango wa kufadhili upelekaji wa mawasiliano ambapo maeneo ya Vijiji vya Kata za Katuma na Sibwesa yapo katika Zabuni ya awamu ya kwanza B *(Phase 1B)* ya mpango huo unaogharamiwa na Serikali ya Tanzania kupitia fedha za ndani *(Service Levy).* Mradi huu unategemewa kutangazwa mwishoni mwa mwaka huu wa fedha, yaani 2013/2014.

Aidha, Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Ikola itapelekewa mawasiliano kupitia Kampuni ya Simu ya Airtel baada ya kampuni hiyo kushinda katika zabuni na kusaini mikataba tarehe 8 Machi, 2013 kwa thamani ya Dola za Kimarekani 167,580 sawa na shilingi za Kitanzania milioni 261.13.

[WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA]

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuzipongeza na kuzishukuru Kampuni za Simu za Mkononi za *TTCL, TIGO, AIRTEL* na *VODACOM* zilizoshinda zabuni. Aidha, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, Halmashauri na Wananchi kwa ujumla kuzipa kila aina ya ushirikiano ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na ili wananchi wa maeneo hayo waondokane na adha ya kukosa mawasiliano na wajumuike pamoja na wenzao kunufaika na Teknolojia ya Habati na Mawasiliano. *(Makofi)*

MHE. MOSHI SELEMANI KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa Kata ya Katuma na Kata ya Sibwesa kuna tatizo kubwa sana la mawasiliano na limechukua muda mrefu, nilikuwa napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri anithibitishie:-

(1) Je, ni kiasi gani ambacho kimetengwa cha fedha zitakazotumika kujenga minara katika Kata hizo mbili?

(2) Waziri atakubali kuamabatana na mimi kwenda katika maeneo husika ili ajionee adha wanayoipata wananchi wa kata hizo?

NAIBU SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa.

WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba Kata ya Katuma tumeiweka kwenye awamu ya kwanza B ambayo itatangazwa mwishoni mwa mwaka huu wa fedha na tumetenga jumla ya shilingi milioni 420 kwa ajili ya kupeleka mawasiliano kwenye Kata hizo.

Pia niko tayari kwenda kutembelea eneo hilo ili kuona hali halisi, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatailia mawasiliano kwenye Kata zake. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Swali lina waulizaji wengi kweli, Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Blandes.

MHE. GODBLESS J. LEMA, Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Serikali ilipopitisha Sheria ya usajili wa namba za Simu ilikuwa na maana pana ikiwa ni pamoja na kudhibiti uhalifu, meseji zinazosambazwa, mambo kadha wa kadha, udini na ukabila na mambo mengine.

Lakini mpaka sasa usajili wa laini za simu umekuwa ukifanyika katika sura ya Kimachinga sana kwamba mtu anaweza akasajili namba ya simu kwa jina la mtu, ama unaweza ukasajiri namba ya simu nyingine ukiwa umekaa baa au ukiwa umekaa hotelini na inaendelea kuleta madhara makubwa sana kama usambazaji wa meseji kama hizo.

Je, Serikali inasema nini juu ya jambo hilo ambalo kwa kweli lina athari kubwa sana ukizingatia kwamba kama swala hilo lisipozibitiwa kwa makini.

WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu swali lake la nyongeza, Mheshimiwa Lema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la usajili wa namba za simu liko kisheria na linafanywa kisheria na mpaka sasa hivi linafanywa kisheria na mpaka sasa hivi unaendelea vizuri na kuna sheria ambayo imewekwa kisheria mtu yoyote atakayesajili kwa kutumia jina bandia ama kusajiliwa na mtu mwingine atapata adhabu ya hukumu ya kifungo cha miezi 6 ama faini kama sheria inavyosema.

NAIBU SPIKA:Mheshimwa Blandes swali la mwisho.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu spika, nakushukuru, Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba nimekuwa nikufuatilia sana kwa karibu kwa maandishi, kuzungumza naye kuhusiana na matatizo ya mawasiliano ya minara ya simu katika Kata ya Bweranyange Karagwe, Kata ya Nyakabanga, Kata ya Nyakakika, Kata ya Rugu na Kata ya Rugela na nimekuwa nikipata maelezo ya Serikali kwamba shughuli hiyo ya Ujenzi wa minara itaanza mara moja huu ni mwaka karibu wa nne.

Ningetaka kujua shughuli ya kupeleka mawasiliano katika Kata hizi itaanza lini na inaisha lini?

NAIBU SPIKA: Majibu hayo ya lini Mhe. Prof. Makame Mbawara, Waziri wa Mawasiliano Sayansi na Teknolojia.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Blandes, kama ifuatavyo:-

Ni kweli Mheshimiwa Blandes ameendelea kufuatilia kwa makini na namshukuru sana kwa kufanya kazi hiyo, vijiji vyake tumeviweka kwenye *phase* mbili tofauti, baadhi ya vijiji tumeviweka kwenye *phase* 1 (a) ambayo tumeshatangaza na *phase* nyingine tutaitangaza mwisho wa mwaka kwa ajili ya *phase two* kwa ajili ya Vijiji vyake lakini viko na tunavifuatilia kwa karibu. Mheshimiwa uwe na amani Vijiji vyako vitapata mawasiliano tu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tunaendelea,Waheshimiwa Wabunge, na swali linalofuata la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi Mbunge wa Lulindi, kwa niaba yake Mheshimiwa Mariam Kasembe.

Na. 60

Tatizo la Mawasiliano ya Simu Vijiji vya Jimbo la Lulindi.

MHE. MARIAM R. KASEMBE (K.n.y. MHE. JEROME D. BWANAUSI) atauliza:-

Kumekuwa na tatizo la mawasiliano ya simu katika Kata ya Chiwata, Mkundi, Mkululu, Chikolopola, Sindano na Lipumburu, licha ya ahadi ya muda mrefu.

Je, utekelezaji wa ahadi hiyo umefikia wapi ili wananchi wapate huduma hiyo?

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Serikali kupitia mfuko wa Mawasiliano kwa wote kwa dhati kabisa imeendelea na utekelezaji wa ahadi yake ya kufikisha mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo maeneo ya Jimbo la Lulindi. Sanjari na utekelezaji huo, mfuko wa mawasiliano kwa wote umekamilisha zoezi la kuyaainisha maeneo mbalimbali kwa kuzingatia vigezo vya idadi ya wakazi, ukubwa wa Kata, Kiwango cha mawasiliano na ruzuku inayotakiwa.

Aidha mfuko huo uliingiza Kata ya Lipumburu katika Zabuni ya awamu ya kwanza yaani *(WB Phase 1)* iliyotangazwa na kisha mikataba kusainiwa ambapo Kampuni ya simu ya *TTCL* ilishinda Zabuni ya kupeleka mawasiliano katika Kata hiyo kwa ruzuku ya kiasi cha shilingi. 150 millioni. Utekelezaji wa mradi huu unaendelea vyema baada ya *TTCL* kukamilisha taratibu za manunuzi tayari kwa kuanza ujenzi.

Aidha, Kata ya Sindano iliainishwa na kuingizwa katika Zabuni ya Awamu ya Kwanza A *(WB Phase 1A)* iliyotangazwa Julai, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kata ya Chitawa na Mkuluku, tayari Mfuko wa Mawasiliano kwa wote umeziingiza Kata hizo katika taratibu za Zabuni ya awamu ya kwanza B *(UCSAF Phase 1B)* inayotarajiwa kutangazwa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Aidha Kata ya Mkundi itaingizwa katika zabuni ya awamu ya pili *(WB Phase 2)* itakayotangazwa mwaka ujao wa fedha, yaani 2014/2015.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam Kasembe swali la nyongeza.

MHE: MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda niishukuru Serikali kwa sababu wamenza kutekeleza mradi huu katika Jimbo la Lulindi na vijiji vilivyotajwa lakini Mheshimiwa Spika kwa kuwa *TTCL* wamekuwa wakichelewa sana kufanya kazi zao pale wanapopata Zabuni.

Je, Serikali iko tayari kuisimamia *TTCL* ili iweze kuharakisha miradi hii katika Vijiji vya Jimbo la Lulindi ili wananchi waweze kuondokana na adha ya kubwa waliyonayo ya mawasiliano.

Wakati wa maandalizi ya Bajeti iliyopita, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano alitutaka Waheshimiwa Wabunge kupeleka Vijiji vyetu ambavyo havina mawasiliano. Mimi kama Mbunge wa Jimbo la Masasi nilipeleka Vijiji vya Kata ya Lukuledi, Mlingura, Mwenge, Chiwale, Nanganga, Sululu na Mwenge Mtapika. Vijiji ambavyo hadi sasa Wananchi hawajapata mawasiliano.

[MHE. MARIAM R. KASEMBE]

Je, Mheshimiwa Waziri lile swala ambalo mlituhimiza tulete vijiji ambavyo havina mawasiliano utekelezaji wake hadi hivi sasa ukoje?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kasembe hata mimi nilipeleka Vijiji vya Kongwa na mpaka leo hamna Kitu, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, zile orodha za Waheshimiwa Wabunge majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo.

Ni kweli *TTCL* tumeipa hii kazi na *TTCL* tumewekeana huu mkataba na tunaifuatilia kwa makini sana, kwa vile kwenye suala hii hakuna suala la kuchelewa na tunaamini kwamba *TTCL* ni Kampuni yetu na ina uwezo wa kufanya kazi hii.

Pili, kuhusu Vijiji ambavyo tuliwataka Waheshimiwa Wabunge ili watupatie vijiji hivyo ni kweli Vijiji hivyo tunavyo na tumevigawa katika sehemu mbalimbali ama awamu mbalimbali, baadhi ya Vijiji vitakuweko ama vimetangazwa kwenye *Phase 1 A*, ambayo imetangazwa mwezi Julai, 2013 na baadhi ya Vijiji vitatangazwa kwenye *Phase 1B* ambavyo vitatangazwa mwisho wa mwaka huu wa fedha na baadhi ya Vijiji vitatangazwa kwenye *phase two,* sasa nitaileta tena *list* ile kwamba kila Mbunge aone Vijiji vyake viko katika awamu gani na wakati gani vimepangiwa kupata mawasiliano.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Zabein Mhita.

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana kwa kuniona, katika Bunge la Bajeti lililopita nilichangia kwa uchungu mkubwa sana kuhusu tatizo la mawasiliano katika Wilaya ya Kondoa, katika majibu ya Naibu Waziri na Waziri wote kwa pamoja walinipa pole na wakaahidi kwamba watalishughulikia tatizo hilo.

[MHE. ZABEIN M. MHITA]

Mheshimiwa Naibu Spika, ile pole niliyopewa na Naibu Waziri na Waziri mimi nilidhani ingeongeza uharaka na kasi ya kushughulikia tatizo hilo, lakini mpaka sasa Mheshimiwa Naibu Spika hakuna kilichofanyika .

Je, Serikali sasa Serikali inatoa tamko gani kuhusu tatizo hili sugu linaloleta adha kubwa kwa Wananchi wa Wilaya ya Kondoa na kuhusu pole waliyonipa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Profesa unalikumbuka vizuri kabisa suala la Kondoa, majibu tafadhali.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nalikumbuka vizuri na naendelea tena kumpa pole ni suala ambalo kwa kweli hata sisi kama Serikali linatugusa sana sana na tunalifanyia kazi.

Napenda tu nikujibu kwamba Mheshimiwa Vijiji vyako tumeviweka kwenye awamu tofauti, awamu ya kwanza *Phase One* kuna kijiji chako kimoja ambacho sasa hivi kazi imeanza kufanywa, Vijiji vingine viko kwenye awamu ya 1A na Vijiji vingine viko kwenye awamu ya 1B, lakini naomba Mheshimiwa Mbunge uelewe kwamba kupeleka mawasiliano inachukua kama miezi 6 toka mchakato kuanza mpaka mawasiliano kufikishwa pale.

Kwa sababu kwanza ni muhimu lazima wale wajenga minara watafute eneo wakishatafuta eneo waagize vifaa, kwa vile utaratibu wenyewe unachukua muda mrefu kawaida miezi 5 mpaka miezi 6. Naomba Mheshimiwa usubiri tu lakini tutahakikisha kwamba maeneo yako yote yatapata mawasiliano.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea Wabunge na Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi, Swali linaulizwa na Mheshimiwa Anna Merystella John Mallac, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 61

Hali ya Gereza la Mahabusu Mpanda.

MHE. ANNA MARYSTELLA MALLAC aliuliza:-

Gereza la Mahabusu Mpanda lina vyumba vinne vya kulaza mahabusu kila chumba kikiwa na uwezo wa kulaza mahabusu 21 tu, na vyumba viwili vya selo na vyumba viwili vya wanawake lakini hali ya gereza hilo limechakaa sana na wanalaza mahabusu 50 kwa kila chumba.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vyumba vingine kukabiliana na hali ya msongamano wa mahabusu uliopo sasa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani pia wa kuzikarabati nyumba za askari ambazo zimechakaa katika hali ya kutisha?

(c) Je, Serikali pia ina mpango gani wa kutatua kero ya maji katika gereza hilo ambalo linategemea kisima kimoja tu na pale kinapokauka huwalazimu wafungwa kwenda mbali kutafuta maji?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Marystella Mallac, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua matatizo ya ufinyu wa nafasi uliopo Magerezani nchini kote, likiwemo Gereza la Mahabusu Mpanda. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali kupitia Jeshi la Magereza imekuwa ikitatua tatizo hili kwa awamu kwa kufanya ukarabati na kupanua Magereza ya zamani, kukamilisha Magereza ambayo ujenzi wake haujakamilika na kujenga Magereza mapya kwenye Wilaya zisizokuwa na Magereza.

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Mpango wa miaka kumi na mitano (15) wa kuboresha hali ya Magereza nchini, Gereza la Mahabusu Mpanda ni miongoni mwa Magereza yatakayofanyiwa ukarabati na upanuzi katika mwaka ujao wa fedha 2014/2015. Kukamilika kwa ukarabati huu utatoa nafasi ya kutosha ya kulaza wafungwa na hivyo kupunguza msongamano uliopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba za askari unaendelea na kulingana na hali ya kifedha, kwa kutumia rasilimali zilizopo katika kituo hicho, Uongozi wa Magereza tayari umeweza kujenga nyumba moja ya kisasa kwa njia ya ubunifu za kuishi familia mbili. Kwa sasa nyumba hiyo imefikia hatua ya Linta na tayari Makao Makuu wameshatoa mabo kwa ajili ya maandalizi ya kuiezeka. Ukarabati wa nyumba za Askari unafanywa mara ya hali ya fedha itakaporuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza linao utaratibu wa kutoa huduma za maji kwa kujenga na kukarabati mifumo ya Maji safi na Maji taka katika Magereza yote nchini. Ni nia ya Serikali kuhakikisha kuwa Gereza la Mpanda litapata maji safi yaliyo salama katika mwaka ujao wa fedha2014/2015.

NAIBU SPIKA: Kuna nini jamani! Mheshimiwa Leticia Nyerere, swali la nyongeza.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la msongamano la Mpanda ni sawa kabisa na tatizo la msongamano la Gereza la Ngudu Kwimba. Mheshimiwa Naibu Spika nilipotembelea gereza la Ngudu nilitokwa na machozi nilipokuta kuna msongamano wa kutisha wakiwemo wakina mama wenye watoto wachanga ambao wanachanganyika na mahabusu na wafungwa.

[MHE. LETICIA M. NYERERE]

Ni kwa nini Serikali isitumie gereza la Mallya ambalo haliko mbali sana kutoka Ngudu kwa ajili ya wafungwa na ikaacha gereza la Ngudu kwa ajili ya Mahabusu?

Kwa kuwa, jambo la kuwachanganya akina mama wanaonyonyesha watoto wachanga na wafungwa ni ukiukwaji wa haki za binadamu.

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kuwajengea akina mama ambao wanatokea kujifungua wakiwa mahabusu au wakiwa jela kuwajengea sehemu zao na kuwapatia mahitaji yao ya lazima wakiwa na watoto wachanga?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Pereira Silima.

NAIBU WAZIRI WA MANDO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Leticia Nyerere, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Tanzania nzima ina mlundikano mkubwa wa wafungwa kuliko *Capacity* ambayo tunayo magerezani, hata hivyo mwaka 2010 mlundikano huu ulikuwa unafikia jumla ya wafunga na mahabusu 40 elfu na sasa tumebakisha 34 elfu, bado ni wengi na bado tunaendelea kuchukua hatua za upanuzi lakini kubwa zaidi ni kuhakikisha kwamba wale ambao wanakuwepo na si lazima wabaki magerezani wanatoka haraka.

Hii inajumuisha kushughulikia sheria, kushughulikia dhamana na mambo mengine kama haya. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge nyote mliosimama ambao hamkupata nafasi kwa hili kwamba tunalishughulikia na msongamano huu utapungua haraka iwezekanavyo.

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya kutumia gereza ambalo liko karibu na Ngudu yaani kutumia gereza la Mallya hili nalichukua na tutalitizama ubora wake na mafanikio yake au gharama au na mambo mengine ili tuone ufanisi utakuwaje.

Kuhusu kuchanganywa akina mama wenye watoto hili swali hivi sasa tunalifanyia kazi na tukimaliza basi tunaliona kwamba sio zuri na akina mama wenye watoto na watoto hawatachanganyika na wafungwa wengine. *Ishallah! (Makofi)*

NAIBU SPIKA: Hili swali maarufu kweli, Mheshimiwa Vincent Nyerere.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante kwa kuwa wote tulioko hapa ni wafungwa watarajiwa na nguo wanazovaa wafungwa hasa wa gereza la Musoma limechakaa zina hali mbaya imefikia hatua Wafungwa wanaofanya kazi za nje wanashindwa kupangiwa kazi za nje kwa sababu wanakwenda nusu uchi.

Je, Waziri yuko tayari kujitengenezea mazingira mazuri ya kuwapa wafungwa nguo nzuri ili hata yeye akienda asipate aibu wanayopata wengine.

NAIBU SPIKA: Majibu kwa ufupi Mheshimiwa Waziri, swali lako lina Wabunge wengi sana wanataka kuuliza maswali ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA MANDO YA NDANI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Nyerere, sasa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa mimi nimefika gereza la Tarime na nimeona tatizo hili, ni kweli kwamba taarifa niliyopewa pale ni kwamba wafungwa wale ambao walitakiwa wazalishe hawazalishi kwa sababu ya tatizo la sare.

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

Tatizo hili tukalichukua na tunalifanyia kazi na hivi karibuni watapewa nguo hizo ili tuweze kuwatumia na kuwarekebisha vizuri ili waweze kutoka kule wawe wanajamii ambao wanaweza kuishi na sisi, na labda niseme tu kwa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu maswali ya nyongeza yasingetosha lakini niwaambie Waheshimiwa Wabunge tatizo la msingi hapa kwenye magereza ni ufinyu wa Bajeti. Unaanzia kwenye chakula, kwenye nguo, kwenye majengo, kwenye *infrastructure* kama mlivyoinuka kwa wingi inukeni kuhakikisha kwamba mnaongeza Bajeti kwenye magereza ili tuweze kuondoa matatizo yaliyopo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, swali la nyongeza.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, Ansante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu spika, katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusiana na gereza lililoko Mpanda ni kwamba Serikali ina mpango wa kukarabati yale majengo yaliyoko pale ili waweze kuona wanawasaidiaje wafungwa walioko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba tu nimweleze Mheshimiwa Waziri kwamba, gereza la Mpanda lile liko pale mjini ni gereza dogo, sasa nimshauri kwamba ili pale pawe na mazingira bora na ili tuweze kutumia Wafungwa wetu vizuri katika shughuli za uzalishaji na kwa sababu Katavi ni Mkoa ambao una eneo kubwa la Kilimo ni vema sasa Serikali ikaangalia namna ambavyo inaweza ikapata eneo kubwa la kuweza kuwatumia wafungwa wale vizuri katika shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ushauri Waziri afanye hivyo. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Unaupokea ushauri huo Mheshimiwa Waziri kifupi, majibu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikubaliane na ushauri wake kwamba tutalifanyia kazi hilo.

Hata hivyo naomba nami nimshauri kwamba kwenye Wilaya kunakuwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ambayo ni chanzo cha kupanga mipango kipi kifanyike vipi na kipi kifanyike vipi, wakati sisi tunalichukua Wizarani basi asaidie kule kwenye Halmashauri kuweka mazingira mazuri ili tukifika kule iwe suala hilo linaweza likakubalika kwa kupatiwa maeneo mbadala.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa nawaoneni lakini kwa sababu ya muda basi upendeleo maalum Kamishna Mheshimiwa Mbunge wa Kasulu, swali la nyongeza la mwisho kabisa.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii. Kwanza naomba nimshukuru Naibu Waziri kwa ziara aliyoifanya Wilaya ya Kasulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo Magereza mengi ambayo yamejengwa na Mkoloni likiwemo gereza la Wilaya ya Kasulu. Kwa kuwa limejengwa na Mkoloni na alifika akaliona liko katikati ya mji kabisa.

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kutoa fedha ili kubomoa magereza yote yaliyojengwa na Mkoloni na kujenga magereza ndani ya uhuru wa miaka 50. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa Wizara ya Mifugo na Uvuvi suala la Mheshimiwa Mariba Chacha Nyangwine.

Ahaa!!! Mheshimiwa tafadhali majibu. Maji yamezidi unga?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba tunafanya mpango wa maboresho ya Magereza na mpango huu ambao tunakaribia kuumalizia utazingatia mambo kama haya.

Lakini tujue tu kwamba kazi ya kubadilisha magereza yote itakuwa kubwa kwa sababu itahitaji rasilimali fedha ambazo kwa haraka hatutazipata isipokuwa pale ambapo kuna matatizo makubwa tutatoa kipaumbele ili tuweze kumaliza tatizo hilo. *(Makofi)*

Na. 62

Kutenga Maeneo ya Wafugaji Nchini

MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MHE. NYAMBARI CHACHA M. NYANGWINE) aliuliza:-

Migogoro kati ya wakulima na wafugaji imekithiri sana na kutishia hali ya amani na usalama nchini:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya hali hiyo?

(b) Je, kwa nini Serikali haitengi maeneo ya wafugaji na kuwapatia Hatimiliki ya ardhi hiyo?

(c) Je, kwa nini Serikali haiwapi wafugaji ardhi ya mapori tengefu ambayo hayana wanyama?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chacha Nyambari Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji kuhama kwenda eneo moja kwenda eneo lingine ni kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na upungufu wa malisho na maji, kukimbia majanga kama vile magonjwa ya mifugo na kufuata huduma za kijamii kama vile shule na hospitali. Uhamaji huu mara nyingi husababisha migogoro na kuleta madhara makubwa ikiwa ni pamoja na uharibifu na upotevu wa mali pamoja na maisha ya watu.

Serikali haifurahishwi na matukio ya aina hii, hivyo inasisitiza wafugaji na wakulima kuzingatia Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007 na Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali ya Vyakula vya Mifugo Na. 13 ya mwaka 2010. Serikali inawahimiza na kuwakumbusha wafugaji kuzingatia kufuga mifugo kulingana na maeneo waliyonayo ambayo yameainishwa.

Aidha, wafugaji wanatakiwa kuzingatia ufugaji wenye tija, unaoendeshwa kibiashara na kuzingatia hifadhi ya mazingira ambayo itawezesha kuboresha maisha yao na kuongeza pato la Taifa kwa ujumla.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hutenga maeneo ya wafugaji katika kutekeleza zoezi la kupanga matumizi ya ardhi. Hadi sasa jumla ya vijiji 543 katika Wilaya 75 mikoa 21 zimetengwa jumla ya hekta milioni 1.35 kwa ajili ya malisho.

Maeneo haya yaliyopimwa na kutengwa yanalindwa kisheria kupitia Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo Na. 13 ya mwaka 2010. Serikali inaendelea na jitihada zake za kutenga na kupima maeneo

kwa ajili ya ufugaji kupitia mipango ya matumizi bora ya ardhi kulingana na upatikanaji wa fedha.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Pori Tengefu (*Game Controlled Area)* huanzishwa na kulindwa na Sheria ya Hifadhi za Wanyama Pori Na. 5 ya mwaka 2009. Sheria husika inakataza matumizi mengine yeyote zaidi ya uhifadhi.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Katika swali la msingi sehemu ya (b) Mheshimiwa Mariba Nyangwine alitaka kujua je kwa nini Serikali haitengi maeneo ya ufugaji na kuwapatia Hatimiliki ya ardhi hiyo?

Mheshimiwa Waziri hajajibu swali hilo, tulitaka tujue kama Serikali inatenga maeneo kuwapatia watu Hatimiliki ya mashamba, vitalu vya madini, vitalu vya uwindaji kwa nini Serikali haitoi Hatimiliki ya ardhi kwa ajili ya wafugaji ili mfugaji akaweza kupanga mipango yake endelevu. Swali la kwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri wa Mifjugo anafahamu mgogoro wa muda mrefu sana ambao upo katika iliyokuwa ranchi ya Kitengule katika Wilaya ya Karagwe ambapo eneo hilo liligawiwa kwa wawekezaji wa aina mbalimbali, lakini vijiji vya Kishoju, Kianga, Mlamba, Katanda na Mushabaiguru hazikuweza kupatiwa eneo hata kidogo kwa ajili ya malisho ya mifugo yao.

Najua tatizo hili limeshapelekwa katika Baraza la Mawaziri, nilitaka kujua mgogoro huu unaisha lini ili wananchi hao wa vijiji hivi na wenyewe wapatiwe ardhi ya kutosha kwa ajili ya malisho na mifugo yao? Ahsante sana.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Blandes kwa kuwa mfugaji bora na mfugaji ambaye anafuata taratibu na mfugaji anayefuga kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo. Ni haki baada ya maeneo

kutengwa, kuainishwa na kupimwa ni haki kabisa na hatua ya mwisho ni kuwapatia wafugaji hao Hatimiliki ama Hati ya mfugaji mmoja mmoja ama Hati ya vikundi. Lakini ni haki yao wapate kusudi waweze kuendeleza. Kwa sababu hati hizi hizi zinatumika katika kupata mikopo benki kwa ajili ya kuendeleza ufugaji wake. Kwa hiyo, ni muhimu kupata hiyo Hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lake la pili kuhusiana na vijiji katika jimbo lake la Wilaya ya Karagwe hususan katika ranchi ya Kitengule. Utaratibu unaofanyika sasa hivi kwa sababu kumekuwa na ugomvi katika hizi ranchi za mkoa wa Kagera, ni kuhakikisha kwamba tunagawa upya maeneo haya. *(Makofi)*

Kwa hivyo vijiji hivi vina haki kabisa ya kupata maeneo lakini baada ya kumaliza mchakato wa kupima maeneo haya upya na kuwakabidhi wafugaji pamoja na vijiji, na vijiji vinapewa *priority* ya kwanza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Blandes wananchi wako uwahakikishie kwamba watapata eneo baada ya kupimwa upya.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama lakini nikagundua kwamba suala la migogoro ya wafugaji na wakulima liko kwenye Tume yako, kwa hiyo naomba kuondoa swali langu.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri ambaye amejibu kwamba kuna utaratibu unaendelea. Lakini naomba nimkumbushe Bajeti ya mwaka jana wakati anahutubia Bunge hili alisema kabisa kwamba *Block No. 3* katika Kata ya Kakunyu itarudi mikononi mwa wananchi, nimefanya ziara mara tatu wakinizuia mkutano kwa sababu hamna utekelezaji wowote unaoendelea ukizingatia kule kuna watu wameuawa, kuna watu wanateswa, kuna watu wanapigwa.

Naomba tu nijue huo utaratibu uliosema kufuta ni lini na itakuwa lini kwa sababu muda umepita sana?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikishatoa ahadi ni lazima itatekeleza. Lakini suala hili kwa sababu kuna wawekezaji pale, kuna wadau mbalimbali lakini vilevile kuna hatua mbalimbali ambazo zinatakiwa kuchukuliwa na *process* ambazo zinahusisha Wizara ya Ardhi ni lazima suala hili liende kwa utaratibu mzuri asije akaonewa mtu.

Ni lazima vikao na mikutano ifanyike ili wadau waweze kukubaliana vizuri. lakini ahadi ya Serikali iko pale pale maeneo haya yatapimwa upya kusudi kuweza kupunguza matatizo hayo ya migogoro ya ardhi katika eneo lake.

NAIBU SPIKA: Suala la mwisho Mheshimiwa Sanya nikukaribishe sana Bungeni baada ya kutokuwepo kwa muda mrefu Mheshimiwa Sanya. Karibu sana. *(Makofi)*

MHE. MUHAMMED IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe kwanza pamoja na Wabunge wenzangu wote kwa dua zenu na namshukuru Mola ilikuwa nimshukuru mwanzo namshukuru Mola na nawashukuru nyie kwa dua zenu na nimerudi salama na tuendelee na kazi zetu kama kawaida. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya kwamba Serikali inaandaa utaratibu wa kutenga maeneo ya wafugaji na kwa kuwa Tanzania ni nchi ya tatu au ya nne kwa kuwa na mifugo mingi katika Bara la Afrika.

Lakini bado maendeleo ya wafugaji yanasuasua na hatuna ufugaji wa kisasa, hatuoni kwamba Serikali sasa iende ikajifunze Botswana au Ethiopia ili kuwa na mifugo kidogo lakini inayozalisha na kuweza kusafirisha nyama kwenda nchi za nje kama wenzetu wanavyofanya badala ya kuwaachia hawa wafugaji wakatangatanga na kutembea Tanzania nzima bila ya kuwa na mafanikio wao na Serikali yetu?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumkumbusha kwamba Tanzania ni nchi ya tatu Afrika kwa mifugo mingi. Niseme kwamba asilimia 97 ya mifugo inayofugwa Tanzania inafugwa kwa njia ya kienyeji kwa njia ya kujali wingi kuliko kujali ubora. Ni asilimia 3 tu ambayo inafugwa kwa kuzingatia ubora na kuzingatia kanuni bora za ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ambayo yanatakiwa yafanyike ni pamoja na kutoa elimu. Elimu ya kubadilisha koo za mifugo kutokana na mifugo hii tuliyozoea mifugo midogo midogo tuweze kuleta koo ambazo zinazaa mifugo mikubwa lakini mifugo yenye nyama nyingi na maziwa mengi na mifugo michache. Hii ya kuwabadilisha Watanzania kutojali wingi tujali ubora ni suala ambalo linachukua muda kwa sababu wengi tunaangalia mila zinasemaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimwambia mtu punguza mifugo ana ng'ombe 10,000 ukimwambia punguza upate 500 ambayo ni bora ni shughuli ambayo inahitaji muda mrefu wa kuweza kuelimishana.

Lakini Serikali bado inaendelea kuhakikisha kwamba tunaongeza vituo vya uhimilishaji kusudi tuweze kupandisha ng'ombe zetu tuweze kuwa na ng'ombe bora, tunaendelea kuzalisha nyanda za malisho kusudi mifugo iweze kupata chakula bora, tunaendelea kusomesha maafisa ugani kusudi waweze kutoa utaalam mzuri wa ufugaji bora kwa wafugaji wetu. Mambo mengi ambayo Serikali inayatoa ni pamoja na kutoa ruzuku kuhakikisha kwamba magonjwa mbalimbali na baadhi ya maeneo yanakuwa ni *disease free zone.*

Lakini suala lingine pamoja na kuhamasisha ujenzi wa machinjio kusudi wafugaji waweze kupunguza mifugo yao na kuhakikishia kwamba wanafuga mifugo michache kwa mujibu wa sheria ambazo zipo. *(Makofi)*

Na. 63

Ujenzi wa Lambo Kijiji cha Nsango

MHE. AUGUSTINO M. MASELE aliuliza:-

Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori inazuia Mifugo kuingizwa katika Hifadhi za Wanyamapori:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa lambo la Kijiji cha Nsango ambalo Wizara ya Maliasili na Utalii iliahidi kulijenga kwa milioni sabini na tano (75,000,000/=) na tayari milioni ishirini na tano (25,000,000) zimekwisha tolewa?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009 Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe iliandaa andiko la mradi wa lambo la maji uliolenga kuwezesha mifugo iliyopo katika Kijiji cha Nsango, Kata ya Iponya kupata chanzo cha maji kinachoaminika ili kuzuia maingiliano kati ya mifugo na wanyamapori.

Gharama za mradi ilikadiriwa kuwa shilingi milioni sabini na tano (75,000,000) kwa mujibu wa usanifu wake. Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Shirika la Kimataifa la *World Wildlife Fund (WWF)* ilikubali kuchangia shilingi milioni ishirini na tano (25,000,000) ambazo tayari zimekwishatolewa. Aidha, katika makubaliano hayo kiasi kilichobaki cha shilingi milioni hamisini (50,000,000) kwa ajili ya ujenzi wa mradi kitatolewa na Halmashauri kupitia Bajeti ya Maendeleo na vyanzo vyake vingine vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 ujenzi wa tuta la lambo ulifanywa na Mkandarasi *Ms Jassam Co. Ltd.* wa Kahama kwa gharama ya shilingi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

27,230,829/= iliyojumuisha shilingi 25,000,000/= zilizotolewa na *WWF* na shilingi 2,230,892/= zilizotolewa na Halmashauri ya Wilaya. Kazi zilizobaki ni pamoja na ujenzi wa birika la kunyweshea mifugo, uongezaji wa kina cha lambo, mfereji wa umwagiliaji na mabomba ya kusambaza maji. Fedha za kukamilisha kazi hizi zitatokana na Bajeti ya Halmashauri ya Mbogwe kulingana na makubaliano ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshauri Mheshimiwa Mbunge kuhimiza Halmashauri yake ya Mbogwe kutenga fedha katika Bajeti yake ili kukamilisha ujenzi wa mradi utakaosaidia kutoa huduma kwa mifugo ya Kijiji cha Nsango na vijiji vingine vya jirani. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuzuia uvamizi wa hifadhi ya wanyamapori.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ni mpya na inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ujenzi wa Wilaya hiyo na kwa maana hiyo suala la Bajeti huwa lina ukomo.

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kutoa fungu maalum kwa ajili ya kusaidia kazi hiyo ya ujenzi wa mabwawa katika kijiji cha Nsango?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kitu muhimu ni kuweka mradi huu kwenye Bajeti yao ya Halmashauri halafu suala lingine linalofuata ni kule kusema sasa sisi tuko katika hali hii tunaomba msaada kutoka kwenye Serikali kuu.

Ni dhahiri kabisa akiwasiliana na TAMISEMI Makao Makuu pamoja na Wizara yangu ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi tutaangalia ni jinsi gani tunaweza tukamsaidia.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Na. 64

Hoteli za Bei Nafuu Katika Hifadhi za Taifa

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED (K.n.y. MHE. MAGDALENA H. SAKAYA) aliuliza:-

Kukosekana kwa Hoteli za bei nafuu kwenye Hifadhi zetu kunasababisha Watanzania wengi kutotembelea maeneo hayo na hivyo kudhoofisha juhudi za kukuza utalii wa ndani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa kunakuwepo na hoteli za bei nafuu kwenye hifadhi ili Watanzania wengi waweze kutembelea hifadhi hizo?

(b) Je, nini hatma ya *Hotel* ya Mikumi *Lodge* ambayo ilikuwa na mgogoro na Serikali na ikashinda kesi?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Malazi katika Hifadhi za Taifa yamegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni malazi ya Kudumu yaani Loji (*Lodges*) na hii inakuwa ni *Hotels and Lodges* na Kambi za Muda za Utalii *(Camp Sites)*. Katika malazi ya kudumu, Hifadhi za Taifa zinamiliki sehemu za huduma za malazi zinazojulikana kama Mabanda, *Hostel* na *Rest Houses*.

Mheshimiwa Naibu Spika, (a) Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* hutoza kiwango kidogo Watanzania wanaopenda kulala katika maeneo yanayomilikiwa na Shirika. Kwa sasa gharama za kulala katika mabanda yaliyopo Hifadhi hizi ni kati ya shilingi 20,000/= hadi 50,000/= kulingana na aina ya Mabanda ambayo mtu angependa kulala. *(Makofi)*

Aidha, kulala katika Kambi za Muda za Kitalii, kwa watu wazima ni kati ya shilingi 5,000/= hadi 15,000/= kulingana na aina ya Kambi ambayo mteja atachagua. Kwa watoto wenye umri kati ya miaka 5 hadi 16 hutozwa kati ya shilingi 2,500/= na 7,500/= na watoto chini ya miaka 5 hawatozwi kabisa gharama yoyote. Shirika lina mpango wa kuongeza mabanda zaidi ili kukidhi mahitaji yanayoendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, (b) Mgogoro kati ya iliyokuwa Loji ya Mikumi na Serikali ulishakwisha. Hotel hiyo ilishakabidhiwa kwa Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA).* Aidha, Shirika lipo kwenye hatua mbalimbali za kukamilisha utaratibu wa kumpata mwekezaji mpya ili eneo hilo liweze kupata mwekezaji na hoteli hiyo ijengwe tena.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rajabu swali la nyongeza.

MHE. RAJAB M. MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru. Imekuwa kawaida ya Mawaziri wakati wanakwepa kwepa baadhi ya masuala kusema kwamba tupo mbioni mchakato unaendelea, mipango na mikakati inaandaliwa. Nataka kujua huo mpango ukoje na utakamilika lini? Kwa sababu ni ninyi ndio ambao mnahimiza utalii wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Waziri, suala la pili kwa kuwa Wawekezaji hawa wengi wana kawaida ya kukwepa kulipa kodi za Halmashauri kwa maana ya *Service levy* katika Halmashauri husika ambazo wamewezesha hasa katika Ukanda wa Pwani ukiangalia kule Lindi, Pangani, Kilombero katika milima ile Udzungwa hawalipi zile *service levy* zinazotakiwa.

Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa hawa Wawekezaji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rajabu, kama ifuatavyo:-

Moja tulipozungumzia katika jibu la msingi kwamba hoteli hii *lodge* hii ya Mikumi hatua za kumpatia Mwekezaji zinaendelea hatukua tunababaisha, hadi kufikia hapa nilipo Shirika la Hifadhi za Taifa *TANAPA* limetangaza tenda ya wazi kwa Wawekezaji wote wa ndani na nje ya nchi. Tayari wamefanya kinachojulikana kama *short list* na Shirika linapenda kushiriki kwa njia ya *(Public Private Patnership (PPP)* ambayo italiwezesha Shirika kuwa sehemu ya umiliki wa hiyo hoteli mpya ambayo itajengwa badala ya kumilikiwa na Mwekezaji mmoja kwa asilimia mia kwa mia. Nikuhakikishie tu Mheshimiwa Rajab haya tunayozungumza hapa ni maneno ya kweli na tunaamini wakati wowote Shirika la Hifadhi za Taifa litampata Mwekezaji ambaye ataanza shughuli kwa kushirikiana na Hifadhi ili hoteli hii ya Mikumi irudi katika utukufu wake wa mwanzo.

Swali lako la pili, Mheshimiwa Rajab nipende kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba mwaka huu Serikali kupitia Bunge lako tulipitisha TOZO *(Tourism Developent Levy)* ambayo inatozwa dola moja na centi hamsini kwa kitanda.

Kwa maneno mengine kwa kila mgeni ambaye analala katika kitanda atalipa dola moja na senti hamsini ili ziweze kusaidia harakati za Serikali za kuendeleza Utalii. Ikiwa ni pamoja na kuutangaza Utalii ndani na nje na tunaamini kwamba kwa mpango juu mpya na labda nimhakikishie tu Mheshimiwa Rajab kwamba tatizo la ukusanyaji tunalitatua kwa kuikabidhi *TRA* haki na dhamana ya kukusanya mapato yote yatakayotokana na *Tourism Developent Levy* na tunaamini kwamba itakuwa *more efficient* na tutaongeza jitihada za kuhakikisha kwamba tunatangaza Utalii wa nchi yetu duniani kote.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Kivuli Mheshimiwa Mch. Peter S. Msigwa.

MHE. MCH. PETER SIMON MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa kumekuwa na matatizo mengi ya malazi hasa *lodge,* na kumekuwa na tatizo kubwa wageni wakija wakati Fulani wanakosa.

Lakini kama vile haitoshi hizi *lodge* waswahili wamekuwa wakibaguliwa sana hasa wenyeji wakati zinakuwa vile vile zina nafasi na imeonekana kabisa kuna ubaguzi wa wazi wa *citizen native* Wizara inasemaje kuhusu kukomesha tatizo hili ambalo waswahili wanabaguliwa kwenye hizi *lodge* za hadhi ya juu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii kuhusu ubaguzi katika *lodge.*

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Msigwa kama ifuatavyo:-

Kwanza nimshukuru tu kulileta hili suala hapa. Kwa sababu kwa wakati tofauti tofauti tumewahi kupokea malalamiko ya wananchi ambao wanaamini au wanasema waliwahi kubaguliwa kwa njia moja au nyingine katika baadhi ya *hotels* au *lodges* ambazo zinatoa huduma za kitalii.

Agizo la Serikali ambalo lilitolewa na Mheshimiwa Kagasheki na mimi nalirudia,Ni marufuku kwa hoteli yoyote inayofanya kazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo imepewa leseni na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumbagua mtu yeyote kwa sababu yoyote kwa wakati wowote.

Aidha tumewaomba wananchi wote nchini kama kuna mtu yoyote atashuhudia ubaguzi wa aina yoyote aripoti tutachukua hatua kali sana ikiwa ni pamoja na kuwafungia

wahusika. Kwa sababu ubaguzi hauna nafasi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresso swali la mwisho.

MHE. CECILIA DANIEL PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa hakuna maendelezo yanayo ruhusiwa katika *Crater Rimes* ya Ngogoro, maendelezo hayo yakiwa ni hoteli au *Camp Sites*. Kutoka mita mia tano kutoka *rimes* hakuna maendelezo pia yanayoruhusiwa.

Je, ni kwa nini Serikali inaruhusu ujenzi wa *Kibo Palace* kujengwa katika maeneo yasiyoruhusiwa?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso, kama ifuatavyo:-

Moja nirudie tena kulihakikishia Bunge kwamba utaratibu uliowekwa katika kuwekeza katika Hifadhi zetu zote za Taifa ikiwa ni pamoja na *Ngorongoro Conservation* una zuio, zuio ni mahali ambapo hairuhusiwi kuwekeza kutokana na sababu za kiuhifadhi na mpango unaojulikana kama *GMP* au kwa lugha *nyingine General Management Plan* unawekwa kwa kila Hifadhi ama kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na unakuwa *reviewed* kila baada ya miaka kadhaa na mara nyingi ni miaka mitano.

Ili uweze kuonyesha Geologia ya hilo eneo, tabia za wanyama ambazo zinabadilika mara kwa mara, mifumo mbali mbali ya kigeolojia ambayo inaendelea na hiyo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

inawawezesha Wataalam kuweza kupanga ni mahali gani inawezekana sasa kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile niseme uwekezaji wa aina yoyote bado ni lazima upate kibali cha Ofisi ya Makamu wa Rais inayoshughulika na masuala ya *environment* na lazima ipatikane cheti cha *Enviromenal Impact Assessment* ambacho kwa vyo vyote vile haiwezekani kama upande mmoja wa Hifadhi walikosea, upande mwingine wa *environment* watarekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kumhakikishia Mheshimiwa Cecilia Paresso kwamba hakuna uwekezaji wowote ambao unaruhusiwa na ambao tutaukubali kama haujazingatia *The General Management Plan* ya Hifadhi husika na tunaagiza kwamba kwa vyo vyote vile katika kugawa haya maeneo lazima mpango huu uzingatiwe.

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, swali linaulizwa na Mheshimiwa Ismail Aden Rage, ambaye simwoni. Kwa niaba yake Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba.

Na. 65

Usajili wa Magazeti Nchini.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA (K.n.y. MHE. ISMAIL A. RAGE aliuliza:-

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumika kusajili magazeti nchini?

(b) Je, kuna magazeti mangapi yaliyosajiliwa hapa nchini?

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, kama lilivyowasiliswa na Mheshimiwa Komba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kusajili magazeti ni kwamba anayetaka kusajili gazeti huwasilisha barua ya maombi kwa Msajili wa Magazeti huku akiainisha jina pamoja na madhumuni ya gazeti husika. Kusudi la kuwasilisha majina ni kutoa fursa wa Msajili wa Magazeti kuchunguza katika orodha ya magazeti/majarida ili kufahamu kama jina hilo limesajiliwa au la.

Baada ya Msajili kujiridhisha kwamba jina la Gazeti tarajiwa halimo kwenye orodha, mhusika hupatiwa masharti na fomu za usajili. Mhusika hutakiwa kujaza na kukamilisha fomu za aina nne na kuziwasilisha zikiwa zimeambatanisha na vitu vifuatavyo:-

Vyeti na Wasifu *(CV)* wa Mhariri, Vyeti na Wasifu *(CV)* wa Waandishi angalau wanne waliohitimu katika Vyuo vya Uandishi wa Habari vinavyotambuliwa na Serikali. Vyeti vya Usajili wa kampuni, nakala ya Sera ya Gazeti, Mchoro wa Gazei *(Dummy)* tarajiwa pamoja na andiko la uendeshaji wa mradi wa gazeti.

Vile vile mwombaji baada ya kutimiza masharti tajwa hapo juu, hupaswa kulipa ada ya usajili ya Shilingi laki Tano tu (500,000) na kisha kupatiwa Hati ya usajili.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina jumla ya magazeti na majarida mia nane na tatu (803), ambayo yote yamesajiliwa kwa mujibu wa Sheria.

NAIBU SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa Capt. John D. Komba.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mema na mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Hesabu zipi ambazo zimefanya magazeti ya Mwanahalisi, Mtanzania na Mwananchi yafungiwe?

(b) Je, ni mara ngapi gazeti la Mwanahalisi limewahi kuonywa? Je, kuna hatua zozote zimechukuliwa kabla ya kufungiwa?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Dkt. Fennela Mkangara.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Capt. John Komba, kwa niaba ya Mheshimiwa Rage kama ifuatavyo.

Kwanza swali la kwanza la kuhusu sababu zilizopelekea kufungiwa magazeti ya Mwanahalisi, Mtanzania na Mwananchi kwa ujumla. Labda niseme tu kwamba magazeti haya yalifungiwa kutokana na mwenendo wake wa kuchapisha habari na makala za uchochezi, uhasama na uzushi na zenye mwelekeo wa kujaribu kutoa Taarifa mbalimbali ambazo zilikuwa zinaelekea uvunjifu wa amani. Katika matoleo yao mbalimbali hasa gazeti la Mwanahalisi, limeandika vitu vingi sana.

Kwa mfano vichwa kama vile kuanzia mwaka 2008 mpaka 2010 liliweza kuonywa kama mara kumi. Liliendelea kuandika limeweza kufungiwa kwa miezi mitatu hili ni gazeti la Mwanahalisi. Lakini baada ya kufunguliwa bado ilkaendelea kuandika vitu mbalimbali vya kukiuka maadili.

Kwa mfano vichwa vya Habari kama Njama za kumng'oa Dkt. Kikwete zafichuka. Lakini pia tatizo la ma-*First Lady* wetu ni hizi hapa. Lakini pia waliweza kuandika habari kuhusu Mheshimiwa Sophia Simba hawezi kuwaza zaidi ya ngono. Njama za kuiba kura hizi hapa.

[WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO]

Kwa hiyo, ni gazeti ambalo lilikuwa linatoa maudhui ambayo kwa kiasi kikubwa yanapelekea kugonganisha watu. Lakini pia kuweza kuvunja amani kwa namna moja au nyingine. Yameendelea kuchapisha habari Uraia wa Kabila jambo ambalo lingeweza kutuletea matatizo baina ya nchi yetu pamoja na nchi ya *Congo DRC.*

Limeendelea pia kuzungumza pia masuala mbalimbali kama vile Kikwete ni dhaifu, Njama za mauaji mbali mbali na wamekuwa wamepelekea moja kwa moja hili ni gazeti la Mwanahalisi kuonyesha kama vile mipangilio yote ya wale wanaumizwa mbali mbali ni mipangilio ambayo yanafanyika kwa makusudi kabisa kutokana na Serikali.

Sasa swali lingine la pili na Mtanzania na lenyewe limekuwa katika kuchukua maudhui ya namna hiyo hiyo. Mtanzania pamoja na Mwanahalisi yamekuwa yanajikita kutoa Taarifa zenye mwelekeo wa kuvunja amani uchochezi na uzushi kwa kiasi kikubwa.

Kwa mfano, gazeti la Mtanzania tuliweza kulifungia baada ya kuandika maudhui yenye kuzungumzia tena katika ukurasa wa juu kabisa uraisi wa damu na kuzungumzia masuala kwamba mapinduzi hayaepukiki. Ukisoma mle ndani unaona kabisa ni maudhui ambayo yanalenga kugombanisha aidha Serikali na wananchi wake. Lakini pia kutaka kuleta uvunjifu wa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia waliweza kuandika kitu kinachosema Serikali inanuka damu na kuweka picha mbalimbali katika magazeti ambayo unaona kabisa yamesukwa kwa kiasi kikubwa. Lakini picha ambazo kwa kiasi kikubwa sio nzuri kuweza kutokea kwa wananchi au kuendelea kuhimiza au kuitengenezea kama vile ndio habari muhimu kwa wananchi. Gazeti la Mwananchi limeandika habari ambazo ni mishahara ya Serikali lakini pia wameweza kuandika masuala ambayo tulikuwa katika kipindi kigumu cha kushughulikia waliweka gazeti ambalo linazungumzia masuala ya Waislamu wanasali katika ulinzi mkali. Lakini

katika gazeti wakaweka picha kubwa ya mbwa pamoja na Waislamu wakiwa katika shughuli zao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ile peke yake inakuwa inaleta picha ambayo sio nzuri, ambayo sisi kama Serikali tumeona ni muhimu tuweze kutoa adhabu stahiki ili Taarifa na shughuli za namna hiyo tuseme kabisa kama Serikali sio kitu ambacho sisi tungependa kiendelee. Yapo mambo muhimu kabisa yakuweza kuendelea kuyaandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika swali lingine amesema ni mambo gani ambayo magazeti yanatakiwa kuzingatia ili yasiweze kufungiwa? Ni mara nyingi tunahimiza magazeti mbalimbali pamoja na vyombo vya Habari yazingatie Taarifa, yazingatie Sheria na Kanuni zake.

Kwa mfano, kama kuna Taarifa ya mabadiliko ya gazeti wanapobadili Mhariri, ni lazima Msajili aambiwe, Mchapishaji anapo badilika kwa maana ya *publisher*, Mchapaji kwa maana ya *printer* anapobalika, Mmiliki wa magazeti au wamiliki wanapobadilika kwa kuuza kampuni au kuuzwa kwa gazeti hata Ofisi ya gazeti inapohama sehemu moja kwenda sehemu nyingine na kadhalika.

Hivyo ni vitu ambavyo vinatakiwa Msajili aambiwe kwa sababu zipo taratibu ambazo zimewekwa za kufuatilia hawa watu, kwa sababu kwa kiasi kikubwa ni watu ambao tumewapa dhamana kubwa ya kuweza kuwafikia wananchi moja kwa moja. Kwa hiyo, taratibu na Sheria zilizowekwa ni muhimu na ni lazima ziweze kufatiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine kubwa ni kutochapisha habari za uongo na uchochezi kuhusu wananchi, Serikali na Taasisi zake. Hivi ni vitu ambavyo tumehimiza kabisa ni lazima vizingatiwe.

Kwa hiyo, wanapokwenda kinyume cha hii ndio hapo unaona gazeti tunalifungia, lakini hata vyombo vingine vya habari kwa maana ya Redio na *Television,* tunazifungia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Na. 66

Kujenga Shule za Masomo ya Sayansi kwa Kila Mkoa

MHE. RUKIA KASSIM AHMED aliuliza:-

Karibu asilimia tisini (90%) ya wanafunzi wanaosoma masomo ya Sanaa *(Arts)* wamefanya hivyo kwa kukosa msingi mzuri wa Elimu ya Sayansi na Hisabati.

Je, Serikali iko tayari kujenga shule moja kwa kila mkoa ambayo itakuwa na vifaa kamili vya maabara na walimu wazuri kwa ajili ya wanafunzi wa Sayansi tu?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Elimu na Mafunzo ya ya Ufundi ya mwaka 1995 inatambua umuhimu wa kuweka msingi imara wa masomo ya Sayansi na Hisabati. Kwa mantiki hiyo, masomo haya yanafundishwa kuanzia shule za msingi.

Kimsingi ufundishaji na ujifunzaji wenye tija unategemea uwepo wa walimu mahiri pamoja na miundombinu na vifaa vinavyotosheleza mahitaji kama vile maabara, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na vitabu vya kiada na vitabu vya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Mpango wa Maendeleo ya Sekondari, Serikali inatekeleza mkakati wa kuzifanya shule 1,200 kuwa shule zilizokamilika kwa awamu tatu. Katika awamu ya kwanza Serikali inaboresha miundombinu mbalimbali ya shule 264 ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maabara ya masomo ya Sayansi. Aidha, Serikali

inakusudia kuajiri walimu wa kutosha wa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa kadiri ya mahitaji ya ikama katika shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo wazo la Mheshimiwa Mbunge la kujenga shule moja kwa kila mkoa yenye vifaa kamili vya maabara na walimu wa kutosha wa masomo ya Sayansi na Hisabati litakuwa limetekelezwa kupitia mkakati huu.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Pamoja na majibu mazuri yenye afya na ya kuridhisha bado nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa maendeleo ya nchi yanaletwa na Sayansi na Teknolojia.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuwapembua wanafunzi wa *Primary* ambao wanaonekana kuwa na uwezo na vipaji vya masomo ya Sayansi na Hisabati na kuwaweka pamoja ili iwe ni rahisi kwao watakapofika sekondari waweze kuendelea na masomo haya bila ya shida na Tanzania iweze kuwazalisha wanasayansi wengi?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la Mheshimiwa Mbunge ni zuri na nadhani anatuongezea kazi katika mchakato huu ambao tunaufanya sasa hivi kujaribu kutafuta njia mbalimbali za kuhamasisha masomo haya Sayansi.

Tumejaribu pamoja na njia za kutenga baadhi ya shule ziweke mkazo wa Sayansi na hisabati kama vile tulivyojenga sasa hivi shule ya Sekondari ya Wasichana Miono tumei-*dedicate* kwa ajili ya Sayansi peke yake na tunaikamilisha vizuri kwa ajili ya sayansi.

Lakini tunaangalia pia namna zingine ambazo tutawezesha kuanzia mapema kabisa ngazi ya msingi mpaka sekondari kuona namna gani ambavyo vijana hawa tutawawezesha waendelee kupenda masomo haya ya Sayansi pamoja na Hisabati. Tutaweka mkazo zaidi, tutafuata

mawazo ya Mheshimiwa Mbunge, kama vile ambavyo amependekeza. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. SABREENA SUNGURA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa ilikuwa ni azma ya Mheshimiwa Rais kwamba katika nchi nzima kila Mkoa *at least* iwe na shule ya mchepuo wa Sayansi na Kigoma tumekuwa mkoa ambao tumetoa mfano kwa kuandaa eneo katika maeneo ya Kasulu, kwa kujenga *Kigoma Grand High School* na wananchi wa Kigoma na maeneo mengine mbalimbali ambayo yanaitakia Mkoa wa Kigoma tumechanga kiasi zaidi milioni 300 mpaka sasa hivi.

Je, Serikali sasa iko tayari kutusaidia kwa sababu mradi wenyewe unahitaji zaidi ya bilioni 2?

Serikali iko tayari kwa namna moja ama nyingine kutu-*support* ili kuhakikisha kwamba azma hii ya Mheshimiwa Rais inafikiwa? Shukrani. *(Makofi)*

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze sana Wana Kigoma kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kuchangia katika maendeleo ya elimu. Ni elimu tu ndiyo ambayo itatutoa katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilichukue hili kama taarifa rasmi ili niweze kuona ni namna gani ambavyo tutaweza kuwasaidia Wana Kigoma waweze kutimiza lile ambalo Mheshimiwa Rais ameliahidi katika Mkoa wa Kigoma.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge maswali yetu yameisha na muda wa maswali kwa kweli hauko upande wetu. Sasa ni matangazo.

Tangazo la kwanza tunawaomba radhi sana Waheshimiwa Wabunge kwa aina ya pipi ambazo mmeletewa, baadhi yake *cover* zake siyo nzuri sana. Tutarekebisha, natumaini Makatibu wangu mmenipata.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wanafunzi 64 toka Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es Salaam, wakiongozwa na Mwalimu wao Ndugu Omari Shegila. Wanafunzi pale mlipo simameni. Ahsanteni sana na karibuni sana Dodoma. Karibuni sana hapa Bungeni.

Wako wageni wawili kutoka *Tanzania Fellowship of Churches Dar es Salaam,* karibuni sana hapa Bungeni.

Matangazo ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge na Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mgimwa anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya Uchumi, Viwanda na Biashara wakutane saa 7.00 mchana Msekwa B, saa saba mchana. Mheshimiwa John Lwanji, Makamu Mwenyekiti, wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane Ukumbi wa *Basement* saa saba na robo mchana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mama Anna Abdallah, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo saa 7.00 mchana wakutane katika Ukumbi Namba 227. Hiyo ni Kamati ya Ulinzi na Usalama Ukumbuni Namba 227 saa saba na robo mchana.

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, wakutane Ukumbi wa Pius Msekwa saa 7.15 (Saa saba na robo mchana), Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Gosbert Blandes, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, anawaomba Wajumbe wa Katiba, Sheria na Utawala saa 7.00 mchana kwenye Ukumbi Namba 231.

Mnadhimu wa Kambi ya *CUF* anawaomba Wabunge wa Kambi hiyo wakutane saa 7.00 mchana huko *Basement* kwa sababu kuna Kamati nyingine inakutano huko huko mtajua namna gani ya kugawana. Wabunge wa Chama

[NAIBU SPIKA]
cha *CUF* saa 7.00 mchana wakutane *Basement*. Katibu tuendelee na *Order Paper.*

HOJA ZA KAMATI

Taarifa za Kamati za Bunge za Hesabu za Serikali za Mitaa, Kamati ya Bunge ya Bajeti na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Pamoja na Mapendekezo na Maoni Yaliyomo Katika Taarifa hizo

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Majadiliano yanaendelea Waheshimiwa Wabunge na utaratibu wetu ni kwamba katika orodha niliyo nayo kama itakuwa sikuoni humu ndani sitakutaja ili wapiga kura wako wasione kama unatoka toka sana. Kwa hiyo nikiwa katika orodha yangu na ninakuona nitakupa nafasi moja kwa moja. Kwa hiyo, msitoke toke sana.

Tutaanza na mchangiaji wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Felix Mkosamali na Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, atakuwa wa tatu. Mheshimiwa Betty Machangu.

MHE. BETTY ELIEZER MACHANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa *CAG* kwa kazi nzuri anayofanya ya kugundua dosari katika Serikali na Idara zake katika kusimamia fedha na rasimali za umma. Napenda pia nimpe hongera kwa Ofisi yake kuchaguliwa miongoni mwa Taasisi za Wakaguzi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa taarifa za *CAG* zinaonyesha kwamba hati za kuridhisha za ukaguzi zimeongezeka kutoka asilimia 85 kwa mwaka 2010/2011 mpaka asilimia 94.7 mwaka 2011/2012 bado usimamizi wa fedha na rasilimali nyingine za umma hauridhishi. Ziko dosari nyingi katika tofauti ambazo *CAG* ameelekeza zitekelezwe

na Serikali kwa miaka ya nyuma na mpaka sasa bado hazijatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitaje maeneo machache ambayo kwa muda mrefu *CAG* ametoa hoja yatekelezwe lakini Serikali bado haijatekeleza. Mojawapo ni uundwaji usiyo sahihi wa vitengo vya kusimamia manunuzi yaani *PMU.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linaloonekana hapa ni viwango vya elimu walivyonao Maafisa wa Taasisi nyingi za manunuzi. Maafisa hawa wanatakiwa angalau wawe na Shahada moja. Kwa nini Shahada. Kwa sababu ile kazi wanayofanya inatakiwa iwe kazi ya umakini mkubwa. Kwa mfano, wanatakiwa waunde Kamati ambazo zitakuwa zinafanya ukaguzi wa ndani na vifanye vikao mara nne kwa mwaka. Kwa kupitia Taarifa mbalimbali za Taasisi zile ambazo wanasimamia.

Lakini pia wana kazi ya kutoa msukumo kwa Taasisi kwa ajili ya kujibu hoja za CAG na kupitia pia mpango kazi wa Taasisi hizo. Wapitie Bajeti za Taasisi hizo na kutoa *recommendation* kwa Watawala lakini washauri pia watawala inapoonekana kwamba kuna athari inaweza kutokea yaani wafanye *risk management.*

Lakini Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa hawa hawawezi kufanya hii kazi kikamilifu. Mwisho wa siku Serikali inaendelea kupata hasara. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeshauri Serikali ipitie upya *CV* za Maafisa hawa kwa sababu wako vijana wengi waliomaliza Vyuo Vikuu nchini na wanaweza kuifanya hii kazi kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hizi ni uundaji usiyo sahihi wa mipango ya mwaka ya manunuzi. Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* anashauri kwamba kama mipango ikiwa mizuri ya manunuzi inaepusha sana manunuzi ya dharura ambayo yakitokea yanaweza kuwa na gharama kubwa. Lakini pia kwa kujumuisha manunuzi haya unaponunua kwa wingi kuna unafuu wa bei. Lakini pia

inasaidia Taasisi kuingia katika mikataba endelevu na hasa pale ambapo kuna manunuzi yanayotakiwa mara kwa mara. Mwisho ni kwamba kwa kupanga kuweka mpango mzuri wa manunuzi ni rahisi kuweka vikao vizuri vya Bodi za Zabuni na hiyo inapunguza gharama.

Mheshemiwa Naibu Spika, *CAG* pia alishatoa kwa siku nyingi udhaifu ulioko katika usimamizi wa mikataba nchini. Anasema kwamba Serikali inaandaa mikataba ambayo wakati anafanya ukaguzi unakuta mikataba inakosa nyaraka muhimu. Mikataba mingine inaonekana ina nyaraka ambazo siyo za mikataba. Dhamana zilizowekwa hazitumiki inapotokea kushindwa kutekeleza mkataba na pale ambapo mali zinapokelewa ambazo hazina ubora muda wa kupewa huduma za malipo hautumiki.

Pale ambapo kuna uchelewesha wa kutekeleza mikataba hakuna fidia. Hakuna vikao vinavyofanyika kwenye miradi, katika miradi yote inayopitiwa. Hakuna udhibiti wa kuhakikisha wa utekelezaji wa mikataba hii na hata ubora wa mikataba hii. Lakini pia hakuna hata Kamati ya Mapokezi sasa inapokuwa ni manunuzi yamefanyika, mapokezi ya kuhakikisha ubora na uhalali na idadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunafanya mambo ambayo yataliumiza Taifa hili. Ni mikataba hii hii ambayo imekuwa inalalamikiwa kwa muda mrefu. Mikataba hii imetuingiza katika hali mbaya. Tukalalamika kwa muda mrefu. Kwa hiyo, kwa kipindi kuna umhimu sana Serikali izingatie hizi hoja za *CAG* iweze kutekeleza. Ni vizuri mikataba hiyo ipitiwe na kwa mfano ameshauri sana kuhusu Serikali kupitia mikataba kama ya Songas, *IPTL, TICS na ATMAS* kwa sababu katika mikataba hiyo kuna mapungufu mengi, amesema *CAG.* Laiti Serikali ingekubali kupitia hii mikataba, maana yake ni kwamba yale mapungufu yaliyopo yangerekebishwa na ingekuwa mikataba iliyo na tija kwa taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo lingine pia ambalo *CAG* anasema hata mikataba hii basi inapokamilika, Kanuni ya 21 (1) na ya 67(4) ya matangazo ya Serikali ya 97

na 98 ya mwaka 2005 inataka sasa serikali ikishaweka mikataba iweke kwenye jarida na tovuti. Lakini anasema nalo hili ni tatizo kwa Serikali huaga haifanyi hivyo. Hata kumbukumbu kutunza anasema ni kutunza kumbukumbu kwa Serikali imekuwa ni vigumu sana. Akitaka orodha ya zabuni hazionekani. Wakitaka nukuu za bei za mikataba nazo hazionekani na inaelekea hata Maafisa wengine wanaficha karatasi au nyaraka nyingine kwa sababu wanajua kabisa kwamba kuna mapungufu yametokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo lingine ambalo *CAG* amekuwa analishauri na mojawapo ni kukokotoa vibaya mafao ya wastaafu. Anasema isingekuwa ni ukaguzi wako wastaafu 184 ambao wangelipwa kiasi kisichostahili cha shilingi milioni 328,261. Lakini wako wengine 151 ambao pia wangepunjwa kiasi cha shilingi milioni 258,915.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yanafanyika kwa sababu ya uzembe wa Watendaji, kwa sababu ya Watendaji kutokuwa makini ya kutafsiri tofauti Sheria za mafao. Hebu fikiria, hebu *imagine* jinsi ambavyo mafao ni machache jinsi watu waliostaafu wanapata hela kidogo. Lakini huyu mfanyakazi au mtendaji amekaa Ofisini anakokotoa kiasi ambacho anampunja huyu mtu ambaye anatakiwa kulipwa mafao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ilifuatilie hili. Lipo tatizo la usimamizi wa madeni yanayotokana na ubia wa Serikali na Sekta binafsi. *CAG* amekuwa anashauri mara nyingi kwamba Serikali isitoe mikopo kwa watu binafsi na hasa kwa kampuni zile ambazo hazina uwezo kifedha. Zile ambazo zinataka kuwekeza kwa sababu anashauri kwamba mwisho wa siku mzigo wote unaangukia Serikali na katika Sheria ya mwaka 1974 ya mikopo, udhamini na misaada ambayo ilirekebishwa mwaka 2004, Sheria hii Mheshimiwa Naibu Spika, inabidi irekebishwe kwa ajili ya Serikali iweze kuanzisha Kitengo cha *Mortgage Financing.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sisi Kamati ya Mambo ya Nje tumekuwa tunapigia kelele hii Sheria kwa sababu yapo

[MHE. BETTY ELIEZER MACHANGU]
majengo mengi yaliyoko Balozini na viwanja ambavyo vitahitaji kujengwa. Lakini tunailaumu Wizara ya Mambo ya Nje ambapo haitaweza mpaka hiki Kutengo kianzishwe na kitaanzishwa tu kama hii Sheria itarekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nikumbushe Serikali kuhusu hoja ya *CAG* ya kulipa deni la fedha ya hifadhi iliyojenga *UDOM,* hosteli za Mabibo na nyumba za Polisi na yenyewe Serikali imenyamazia kimya. Lakini pia nikumbushie pia kwamba kuna misamaha ya kodi ambayo imetolewa katika makubaliano ya *Production Sharing and Agreement.* Hii ni makubaliano ya *gas,* mafuta na gesi ambayo *TPDC* inafanya na makampuni ya nje na ibara ya 14 ya makubaliano hayo inasema makampuni haya yatalipa kodi na katika kulipa pia inapata misamaha ya mashine, vifaa, malighafi na magari. Lakini *CAG* alishindwa kupata taarifa hiyo ya misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali isimamie hili jambo la misamaha ya kodi na ningeshauri kama inawezekana Serikali itunge Sera au mwongozo kwa ajili ya usimamizi wa misamaha ya kodi. Lakini pia *CAG* anaitaka Serikali kurekebisha, katika Sheria ya Mapato ya mwaka 2004 (10) Kidogo cha tatu inasema mikataba yote iliyoingiwa na Serikali baada ya tarehe 1 Julai, 2004 isipewe misamaha. Lakini ajabu mwaka 2008 Serikali iliendelea kutoa mikataba ambayo ina misamaha ya kodi kwa kampuni ya *MCC.*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, unaona ni matatizo makubwa Serikali inabidi izingatie. Mambo yaliyojitokeza katika mwaka 2011/2012 ni pamoja na Serikali kushindwa kuweka masurufu ya *1.5 billion.*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajiuliza kwa sababu masurufu yanalipwa kwa Maafisa kwa majina yao. Sasa unajiuliza ni kwa namna gani Serikali imeshindwa kuweka kumbukumbu ya masurufu hayo. Lakini ziko bilioni 19 ambazo hazijaweza kukusanywa kutoka Mgodi wa Kahama na Shinyanga kwa sababu Sheria tuliyotunga mwaka 2010 Kifungu cha 87 kidogo cha kwanza

Kwa majina yao sasa unajiuliza ni kwa namna gani Serikali imeshindwa kuweka kumbukumbu ya masurufu hayo. Lakini ziko bilioni 19 ambazo hazijaweza kukusanywa kutoka Mgodi wa Kahama na Shinyanga kwa sababu Sheria tuliyotunga mwaka 2010 kifungu kidogo cha (87) na kidogo cha (1) na (c) kinasema mrahaba utakuwa 4% lakini kwa hapa Serikali imepokea 3% naomba Serikali ituambie kwanini ilipokea 3% wakati tulitunga Sheria zipokelewe 4%. Kwahiyo, Shilingi bilioni 19 bado hazijakusanywa.

Mhesimiwa Naibu Spika, iko amana ambayo iko kwenye *Deposit Account* ya Mhasibu Mkuu ya *1.5 billion, fedha* ambazo zilitakiwa miaka mitano iliyopita ziende kwenye Sekondari za Lindi, Mara, Iringa, Mwanza, Kagera, Rukwa,Tabora, Mbeya na Shinyaga, lakini *CAG* amezikuta ziko kwenye *account,* zaidi ya miaka mitano zimekaa kule, Shule hazina madawati, hazina maabara, lakini fedha hizi zimekaa mahali pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itakapojibu iseme ni kwanini fedha hizi hazipelekwi kunakohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko pia deni la *PSPF* ambalo Serikali inatakiwa ilipe na iliahidi kwamba ingelipa Shilingi bilioni 71 kwa kila mwaka kwa kipindi cha 2011/2012 kwa miaka kumi, lakini mpaka sasa Serikali bado haijafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo malipo yasiyokuwa na nyaraka za matibabu, hakuna majina ya wagonjwa, hakuna majina ya Hospitali, hakuna risiti, ambayo ni Sh. 448,144,000/= ambazo zimetumika. Naomba pia Serikali ituambie Waheshimiwa Wabunge, hizi fedha nyingi zimekwenda wapi? Mbona hakuna majina ya wagonjwa na majina ya Hospitali?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ni gari iliyonunuliwa TAMISEMI kwa Sh. 979,000,000/= lakini Mkaguzi alipoangalia akakuta kwamba kulikuwa na mpango wa dharura wa tarehe 26/3/2013 zilitolewa Shilingi bilioni 1,036, lakini risiti iliyokuwa ilionesha hii Gari, *Four Wheel Drive, Land*

[MHE. BETTY E. MACHANGU]

Cruiser ilinunuliwa kwa Shilingi milioni 979. Mimi nikasema, mbona ni ghali sana?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Betty Machangu, ni kengele ya pili.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilipigwa na butwaa uliposema gari ya Shilingi milioni 900, basi ikawa taabu kidogo. Mheshimiwa Rajab.

MWOGOZO WA SPIKA

MHE. RAJABU M. MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kutokana na kifungu namba 68.7 cha kanuni zetu za Bunge. Ni juzi tu hapa Mheshimiwa Kangl LugoLa, alizungumzia suala la uwepo wa Mawaziri katika Bunge, na Mheshimiwa Spika, alilisisitiza hili. Ni jambo la kushangaza kwamba, Wizara husika kama Wizara ya TAMISEMI sio Waziri, wala Manaibu wake, pamoja na Waziri Mkuu hawapo hapa. Kinachozungumzwa ni suala zima vile vile linalohusu Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hii, ni dharau kwa Bunge hili, ni dharau vile vile kwa Kiti chako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate mwongozo wako. Lakini vilevile naomba nitoe hoja kwamba kwamba mjadala huu uahirishwe mpaka pale Serikali itakapokuwa tayari kusikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida taarifa za Mawaziri wa Serikali wanapokuwa hawapo Bungeni, huwa zinatolewa kwa Mheshimiwa Spika, hazitolewi humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko Dar es Salaam. Leo anampokea Kiongozi Mkuu wa Uholanzi, Malkia, na kazi hiyo amekasimiwa na Mheshimiwa Rais kwasababu Mheshimiwa Rais amekwenda *South Africa*. Kwahiyo, hapa ndani tunaye Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali, yupo. Maana yake Waziri Mkuu sio Pinda, habebi wadhifa mgongoni, yeye siyo Kobe. Waziri Mkuu yupo hapa. Mheshimiwa Hawa Ghasia anafanya kazi katika Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ndio mratibu Waziri Mkuu wa shughuli za Serikali tupo na wataalamu wake wako pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za kila Waziri asiyekuwepo hapa ndani Ofisi yako inajua. Labda niseme kwamba ziko safari na ziko kazi zilipangwa, bila kujua kwamba Bunge hili litasogezwa muda. Kwa hiyo, ratiba hii imesababisha baadhi ya mipango ambayo Serikali ilikuwa imejiwekea iendelee. Hivi ninavyozungumza, Kamati teule ya Maliasili iliyoko Kunduchi ina Mawaziri kule; Bunge hili limewatuma baadhi ya Mawaziri kwenda Uganda; kwa hiyo, Mawaziri hawa ni wachache lakini wako kwenye shughuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kukuhakikishia kwamba yote yanayosemwa na Waheshimiwa Wabunge, yatapata majibu ya Serikali.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. SAsa namwita Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Gekul.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru ili nami niweze kuchangia kwenye hoja zilizowasilishwa wiki iliyopita; japo Mawaziri hawapo na maneno maneno haya tumekuwa tunayasikia kila siku wamekuwemo wawili watatu, wangapi ni mambo ya

kawaida tu. Sisi tunahutubia tu kwasababu tunajua ni *business as usual,* hakuna kitakachofanyika. Kwasababu hata mwaka 2012 tumeyazungumza haya, hawaji! Hii inaonesha kabisa kwamba hii Serikali imechoka na ni dhaifu mno. Sasa ngoja nichangie.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina ripoti ya jumla ya Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Machi, 2013. Sasa naomba ninukuu ukurasa wa 27, inasema hivi: "katika ukaguzi, ilibainishwa kuwa katika Halmashauri zote zilizotembelewa kulikuwa hakuna mipango ta ufuatiliaji wa usimamizi wa miradi na maelezo yanaendelea mengi sana. Yaani anamaanisha kwamba tukishapitisha fedha hapa Bungeni, fedha zikienda huko kwenye Halmashauri na hawa Mawaziri wanaojifanya sijui wako wapi, hakuna mtu anayefuatilia. Sasa mimi nikawa najiuliza, hivi nyie CCM mnatumia mbinu gani kushinda uchaguzi miaka 50 yote ya Uhuru? Kama tunawapitishia fedha hapa, halafu hizo fedha hazifuatiliwi, miradi haifuatiliwi, mbinu mnazotumia kudanganya wananchi, ni mbinu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunakushukuru, Juni, 2013 ulituitishia semina hapa nyuma katika Ukumbi wa Pius Msekwa ya *APNAC.* Kwenye semina hiyo tuliyopewa ilikuwa inahushu mambo ya rushwa, mie nina *paper* yake. Ikasema kwamba, "inakadiriwa kuwa asilimia 20 ya bajeti ya Serikali huliwa na rushwa kila mwaka." Ndiyo tulipewa taarifa hiyo hapo kwenye semina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, semina hii kama ulivyotuelekeza, ni kwa ajili ya kujifunza kwamba Serikali na Wabunge tujifunze ili haya mambo yasitokee tena. Sasa tumepewa semina tumeambiwa kila mwaka tukipitisha fedha hapa Bungeni, asilimia 20 zinaishia mifukoni mwa watu. Kwa maana hiyo ni kwamba, Serikali ya namna hii, hata tuongeze bajeti kiasi gani, hata bajeti ifike Shilingi trilioni 40, asilimia 20 ya fedha hizo zitaliwa, ndiyo watu hawa!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkosamali, ongea na mimi.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Sasa kwenye semina hiyo pia tukaambiwa kwamba taarifa za *CAG* na mapendekezo ya Kamati za Bunge kutofanyiwa kazi ipasavyo na Serikali, sasa haya tuliambiwa kabla ya taarifa za leo, ilikuwa ni taarifa ya nyuma. Maana yake *CAG* akiwaambia, akiandika, hawafanyi chochote. Sasa kama fedha zinaliwa na nyie hamchukui hatua na nyie si mnashiriki kwenye kula hizo pesa?

Haiwezekani Waziri wa TAMISEMI aambiwe kila mwaka, fedha zinaliwa kwenye Halmashauri, halafu hachui hatua yoyote, maana yake ni kwamba na yeye anahusika kwenye wizi wa hizo fedha. Ndiyo maana hachukui hatua! Anapewa bahasha! Angekuwa hapewi, angechukua hatua! Ndiyo maana leo amekimbia, hataki kuja kusikiliza. Sasa hiyo Semina ikawa imepita. Tukapewa Semina nyingine. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Semina hii nayo ilikuwa tarehe 5/ 4/2013, tukaambiwa kuna kitu kimeanzishwa kinaitwa *Big Results Now,* tukapewa hii *paper* tarehe 5/4 hapa hapa Dodoma. Tukaambiwa kuna nguzo tano za *Big Results Now.* Moja, tukaambiwa ni nidhamu ya hali ya juu ya utekelezaji uliojengwa juu ya uwepo wa program za kinaganaga, na mfumo wa ufuatiliaji na utathmini. Kwa hiyo, tukaambiwa ili *Big Results Now* tuliyopitisha ya Shilingi bilioni 29 ifanye kazi lazima kuwe na mambo ya kinaganaga ya ufuatiliaji na utathmini. *CAG* amewaambia mnapeleka pesa hamfuatilii na nyingine zinaliwa. Sasa hiyo *Big Results Now* mtaweza nyie! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza hotuba za Kamati zote, nimeshangaa sana. Bunge lako lisipoanza kuchukua hatua ya kuwafuatilia watu hawa, tutakuwa tunapoteza muda hapa Bungeni. Inatakiwa kabla ya Bunge hili kwisha, Mawaziri kadhaa hapa wasiwepo. Huwezi kuwa na Waziri ambaye kila mwaka analalamikiwa. Juzi Mheshimiwa Kangi Lugola, amezungumza, naomba nimpongeze sana huyu Mbunge wa Chama cha Mapinduzi ambaye anapiga hoja bila kuogopa. Nampongeza sana. *(Makofi)*

[MHE. FELIX F. MKOSAMALI]

Mheshimiwa Naibu Spika, Gazeti la Mwananchi hili, liliripoti kwamba TAMISEMI kutafuna fedha za Wafadhili ni kashfa. Hili ni Gazeti liliripoti kwamba TAMISEMI inakula fedha za wananchi na hii ni kashfa kwa Taifa; fedha za Wafadhili. Sasa kwenye Gazeti hili, aya ya mwisho Wafadhili wanasema, "sisi hatuna zaidi la kusema isipokuwa kumdhalilisha Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kuhusu athari za kuteua Mawaziri dhaifu kuongoza Wizara kubwa na nyeti kama TAMISEMI. Kashfa za wizi na ubadhirifu zimeielemea TAMISEMI, na hayo madudu na matatizo yaliyojificha ndani yake, hata hivyo, tunadhani kashfa hiyo angalau itasukumwa kuchukua hatua stahiki haraka iwezekanavyo. Ndiyo wanavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zimeibiwa, Wafadhili wanamtaka Mheshimiwa Rais Kikwete awafukuze hawa watu, lakini hakuna kitu kinachofanyika. Gazeti la Mwananchi la tarehe 27 Novemba, 2013. Sasa katika Katiba ya nchi Ibara ya 52, ndiyo inazungumza haya ambayo yamo kwenye kitabu cha *CAG* kwamba Waziri Mkuu, atakuwa na madaraka ya juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hata siku wa shughuli za Serikali. Sasa kama yote haya yamefanyika, huyu Waziri Mkuu anafanya kazi gani? Kama yeye kazi yake ndiyo kufuatilia shughuli za kila siku, wizi unafanyika TAMISEMI na yeye ndiyo yuko hapo juu, kwanini tusipige kula ya kumwondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe kama Kiongozi wetu, ndio unapaswa kutuongoza kupiga kura ya kuwaondoa hawa watu. Sisi tukileta hoja hiyo upande huu wa pili najua haitapitishwa. Wewe ambaye pia umechaguliwa na wananchi, ambapo pesa hizi zinazoliwa zingeenda kusaidia na kule Kongwa; unapaswa kutuongoza kuwafukuza hawa ambao Wafadhili wanasema ni mizigo. Maana usipofanya hivyo, wanakuathiri na wewe. Nawe utachomoka kule kwako! Chama cha Mapinduzi kikiendelea kuboronga hivi na wewe utachomoka! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipaswa kupumzika kistaraabu yeye mwenyewe. Waziri wa

[MHE. FELIX F. MKOSAMALI]
TAMISEMI pumzika! Sisi hatuwaambii ninyi kwasababu tunawachukia, hapana. Ni kwasababu mmeshindwa kufanya kazi ambazo tumewapatia. Hatuna chuki na mtu. Hata tukiwaambia tunajua hamtafanya, hamtaweza. Tumeshawapima, tumeona. Sasa tunawashauri nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tu nilimwuliza Mheshimiwa Waziri swali la kutatua mgogoro wa Kijiji, hawezi. Katoa majibu ya ubabaishaji hapa, ataweza kutatua matatizo ya nchi yote hii? Hawa watu ni wakupiga nje! Futa! Mabaraza ya Madiwani yanayoongozwa na CCM na yenyewe yanasababisha matatizo haya. Katika maeneo mengi Mabaraza ya Mabadiwani yameshindwa kusimamia Halmashauri zao. Hayo Mabaraza yanaongozwa na Chama chenu, Mabaraza haya na yenyewe yangekuwa hayali rushwa haya...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Mkosamali.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Hawa watu watoke. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa Pauline Gekul, atafuatiliwa na Mheshimiwa Mohamed Mgimwa.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika hotuba zilizoletwa mbele ya Bunge hili ambazo ni Kamati na ripoti za Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie pale ambapo Mheshimiwa Mkosamali ameishia, nianzie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliyoko madarakani, kila mwaka inawaambia Watanzania kule mnakotutuma kule tukarine asali, hakuna asali ya kutosha. Kasungura kadogo,

fedha hazitoshi, bajeti ni ndogo. Tunakwenda kwa wahisani, tunakopa, tulete maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukweli wa mambo haya, tuwaambie tu Watanzania, hatuna sababu ya kuongea na Mawaziri ambao wao walishalipuuza Bunge hili. Naamini kwamba Watanzania wanatusikia tukiwa kama Wabunge wao, tuwaambie jinsi gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi inawaibia Watanzania hela zao na kodi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wakati anahutubia Kamati Kuu hapa Dodoma, aliwaambia Chama cha Mapinduzi, Chama chetu kinanuka rushwa. Tusipojirekebisha, 2015 tutaondoka madarakani. Mimi nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kauli hiyo ya ushujaa, kwamba kuanzia Chama mpaka Serikali wananuka rushwa. Matokeo yake ni haya ambayo tunakwenda kuwaambia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vitabu 2,990 vya Makusanyo katika Halmashauri mbalimbali, ikiongoza Halmashauri ya Mbarali, vitabu 2,546 ukurasa wa 315 katika kitabu cha *CAG*, hivi vitabu havikuwasilishwa Halmashauri. Hivi vitabu havionekani! Vimekusanya kodi za wananchi. Je, vimekusanya hela kiasi gani hivi vitabu? Vitabu 2,990 vinavyokusanya kodi za wananchi, havionekani! *CAG* ameonesha! Ni hela kiasi gani zilizoibiwa Ndugu zangu Watanzania, halafu tunaambiwa kasungura kadogo, fedha hazitoshi.

Kosa letu Watanzania tunarudisha Chama kile kile miaka 52 ya uhuru, kituongoze kituambie chakula hakitoshi. Watanzania wangetaka kujua kwamba kodi zinatosha kuwaletea maendeleo, wangeliwaondoa hawa Chama cha Mapinduzi, angalau miaka mitano tu wakae pembeni, wajue chakula kipo au hakipo. Lakini tukiendelea kuwaweka madarakani watu hao hao, wakutuambia chakula hakitoshi, kweli Watanzania katika miaka 100 ijayo hatutaona maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

[MHE. PAULINE P. GEKUL]

Mheshimiwa Naibu Spika, maduhuli yaliyokusanywa na Mawakala hayakuwasilishwa Halmashauri, zaidi Shilingi bilioni 4.466. Shilingi bilioni nne, Mawakala mmewapa wakusanye hizo fedha, hawajapeleka kwenye Halmashauri, wametafuna. Kasungura ni kadogo kweli!

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania waangalie jinsi hela zao zinavyoibiwa. Lakini hao hao Watanzania katika shughuli za Maendeleo, wakijenga Zahanati, wakijenga shule, wanachangishwa na Watendaji wa Kata na wa Vijiji. Lakini hawa Watendaji na Mawakala hizi pesa wanashirikiana kula na watumishi wa Halmashauri. Fedha hizi hazionekani! Shilingi bilioni nne ni hela nyingi sana! Watanzania tujifunze kwamba tatizo siyo kodi zetu ni chache, tatizo ni Chama ambacho kimekufa ganzi miaka 52 ya uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara isiyolipwa, yaani mishahara hewa. Mheshimiwa Waziri amekuwa akituambia kwamba wameanzisha mfumo wa *Epicor 9.05.* Uliliambia Bunge hili Tukufu kwamba sasa mishahara hewa itakuwa ni wimbo wa zamani. Hii mishahara hewa haitakuwepo tena. Lakini hapa kwenye Kitabu hiki tunaambiwa, zaidi ya Shilingi bilioni 1.596, hii mishahara haikurejeshwa Hazina, imeliwa katika ngazi za Halmashauri. Mheshimiwa Waziri kwa nini usiwajibike kama mishahara hewa ndiyo iko hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara iliyolipwa kwa watu Waliofariki, watoro na hawako makazini; malipo hayo yamefanyika kwa watu ambao ni watoro, waliofariki zaidi ya Shilingi milioni 693, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imelipa watu waliofariki! Watanzania wanatusikia!

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 331, hizi pesa zingetosha kuwalipa Walimu posho ya Mazingira magumu ambayo asubuhi tulisemea hapa zaidi ya Sh. 500,000/= zingetosha kulipa zaidi ya Walimu 1,400 posho ya Mazingira Magumu ya Sh. 500,000/=. Hizi Shilingi milioni 693 zimeliwa, zimelipwa watu ambao wamefariki inasemekana wamezikwa, hawapo. Hii ni Serikali ya namna gani Watanzania? Ni aibu! *(Makofi)*

[MHE. PAULINE P. GEKUL]

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za ruzuku ya *MMAM (*Mpango wa Afya ya Msingi). Tunasema Zahanati hazitoshi Mheshimiwa Waziri, Zahanati hazionekani, lakini zilizojengwa hata hazijaunganishiwa umeme. Katika Mkoa wangu wa Manyara pale Babati, Zahanati ya Hala haina umeme mpaka leo. Zaidi ya Shilingi bilioni 2.589, hizi pesa hazikufanya kazi katika Halmashauri zetu. Ni kwa nini Serikali ya CCM mnaendelea kuwahadaa Watanzania mwendelee kuishi Madarakani, wakati haya mambo ya kusimamia pesa zao na kodi zao mmeshindwa? Lakini malipo yenye nyaraka pungufu, naomba tu leo niwasomee Watanzania mahesabu ya fedha zao. Zaidi ya Shilingi bilioni 3,367, hizi fedha zimelipwa na nyaraka hazionekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashirika binafsi au *NGOs,* zinafanya kazi nzuri.

NAIBU SPIKA: Kidogo tu Mheshimiwa Pauline. Bahati mbaya sana sikuwepo wiki iliyopita, Wakati tumeanza mjadala huu, nilikuwa napata taabu sana hapa, ndiyo maana nikamhitaji Katibu anisaidie kidogo kinachoendelea ni nini? Kwa sababu japo ninaongoza kikao, lakini naona kama nimeachwa kwenye mataa kidogo. *(Makofi)*

Hoja iliyopo mbele yetu, Mezani hapa za kujadiliwa ni hoja za Taarifa za Wenyeviti Watatu. Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa; Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti; na Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Baadhi yetu tumekuwa tukisimama tunajadili taarifa ya *CAG*. Twende taratibu. Taarifa ya *CAG*, ni kitu ambacho ni *very raw.* Sijui Kiswahili chake itaitwaje. Yaani ni taarifa ambayo bado haijachambuliwa. Unaweza ukasema hapa hela fulani zimeibiwa, kumbe baada ya ufuatiliaji wa Kamati na Uchambuzi wake hela hizo hazikuibiwa. Kwa hiyo, tukajikuta tunapotosha sana Taifa. Kwa sababu kwa utaratibu mzuri ni kwamba, Taarifa ya *CAG*, imewekwa hapa Mezani, na majibu ya Serikali na uchambuzi unafanywa na Kamati,

[NAIBU SPIKA]
halafu Wenyeviti wa Kamati wanatuletea taarifa zao baada ya kuwa sasa zimeshachambuliwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunapojadili zile Taarifa za Wenyeviti wa Kamati pale ndiyo mahali pake hasa pa kuona hiki kitu kweli ni wizi, na hiki kitu siyo kweli ni wizi. Kwa sababu siyo kweli kwamba kila kitu kilichoandikwa katika Taarifa ya *CAG* huwa ni kweli kwa asilimia 100, siyo kweli hata kidogo! *(Makofi)*

Kwa hiyo, unaweza ukajikuta hapa kwa kweli tunafika mahali ambapo hatuelewani kabisa. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwa sababu ya *Order Paper* yetu inavyojiekeza moja kwa moja, *Order Paper* yetu ukiisoma leo ukurasa ule wa mwisho, ukurasa wa 11 ni Hoja za Kamati ambapo hoja zilizoko Mezani ni Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ameleta hotuba yake hapa; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, ameleta hotuba yake hapa; na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Tukijikita hapo itakuwa vizuri sana, japo mimi simfungi Mbunge mwingine yeyote kuongelea kitu kingine chochote ambacho ni *relevant.* Sina nia ya kuwafunga.

Muda wa Mheshimiwa Pauline Gekul, uendelee kulindwa Makatibu. Huo ulikuwa ni ushauri kwa ujumla tu.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, lakini naomba tu nikubaliane na wewe kwamba kinachojadiliwa ni Taarifa ya *LAAC*, lakini taarifa ya *LAAC* imechambua yale yote ambayo yameonekana kwenye vitabu vya *CAG,* na kile ambacho ninakisema katika ukurasa 13 kwenye taarifa hii ya Kamati imeeleza yale yale ambayo nilikuwa nakisema, katika Jedwali Na.4, Mwenendo wa Mishahara iliyolipwa kwa watumishi waliotoroka, waliostaafu na waliofariki. Zaidi ya Sh. 693,000,000/= *the same,* kitu ambacho nilikuwa nakijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuwaeleza Watanzania jinsi ambavyo fedha zao zimetafunwa. Malipo yenye nyaraka pungufu nimesema ni

[MHE. PAULINE P. GEKUL]
Shilingi bilioni 3.367, na Kamati imeonesha, hizi fedha ni nyingi sana. Nilikuwa nazungumzia fedha za MMAM, Mpango wa Afya ya Msingi, zaidi ya Shilingi bilioni mbili hazijafanya kazi. Hii yote Watanzania wanafahamu kwamba wanachangia tofali, wanachangia mchanga, lakini Serikali inapeleka hizi pesa mwishoni mwa mwaka wa Bajeti, fedha hazifanyi kazi. Hii inasababisha Watanzania wanakosa huduma. Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi, misamaha ya kodi katika nchi hii inatisha. Watanzania wafahamu kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi, inasamehe zaidi ya Shilingi bilioni 789 misamaha ya kodi. Imeelezwa jana wakati Kamati hizi zinasoma, wameleta hizi takwimu. Shilingi bilioni 789 ni misamaha ya kodi, lakini Mama Lishe yule anayepika tu kachapati, anafuatwa kodi. Yule Machinga anayetembeza nguo mkononi, anafuatwa kodi. Kila mtu nchi hii analipa kodi, wafanyakazi wanalipa kodi; lakini Serikali inasamehe zaidi ya Shilingi bilioni 789.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi, Makampuni Makubwa nchi hii ndiyo yanayoongoza kwa kusamehewa kodi. Twende kwenye Makampuni ya Simu. Makampuni ya Simu, *TCRA* wao wameshindwa ku-*control.* Lakini nitoe mfano wa Kampuni ya *Airtel.* Kampuni ya *Airtel* katika mwaka huu ambao tunajadili mahesabu yake, dakika zaidi ya 4,847,000,000 ndizo zilitakiwa zilipiwe kodi. Kwa sababu ya Serikali dhaifu ya Chama cha Mapinduzi, hawa *Airtel* wakaonyesha ni dakika 4,233,000,000, tofauti ya dakika 614,000,000 hazikulipiwa kodi. Ni fedha kiasi gani kwa Kampuni hii moja tu ya *Airtel,* imeonyeshwa katika Taarifa za Kamati. Tuna Makampuni ya Simu zaidi ya matano katika nchi hii; Kampuni moja kama ina uwezo wa kuficha dakika 614,000,000, ukipiga kwa *VAT* ya asilimia 18 ni dakika ngapi na ni kodi kiasi gani? Ni zaidi ya Shilingi bilioni 30 Kampuni moja inashindwa kulipa, wastani huo. Makampuni mangapi nchi hii hawalipi kodi?

Mheshimwia Naibu Spika, lakini Mtanzania huyu huyu, ukienda kwenye nchi za wengine huwa hawanunui *line* ya

simu, ile *chip.* Nchi yetu tuna nunua *line,* nchi yetu tunanunua muda wa maongezi, nchi yetu tunachukuliwa Sh. 1,000/= kila mwisho wa mwezi kwa kila *line.* Hii ndiyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi! Ni Serikali dhaifu, hata Baba wa Taifa alisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba tu Watanzania, haya yote hayavumiliki. Tunayavumilia kwa sababu kuna watu bado wanaichagua Serikali ya CCM ambayo imeshindwa kuongoza nchi hii kwa ubadhilifu wa fedha za Watanzania kwa kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wafahamu, kuendelea kukichagua Chama cha Mapinduzi ni kuendelea kulalamika na kuendelea kutokuona matokeo ya fedha za kodi zao. Ni vizuri wakafanya maamuzi wakajua ni kiasi gani wanachopoteza kwa kila mwaka ili wafanye tathmini waone kuna sababu gani ya kuendelea kukaa na watu ambao hata Walimu wameshindwa kuwalipa posho za mazingira magumu; Maaskari wao wanaidai Serikali malimbikizo; lakini barabara hizo zinazojengwa zilitakiwa zijengwe miaka 20 iliyopita, leo wanajivunia kujenga barabara za Mikoa, halafu wanasema wanajenga barabara; miradi ya maji imeshindikana; mnawadanganya Watanzania mnajenga visima vya Maji vya *World Bank* imekuwa ni wimbo. Watanzania wapime. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wizi unaofanywa na Serikali kwa utendaji mbovu unatisha. Kwa kweli msipodhibiti, ni vizuri mkaondoka mdarakani mapema sana. Nitoe mfano wa Wizara ya Ujenzi katika Mahesabu haya. Katika Bunge hili tulipitisha bajeti ya zaidi ya Shilingi bilioni 252, wakasema ni kwa ajili ya miradi maalum, lakini wakaieleza Kamati kwamba hizi fedha zilikuwa ni za madeni, zinakwenda kulipa madeni. Lakini bado hata haikuoneshwa kwamba ni madeni gani yaliyolipwa na hizi fedha ziliombwa hapa mnakumbuka Waheshimiwa Wabunge, lakini huko sasa katika utendaji hazijulikani zimetumikaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Watanzania, nchi yetu siyo maskini. Miaka 52 ya uhuru ni vizuri tukajitafakari.

[MHE. PAULINE P. GEKUL]

Hakuna sababu ya akina mama kujifungulia chini, wakalala chini kama mabilioni ya pesa yanatumika kiasi hiki! Hakuna sababu Walimu kutokupata posho ya mazingira magumu kama fedha hizi TAMISEMI mmeshindwa kuzisimamia. Nilisimama hapa Bungeni nikasema Waziri Mkuu ajiuzulu wakati wa *Operation* Kimbunga. Lakini kumbe huku fedha zinaibiwa, mimi nilifikiri tu walishindwa kusimamia yale masuala ya *operation.* Ni vizuri Waziri Mkuu akaondoka mapema sana na Mawaziri wake, hatuna sababu! Lakini tukifanya *analysis* ya kutosha, hata kila mwaka tukiwaondoa hawa Mawaziri siyo *solution* Watanzania. *solution* ya matatizo yetu ni kuondoa Chama ambacho kimeshindwa kusimamia Serikali iliyoko madarakani.

Waheshimiwa Wabunge, tutawaondoa Mawaziri, ataondoka leo Mheshimiwa Mama Ghasia pale, ataingia mwingine, ni waambie, hamtaweza kuongoza nchi hii, kwa sababu mfumo mzima umejaa rushwa na Chama kimeshindwa kukemea. Kwa hiyo, msiwapigie kelele tu hao waondoke. Nyinyi wote mnafanana, hakuna tofauti! Ataondoka huyu ataingi Yule, wote ni mfumo ule ule, hamtasimamia Serikali hii. Watanzania wawaadhibu kwa kuwaondoa kwenye masanduku ya kura haraka sana, kwa sababu pesa zao zinaibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niseme kwamba hii *doze* inatosha kwa leo na wengine wataiendeleza. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, nimekuona umesimama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni yetu ya 64(1) nimemvumilia sana huyu Mheshimiwa kwa sababu ni Mbunge wa Viti Maalum, Dada yangu, nimeshindwa kumzuia hotuba yake. Lakini nataka kusema, siyo kwamba sisi hatuwezi kusema, tuna uwezo wa kusema sana. Lakini nataka kusema kwamba katika hotuba yake amevunja kabisa Kanuni ya 64(1) yote, ameivunja kwa makusudi.

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kanuni hiyo ya 64(1) inasema hivi: "Mbunge yeyote hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala," yaani mambo yote anayoyazungumza hapa hayako kwenye hotuba ya Wenyeviti waliyotoa. "Hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine." Amezungumza matusi matupu hapa.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): "Hatatumia lugha ya kuudhi na inayodhalilisha watu wengine."

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni watu wazima, wastarabu, hata ungesema namna gani, bado unaweza ukatumia lugha ya kistarabu na ujumbe wako ukafika. Tunazungumzia mahesabu ya Serikali kama taarifa zilizoletwa na Wenyeviti.

Nawashauri Waheshimiwa Wabunge kwamba tutumie lugha ile ile ili angalau Watanzania huko watufuatilie wajue tunachofanya hapa ndani, badala ya kutumia dakika Kati ya dakika 15 kutukana, kashfa, kusingizia CCM. Hapa hakuna CCM hapa! Sisi wote hapa ni Wabunge. Hivi leo tukianza kuchambua ya CHADEMA, *CUF, NCCR*, tutamaliza hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba mwongozo wako ili angalau uturudishe kwenye mstari, tuzungumze kwa staha, kwa heshima ili wananchi waweze kutufuatilia vizuri.

NAIBU SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie Kanuni ya 68(7) nami naomba mwongozo wako juu ya hiki ambacho tunakijadili. Sisi ratiba ya Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge ambayo tumepewa kuanzia tarehe 3 Desemba, 2013 hadi tarehe 20 Desemba, 2013, ukiangalia siku ya tarehe 6 Desemba, 2013, Ijumaa, moja ya jambo ambalo lilipangwa mapema, ulisema mwenyewe pengine ulikuwa haupo, ni taarifa za *CAG*. Wajibu wa Serikali na Kamati za Bunge katika kusimamia fedha za umma. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba mpunguze makofi kwa sababu inanifanya nisimsikie alichokuwa anakisema. Naomba urudie tena.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 3 Desemba, 2013 ratiba hii ilipopangwa mpaka tarehe 20 Desemba, 2013, Tarehe 6 Desemba, ratiba tuliyopewa na Bunge lako Tukufu, siku ya Ijumaa, ilikuwa inasema kwamba ni Taarifa ya *CAG*: Majibu ya Serikali na Kamati ya Bunge inayosimamia fedha za Umma; Kamati ya Hesabu za Serikali; Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa; na Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumamosi pia ratiba ikaeleza tarehe 7 Desemba, 2013 mapema tu, katika ratiba ya awali pia taarifa ya CAG: Majibu ya Serikali za Kamati za Bunge za kusimamia fedha za Umma; inaendela kila mahali taarifa ya *CAG*, mpaka Jumanne na kuendelea mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapotuambia wewe hasa kwamba hapa sasa *CAG* haipo na haihusiki haitachambuliwa, kidogo mimi napata wasiwasi, napata kigugumizi juu ya jambo ulilolizungumza wakati ratiba hii ya Bunge mliyoitoa nyinyi wenyewe uongozi wa Bunge, sisi inaturuhusu juu ya kujadili suala hili la *CAG*. Ni kawaida mara zote tunapojadili taarifa hizi *CAG* na hata wenyewe Wenyeviti wa Kamati walivyochukua wamedondoa kwenye taarifa ya

[MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM]
CAG; hili ni jambo la kawaida, lipo. Naomba mwongozo wako.

Ratiba yenu mnatuletea tujadili taarifa ya *CAG*, wewe Kiti unasema tusiijadili ya *CAG*. Naomba mwongozo wako juu ya jambo lililopo mbele yetu. Nakushukuru sana. *(Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Wenje.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mimi naomba kuhusu utaratibu kanuni ya 68(1) ikisomwa pamoja na kanuni ya 64.

Mheshimiwa Naibu spika, ni kweli kwamba maneno aliyozungumza Mheshimiwa Pauline Gekul yanachoma sana kwa upande wa Serikali, lakini pia ni ukweli kwamba hajatoa neno la tusi hata moja. Kwa maana hiyo Mheshimiwa Lukuvi anasema uongo Bungeni kwamba Mheshimiwa Pauline Gekul ametoa neno la tusi, pamoja na kwamba maneno aliyosema yanaumiza sana. Naomba Mheshimiwa Lukuvi athibitishe hayo matusi anayosema, na siyo busara kwa Mzee kama Lukuvi kusema uongo Bungeni. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, niwaombe utulivu na amani, vile vile naomba mjikite katika jambo lililo mbele yetu. Kinachotuongoza siku zote katika Bunge huwa ni hii karatasi yetu na kwa makusudi kabisa, uongozi wa Bunge zamani ilikuwa ni karatasi nyeupe tu kwa wale Wabunge wa siku nyingi, lakini tulibadilisha rangi makusudi ili usiichanganye na karatasi nyingine zozote zile. Unapoishika unajua hii ndiyo inayoongoza shughuli za leo.

Sasa ukiikamata hii karatasi yetu ambayo ndiyo mwongozo wa shughuli za leo, ukurasa wa mwisho na ndiyo maana tunamwita Katibu, anatuongoza: “Hoja za Kamati”. Utaona hoja za Kamati zilivyokaa, ni mawasilisho ya Wenyeviti wetu watatu. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa - Mheshimiwa Rajab, ripoti yake ni ndogo sana ina kurasa chache tu na unaweza ukaipitia hata kwa dakika kumi tu. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti -

[NAIBU SPIKA]
Mheshimiwa Chenge na Mwenyekiti wa Hesabu za Serikali Kuu - Mheshimiwa Zitto Kabwe. Ripoti zote tunazo. Kwa maana ya uongozi wa Bunge wa leo hicho ndicho ambacho tunakijadili kwa kweli.

Kwa hiyo, ni vizuri tukajikita kufuatana na kile ambacho kipo katika mwongozo wetu na ni wajibu wangu kama Kiti kuwaongoza Wabunge na siyo kuwazuia kujadili chochote ambacho hakipo.

Waheshimiwa Wabunge, tukipanua wigo kwa mambo ambayo hayapo yanatuletea tatizo kubwa sana la namna ya kuenenda. Kwa mfano, mambo mengi aliyokuwa anayaongea Mheshimiwa Pauline Gekul mimi nilikuwa nashangaa mezani hapa, ndiyo maana nilikuwa nawauliza Makatibu kwamba hiki kitu kipo wapi? Nilikuwa Napata taabu sana ya ufuatiliaji na Wenyeviti wetu watakavyokuwa wanakuja kujibu hoja mwishoni sasa sijui watajibu vipi hoja hizi zinazoongelewa na ambazo hazipo.

Vile vile suala la kutumia lugha ya staha, hilo ni muhimu kwa sisi Wabunge wote na nina hakika kabisa mkifungulia mbwa hapa, ninyi nyote ni Wanasiasa, mna uwezo mkubwa kabisa wa kurusha makombora ya kila aina na patakuwa hapatoshi.

Kwa hiyo, ni wajibu wetu kila wakati kwa kweli kuwarudisha kwenye mada, maana ya kuongea yapo. Kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge fulani fulani, ukishaanza kuingiza habari ya CCM, CHADEMA na kadhalika ya kusema yapo, tena watu wana hamu nayo kwa hiyo, ningependa msiende sana huko kwa sababu ...*(Kicheko)*

Tufungulie Mbwa?

WAJUMBE: Ndiyoo!

NAIBU SPIKA: Hapana, hapana. Kanuni haziruhusu. Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hizi ripoti tatu za Wenyeviti wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aprili, 2012 Wenyeviti wa Kamati mbalimbali waliwasilisha ripoti kwenye Bunge lako Tukufu na zilijadiliwa na Waheshimiwa Wabunge. Lakini kwa masikitiko makubwa, Serikali mpaka leo haiku-*respond*, haikutoa majibu kwenye yale majadiliano na yale maazimio ambayo Bunge lako Tukufu lilipitisha mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majadiliano haya yanayoendelea leo hii yapatiwe majibu. Naamini kabisa, kama majibu yangekuwa yamepatikana mapema, basi yale yaliyokuwa yamejitokeza mwaka 2012 ambayo yamejitokeza tena mwaka huu kwenye hoja za Wenyeviti yasingejitokeza tena. Kwa hiyo, naomba sana Serikali itoe majibu haraka iwezekanavyo kwa Waheshimiwa Wabunge na tujue hatua zipi wanazochukua katika maeneo ambayo yamelalamikiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia matumizi mabaya ya fedha za Serikali, yaani *misappropriation of the Government Fund.* Katika ripoti zote tatu zinazungumzia sana matumizi mabaya ya pesa, na Serikali imekaa kimya, hakuna hatua zozote inazochukua kwenye maeneo ambayo yanalalamikiwa na Wabunge. Huu ni udhaifu! Naomba Waheshimiwa Mawaziri wahusika kwenye maeneo hayo ili kusudi watutendee wema sisi Wabunge ambao tunalalamikia ubadhilifu wa fedha, basi wachukue hatua. Wakiendelea kunyamaza kimya, hizi hoja zinazotoka kwa Wabunge wengine kwamba kuna matumizi mabaya ya fedha na wenyewe ni sehemu ya matumizi itaonekana ni kweli. Naomba wachukue hatua za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika matumizi mabaya ya fedha ni kweli tunalalamikiwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, lakini na wenzetu wa CHADEMA wameanza kuonekana kwenye baadhi ya maeneo. Wanajikopesha fedha za ruzuku, mmoja wa Wenyeviti amelalamikia suala la

[MHE. M. H. MGIMWA]
kutokuwasilisha hesabu, nao umekuwa mgogoro. Lakini ikumbukwe tu kwamba Mdhibiti Mkuu huyu anafanya kazi ya kukagua shughuli za Serikali na siyo za CCM.

Kwa hiyo, tunapozungumza hapa, tuzungumzie habari ya Serikali na siyo habari ya Chama cha Mapinduzi. Tukitaka tujielekeze kwenye Vyama, basi hakuna Chama ambacho kiko salama hapa. Tunaona kwa sababu mmeanza hadi kufukuzana kwa sababu mmoja tu ametoa hoja ya msingi kwamba hapa hapako sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika,...

NAIBU SPIKA: Nilisema mapema! Mheshimiwa Mgimwa, endelea! *(Kicheko/Makofi)*

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama msemo unavyosema kwamba, unapomnyooshea mwenzako kidole kimoja, vinakuja vidole vinne kwako. Kama eneo dogo tu la ruzuku umeshindwa kulikabili: Je, ukipewa nchi itakuwaje?

Kwa hiyo, Watanzania wanaanza kujifunza kwamba hawa jamaa tumewapa fedha kidogo tu ili ziwasaidie wao kukikuza chama chao lakini wanagombania hizo fedha sasa tukiwapa nchi itakuwaje? *(Makofi)*

MJUMBE FULANI: Watatumaliza!

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni malipo ya mishahara ya watumishi hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mgimwa, naomba umpe nafasi Mheshimia Aliko Kibona.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji anayeendelea anaonekana kukiuka kile ambacho umetukataza. Mimi naomba nimpe taarifa kwamba Mheshimiwa Naibu Spika ametushauri tuache kushambuliana kivyama. Ni taarifa tu!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Silinde, nini tena?

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako wa Kanuni ya 68(7) kulingana na kanuni 64(f) na (g).

Lengo la mwongozo wangu ni kwamba wakati una *wind up* umesema kwamba unataka kufungulia mbwa. Sasa mimi nataka nifahamu tu kwamba mbwa ndiyo Wabunge wapi? Waheshimiwa Wabunge wa CCM ndio mbwa? Kwa nini umewaita mbwa? Kama hakuna mbwa, naomba urekebishe kauli yako. *(Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Nafikiri hapa kuna umuhimu wa Mheshimiwa Keissy akapata nafasi kidogo kutuweka sawa kabla hatujaendelea.

Mheshimiwa Keissy, nilikuona ulisimama wakati fulani!

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Mimi naona lawama zinawafikia Serikali ya CCM na sisi Waheshimiwa Wabunge wote lawama zinatufikia, maana yake ni Madiwani, pesa zinakwenda Majimboni, Waheshimiwa Wabunge wanazifuata huko na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaomba *diesel* kwa Wakurugenzi na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wako humu Bungeni, vikao vinafanyika kule, wanawekewa fedha wanaghushiwa saini kule wanakwenda kuzichukua. Kwa hiyo, na Waheshimiwa Wabunge wote wawajibike, hawafai! *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, endelea. Miongozo hii nitaitolea ufafanuzi mwishoni.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba nichangie kuhusu manunuzi yasiyo na nyaraka za malipo. Hili ni tatizo! Mimi nashangaa kwenye Halmashauri tuna Wahasibu waliobobea na tumewaajiri wenyewe na sisi Waheshimiwa Wabungeni ni Madiwani katika hayo maeneo. Haya manunuzi yasiyo na nyaraka yanafanyika kule na tunayaangalia na hapa tunakuja kumlaumu Waziri wa TAMISEMI. Sisi ni sehemu ya matatizo kwenye maeneo tunakotoka kwa sababu Mbunge ni Diwani katika Jimbo lake la uchaguzi.

Kwa hiyo, tunatakiwa tujiangaliane na sisi kwenye maeneo yetu, ni kasi gani tunakemea matumizi mabaya ya fedha? Tusiilaumu tu Serikali! Tunapoishauri Serikali tukashindwa, ndiyo tuoneshe kwamba tuliishauri Serikali hapa na tukashindwa. Kuna baadhi ya maeneo mengine Halmashauri hizo zinaongozwa na Vyama vya Upinzani na matumizi mabaya ya fedha yapo kwenye maeneo hayo, ripoti si zipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni Serikali kutuma fedha zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa. Hili ni tatizo na nataka Serikali ijiangalie kwenye eneo hili. Sisi Wabunge tunalalamikia na inaonekana ni sehemu ambayo Serikali inapeleka fedha kwa ajili ya kujipasia. Tuliangalie hili jambo, tupeleke fedha kutokana na matumizi yanayohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kuchangia ni deni la Taifa. Deni la Taifa sasa hivi lipo 47%, tumebakiza 3% tu kufikia kwamba hatuwezi kukopesheka. Naomba Bunge lako Tukufu litoe maelekezo sasa hivi kwenye Serikali yetu kwamba wasikope bila kupata idhini ya Bunge lako Tukufu. *Otherwise* tutakuwa hatukopesheki kabisa katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kuchangia ni suala la Serikali kushindwa kupeleka 10% kwa ajili ya akina mama na vijana. Hili ni tatizo na siyo tatizo kwetu tu bali ni kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Akina

mama na vijana wanatakiwa wasaidiwe. Nataka Serikali ijiangalie upya kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kuchelewesha kupeleka ruzuku kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Baada ya Bunge lako Tukufu, sisi Waheshimiwa Wabunge tukirudi kwenye maeneo yetu huwa tunatangaza kwamba Bunge letu limepitisha hiki na tutafanya hiki na kile, lakini kuchelewesha kupeleka ruzuku kwa ajili ya shughuli za maendeleo ni tatizo na hili linaweza likasababisha sisi Wabunge wote tusirudi hapa. Naiomba Serikali iliangalie hili jambo kwa upana wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni watuhumiwa wa ufisadi kuhamishwa vituo. Kila mtu anapofanya dhambi katika kituo kimoja anahamishwa kwenye eneo lingine. Hili ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mimi nina *DMO* alifanya kosa Kasulu, alifanya matumizi mabaya ya fedha Kasulu sasa hivi wamempeleka Mufindi na Mufindi sasa hivi hapatawaliki. Kwa hiyo, kumhamisha mtu kutoka kwenye eneo moja kumpeleka kwenye eneo lingine siyo *solution.* Kama mtu kafanya kosa tumtoe katika kazi. Hili limekuwa ni tatizo kubwa sana na ndiyo maana tunasema kwamba tunalindana, hatuna sababu ya kulindana. Sasa hivi sisi kama Watanzania tuna raslimali nyingi na tuna vijana wengi wamemaliza vyuo hawana kazi; mtu kama ameshindwa kufanya kazi aondolewe kwenye eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ninalotaka kulizungumzia ni udhaifu katika usimamizi na utekelezaji wa Sheria za Manunuzi ya Umma. Hiki kimekuwa ni kichaka, watu wengi wanajificha hapa na ubadhirifu mkubwa unafanyika katika maeneo haya na sheria hazifuatwi. Bunge lako Tukufu ni vyema likatengeneza utaratibu mpya wa kutunga sheria mpya kwa ajili ya Sheria za Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa kwa mchango wako wa mchana wa leo.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyojua macho na masikio ya dunia kwa hivi sasa yanaelekezwa kwenye uwanja wa *FNB Soweto Johannesburg South Africa* kwenye shughuli kubwa inayohusiana na msiba wa Mzee wetu Nelson Mandela na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano amekwenda kutuwakilisha Watanzania; ningependa kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba katika mazingira hayo, *TBC* nayo inajiunga huko kuanzia itakapofika saa 6.00. Kwa hiyo, tutaendelea kumalizia muda wetu huu bila matangazo ya *TBC* kwa ajili hiyo.

Sasa namwita Mheshimiwa Leticia Nyerere atafuatiwa na Mheshimiwa Moza Abeid.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia hoja za Kamati ya Hesabu za Serikali, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafurahi na ninashukuru kwamba nimepata nafasi kuchangia baada ya Waheshimiwa wengi kuchangia ndani ya Bunge. Baada ya Waheshimiwa Wabunge kuchangia kwa umakini kabisa, nimegundua tatizo kubwa la nchi yetu ni raslimali watu yaani *human resource.* Tatizo lingine ambalo nimeligundua baada ya kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge kwa makini ni tatizo la *law enforcement* katika Taifa letu. Hatuna utawala wa kisheria na kama upo unahitaji maboresho ya hali ya juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la *human resource* au raslimali watu linaweza ama likaangusha Taifa ama likafanikisha Taifa lolote lile duniani. Kwa sababu hizo nilizozisema, kuna haja sasa ya Taifa letu kuangalia pamoja na mambo mengine kutoa kipaumbele katika *human resource* na *law enforcement*. Hatuna ujanja! Vinginevyo, kila siku tutafukuzana na kubadilishana, lakini ukweli wa mambo

ni kuboresha maeneo hayo ukizingatia kwamba sisi wote tunatolewa kwenye kapu moja hilo hilo. Kama kuna udhaifu katika *human resource* ni lazima Serikali ijikite kuliangalia tatizo hili na kulifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Kwimba imeshindwa kutekeleza baadhi ya miradi. Hii siyo kwa sababu Mkurugenzi Pendo Malebelwa ameshindwa kazi, hapana. Ni kwa sababu ya utaratibu uliopo wa kutengeneza bajeti kwa kutegemea wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapopanga bajeti kwa kutegemea wafadhili, ni sawa na kupanga tarehe ya kwenda kujifungua wakati ukijua fika huna ujauzito. Ni lazima tuliangalie hilo kwa umakini zaidi. *(Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Leticia, mpya hiyo! Endelea kuchangia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, Halmashauri imeshindwa kutekeleza miradi kwa sababu ya matatizo mbalimbali. Halmashauri ya Kwimba ina matatizo kwenye suala la maji.

Mheshimwa Naibu Spika, katika hili wewe ni shahidi, nimekuwa nikiimba wimbo wa maji Ngudu Kwimba, maji Ngudu Kwimba, mpaka nimechoka. Kwa kutambua tatizo la fedha na ninakiri kwamba hata Serikali siyo makusudi yake, ni tatizo lililoko kwenye mfumo wetu. Kwa hiyo, ndiyo maana hivi karibuni hujanisikia nikiimba maji Ngudu Kwimba, maji Ngudu Kwimba kwa kutambua kwamba Serikali haina pesa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimekuja na ufumbuzi mwingine. Wakati tunasubiria utekelezaji wa ahadi za Serikali kuhusu maji, nimeamua niungane na wananchi wa Kwimba tufanye harambee ya kusafisha mabwawa yetu, yaani kutoa matope kwenye mabwawa kwa kushirikiana na Waheshimiwa Mawaziri husika.

[MHE. LETICIA M. NYERERE]

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, naomba nitakapoita hiyo harambee mapema mwaka ujao, naomba Mawaziri wote wanaohusika na suala la maji waje Kwimba twende Mwamasururu twende tukasafishe bwawa la Mwamasururu. Tunapowaita, hatuwaiti waje kama wageni rasmi, tunawaita kama watendaji waje waungane na sisi kuondoa tope katika mabwawa haya ili wananchi wa Ngudu na Kwimba wapate maji wakati tunasubiria hizo ahadi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kwimba hawana tatizo la maji tu, *education system* yetu ina matatizo makubwa. Hatuna Walimu wa kutosha, hatuna nyumba za Walimu na hatuna madawati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu, Shule za Halmashauri ya Kwimba tumekuwa tukitumia mawe kwa ajili ya kukalia watoto wetu. Bahati mbaya matumizi yamekuwa makubwa kuliko mawe yaliyoko hapo Kwimba na watoto wengine wanalazimika kwenda kufuata mawe Misungwi Jimboni kwa Mheshimiwa Kitwanga. Lakini naye endapo atatushtukia...

NAIBU SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Ndassa. Mheshimiwa Leticia dakika mbili. Mheshimiwa Ndassa tafadhali.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmoja wa Wabunge wa Jimbo la Sumve na Wilaya ya Kwimba. Wilaya ya Kwimba nataka nimpe taarifa dada yangu na nimshauri, ni vizuri kama Mbunge wa eneo lile, awe anahudhuria vikao vya Halmashauri. Kwa sababu haya anayoyasema ni kuwapotosha na kuwadanganya wananchi wa Kwimba. Mpango wa maji ulivyo sasa kupitia Wizara ya Maji na Waziri anafahamu, mwishoni mwa mwezi huu, Waziri wa Maji atakuja azindue mradi mkubwa wa maji katika Wilaya ya Kwimba Kijiji cha Ngudu. Lakini ni vizuri zaidi na siyo tabia nzuri kuwazalilisha watoto wa Wilaya ya Kwimba kwamba wanafuata mawe Wilaya ya Misungwi kwa ajili ya kukalia. Huko ni kuwadhalilisha.

[MHE. RICHARD M. NDASSA]

Ningeshukuru zaidi kama Mbunge kwa jitihada zake angesema, mimi nina utaratibu huu, nimeshanunua madawati 200, 300 kwa ajili ya Shule fulani. Ningeshukuru zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kazi inayofanywa na Mheshimiwa Mansoor hivi sasa yeye mwenyewe ya kuchimba mabwawa, ni kubwa sana ili tu tufike mahali tuwashukuru kwa kazi nzuri wanayofanya. Lakini siyo vizuri kama Mbunge kusimama hapa na kupotosha.

Nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Leticia unapokea taarifa hii? Endelea kuchangia tena.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi sijasema kwamba Serikali haifuatilii tatizo la maji na ninamsihi awe anasikiliza wakati watu wananchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, wapo wanafunzi wanaokaa kwenye mawe na kama alitaka nibebe mawe kuleta kama ushahidi, sifanyi kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona niendelee. Wananchi wangu wa Jimbo ninaloishi Kwimba wana matatizo. Nimeyataja machache kwa mfano maji ni tatizo, nimetaja vifaa vya shule, ni matatizo; nyumba za Waalimu, ni matatizo; na hata wananchi wenyewe wanaponisikiliza hapa, kwa kweli wanaamini kwamba ninawatakia mema kwa sababu nasema ukweli wa jambo lilivyo. Sina sababu ya kuficha, nataka kumficha nani? Kwa manufaa ya nani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Leticia dakika moja tu, namwona Mheshimiwa Keissy amesimama. Mheshimiwa Keissy.

MHE. ALLY K. MOHAMED:...*(microphone haikurekodi mazungumzo yake)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kombo nimekuona.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Inaonekana uwezo wako unachukuliwa na Wabunge mmoja mmoja. Wasa wao ndio wanaojibu, wanamjibu Mbunge huyu na Mbunge huyu kwa wanavyoona wao. Katika Bunge ni haki yake kusema, kunung'unika, kasema, katukana wakati mwingine, lakini sasa ananyanyuka huyu anamzuia Mbunge japo kanuni inakubali; anajibu yeye, anakuja na mwingine anasema siyo kazi ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Machali, ulisimama.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nasimama kwa mujibu wa kanuni ya 64 (1) (a), kwamba Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa tu nahitaji pengine kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge; baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanakemea kutokujadili mambo ambayo yanazihusu Halmashauri zetu, na hapa ningeomba nim-*cite* kidogo moja kwa moja Mheshimiwa mzee wangu Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy ambaye namheshimiwa na ni rafiki yangu sana.

Unapojadili matatizo ya maji au ukosefu wa madawati, labda fedha zimeliwa, ni sehemu ya taarifa za hesabu za Serikali za Mitaa na taarifa ya *LAAC* imewasilishwa wiki jana.

Kwa hiyo, inasikitisha sana kuona Mbunge anasimama kabisa kifua mbele, ametoa misuli, amechachamaa kweli anasema kwamba tunachojadili ni kitu ambacho kiko nje ya utaratibu. Turudi kwenye mstari nafikiri tujadili mambo ambayo yanatuhusu.

[MHE. MOSES J. MACHALI]

Kwa hiyo, Mheshimiwa Keissy naomba tuwe makini sana. Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Leticia Nyerere muda wako umelindwa.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba nianze na Mheshimiwa Keissy. Kwanza nasikitika kwamba hajui hata kazi za TAMISEMI, kwa hiyo, nampa pole sana kwa hilo. Lakini ndiyo hivyo, usikate tamaa. Tuna mwendo mrefu, bado una muda wa kujifunza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna usemi unaosema: "*you can not give what you do not have".* Kwa hiyo, siwezi nikatarajia mambo muhimu zaidi kutoka kwako Mheshimiwa Keissy.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia matatizo ya Halmashauri ya Kwimba na maana yangu ni kwamba hawa watu kwenye Halmashauri zetu wanajikuta wamekwama kwa sababu Serikali kuu haiwaletei pesa. Serikali kuu hii haipeleki pesa kwa sababu na yenyewe imekwama. Wafadhili wanapotoa ahadi kwamba watawaletea asilimia 80 ya bajeti yetu hawaleti. Sasa utafanya nini? Lakini kama nilivyosema, tujikite kwenye rasilimali watu, tuboreshe rasilimali watu ili tuweze kufanikisha hata haya mambo ya kutafuta fedha kwa wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfadhili anapokwambia atakusaidia kwenye bajeti yako, atakuletea pesa, haimaanishi kwamba siku moja atakuja, atagonga mlango wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha akiwa na furushi la pesa, hapana. Tunatakiwa tuwe *aggressive* kufuatilia hizi ahadi. Kuna ahadi ambazo huwa ni za kweli, kuna ahadi ambazo zinatakiwa zifuatiliwe kwa karibu sana na ndiyo maana rasilimali watu kwa hali yoyote ile tunahitaji kuiboresha ili tusitingwe na haya matatizo ya kukosa hata pesa ambayo iko ndani ya bajeti.

[MHE. LETICA M. NYERERE]

Mheshimiwa Naibu Spika, tuboreshe pia *our law enforcement system*, haiko imara. Watu wanachukua sheria mkononi. Hakuna mtu anayeogopa sheria nchi hii. Hili ni tatizo kubwa, tusipoliangalia kwa macho mawili hakika tutaangamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutalaumiana wee kuonesheana vidole, sijui huyu hajui na yule hajui, lakini hata leo mimi mkiniweka Wizara yoyote huko, kama mfumo wa Serikali ni mfu, sitaweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini muda wangu bado upo kama ulivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi huko Kwimba, nimezungumzia harambee ya kusafisha marambo yetu kuondoa tope. Nawaalika Waheshimiwa Mawaziri mnaohusika mje mtuunge mkono, tusafishe mabwawa yetu wakati tunasubiria ahadi ya Serikali kutimizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona niishie hapa na naomba kuwasilisha. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere. Sasa namwita Mheshimiwa Moza Abeid, atafuatiwa na Mheshimiwa Christina Mughwai Lissu.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mie niweze kuchangia Muswada ulioko mbele yetu kuhusu Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuanza kabisa na suala la malipo ya mishahara hewa. Nilikuwa napata kigugumizi kikubwa sana kuona kwamba katika kila Halmashauri inalalamikia kuhusiana na masuala ya mishahara hewa. Sasa nilikuwa najiuliza, hii mishahara hewa ni nini maana yake? Je, mshahara huu uliokuwa hewa, unalipwa mtu bila yeye mwenyewe kuwepo; Wakaguzi hawapo? Je, katika Halmashauri, hakuna idadi kamili ya Wafanyakazi?

[MHE. MOZA A. SAIDY]

Napenda kunukuu katika Bunge lililopita kwamba kuna kipindi tuliahidi kwenye Bunge kwamba kuwa ipo siku itatengwa maalum kwa kubaini mishahara hewa: Je, mishahara hiyo hewa imekwisha kubainika? Je, imeshagundulika na kama imegundulika, kuna hatua gani zilizofanyika katika Halmashauri zetu? Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho yake atueleze hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye mada ya pili kuhusu kucheleweshwa kwa ruzuku. Hili limekuwa ni suala gumu sana! Suala la ucheleweshaji wa ruzuku katika kila Halmashauri katika nchi yetu hasa katika Wilaya yangu ninapotoka katika Halmashauri ya Kondoa, imekuwa ni kero kubwa. Ruzuku hii haifiki kwa wakati muafaka. Mfano, mradi wa barabara. Barabara zinatakiwa zitengenezwe wakati wa kiangazi, lakini zinakuja kutengenezwa wakati unakaribia wa masika na barabara hizi hazimaliziki. Kumechimbwa mifereji, kumechimbwa barabara sasa hivi kumekuwa kama vile, yaani ili mradi barabara hakuna na nyingine zinakaribia kujifunga.

Ningeomba kwamba Mheshimiwa Waziri angekwenda atembelee katika Halmashauri ya Kondoa, yaani bila kwenda kutembezwa maana yake kuna ule mpango Waziri anafika, barabara inatengenezwa ili apite kwenye barabara nzuri. Mimi naona kwamba ungefika hata wakati huu tu ukatoka hapa sasa hivi na gari yako ukatembea Mitaa yote ya Kondoa uone ndani ya Mitaa yenyewe zipo barabara hizo au zimekwishajifunga?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo kwenye ucheleweshaji wa ruzuku, kumekuwa na upendeleo mkubwa sana. Wilaya nyingine zinapewa hela nyingi, Wilaya nyingine zinapewa hela chache, haziwezi kukidhi haja ya miradi ile. Je, nataka kujua kuna uwiano gani wa ugawaji huu wa fedha katika Halmashauri zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu nije kwenye mpango wa utekelezaji, kutopelekwa kwa asilimia 20 ya ruzuku ya fidia ya vyanzo vya mapato iliyofutwa na asilimia

10 ya mfuko wa akina mama na vijana. Kama mtakumbuka, tulikaa tukajadili katika Bunge hili kuhusiana na mikopo ya akina mama ili tuweze kuwasaidia akina mama hasa akina mama wa kule vijijini, vijana kuweza kuwakopesha ili tusilete wimbi kubwa la watu ambao wanalundikana katika maeneo mbalimbali ya Mitaani na wengine kufanya uhalifu.

Vile vile nasikitika sana, fedha hizi asilimia 10 za akina mama hazipelekwi na wanaopewa ni wale akina mama wanaojulikana wana uwezo na nyingine zinaishia nyumba ndogo. Nataka kujua kwa Mheshimiwa Waziri, wakati fedha hizi zinatolewa zikielekezwa katika eneo husika: Je, kuna ufuatiliaji wa uhakika au ufuatiliaji mnamwachia Mkurugenzi na watu wake ndio wanatekeleza? Kama wanatekeleza, hebu fikeni katika Halmashauri zetu mwangalie ni utekelezaji uliokuwa halali? Mjue kuna akina mama wangapi waliopata fedha hizo na kuna vijana wangapi waliowezeshwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, inakatisha tamaa na inahuzunisha sana kuona akina mama wanakwenda kukopa katika vikundi vinavyotolewa sasa hivi vya mikopo vyenye riba kubwa, wananyang'anywa vitu vyao na wanaume wanakimbia nyumba, kwa ajili ya kunyang'anywa vitu vyao, kama vile nyumba na magari yao kwa fidia ya gharama iliyokuwa kubwa. Sasa lini Serikali itaweza kuwasaidia wananchi wake ili waweze kupata mikopo iliyokuwa nafuu na kuwaweka katika hali nzuri akina mama na vijana?

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la nne la udhaifu wa usimamiaji wa miradi. Ni kweli miradi mingi imekuwa haitekelezeki, na sababu kubwa ni ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi. Hawalipwi fedha zao zote nao hawamalizii kazi waliyopewa. Suala lingine ni mtu ambaye anapewa mradi huu, Mkandarasi anateuliwa tu, hana uzoefu wowote au yuko mbali na eneo la mradi unapotekelezeka. Imekuwa ni kero kubwa na mradi haukamiliki. Ule mradi unaachwa hivyo hivyo ulivyokuwa hewa.

Mimi naomba ungefika tu pale katika Halmashauri ya Wilaya Kondoa uone mradi uliotekelezeka wanaousema

wao, wao wanajua. Lakini ninavyoona, miradi hasa inayoonekana hata kwenye mradi wa maji; juzi Mkuu wa Wilaya amesoma risala mbele ya Naibu Waziri wa Maji; mwulizeni Naibu Waziri wa Maji. Kwa kweli imekuwa inasikitisha sana! Wananchi wanalipa kodi zao, wananchi wanategemea waongozwe, wananchi wanategemea wapate manufaa lakini leo hii wananchi hawapati manufaa yoyote katika nchi yao, imekuwa ni kero juu kwa juu tu. Baraka yake ni michango kwa kwenda mbele na michango hawaoni faida zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala lingine la kutowashirikisha wananchi katika miradi. Suala la ushirikishwaji katika miradi ni moja ya suala ambalo limeibuka kuleta mizozo na migogoro mikubwa katika ardhi. Mradi unapotokea katika eneo husika, inapaswa wananchi waitishwe na waelezwe kuhusu mradi ule, faida ya mradi ule, na mapato ya mradi kwamba mradi huu una faida gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni uzoefu mkubwa wa usimamiaji ndani ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwamba miradi ya Chama cha Mapinduzi inasimamia sera yake na utekelezaji, wananchi wafuate vile watakavyotaka wao; sivyo wananchi watakavyotaka. Wananchi wanakuwa sasa wanabeba mzigo mkubwa kuliko wanavyoona. Unafuu wa sehemu wameona mradi umekuja, wanaona kwamba ile fedha ya pale watapata mzunguko wa eneo lile nao wapate manufaa. Lakini wao tena inabidi wawe wanatoa fedha zao na kuweza kuchangia ndani ya miradi bila kusomewa hata mapato na matumizi. Imekuwa ni kero kubwa, na ni tatizo ambalo halikwepeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitaka kuangalia zaidi napata kigugumizi kutokana na mfumuko mpya wa bajeti. Ni lazima pesa za maendeleo zichelewe katika *quarter* ya mwanzo ya Serikali. Tulishaishauri Serikali ikope. Kwa nini Serikali inaleta kigugumizi juu ya suala hili, na ilisema Tanzania bado tunakopesheka? Sasa kama tunakopesheka, na tunaahidi na tunapanga miradi: Je, miradi hii ni kwa nini inakuwa hewa? Sasa kama kunakuwepo na miradi hewa,

kwa nini tunasema kwamba bado sisi tunakopesheka na tuna uwezo wa kuweza kupata fedha na kuendesha miradi yetu katika maeneo yetu? Hili suala limekuwa ni kero kubwa, hata wananchi kufikia hatua ya kukata tamaa, na pale wanapokuwa hawashirikishwi jambo la aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitakuwa na mengi katika mjadala huu zaidi, ila natoa tena suala langu la kuhusiana na kero niliyokuwa nayo. Naomba Mheshimiwa Waziri akija katika majumuisho yake, aniambie, mimi ni Mbunge wa Viti Maalum katika Mkoa huu wa Dodoma, nini nafasi yangu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa? Nilifika katika Halmashauri ya Kondoa toka nilipoteuliwa kuwa Mbunge. Nimeingia katika mamlaka yangu ya Mji, Lakini mimi nazuiliwa kwenye vikao vya mamlaka ile ya mji, naambiwa kwamba mimi sio Mjumbe halali, na nipo katika mamlaka hiyo hiyo ya mji. Niende wapi? Naambiwa anaruhusiwa Mbunge tu wa Jimbo, tena katika mpango wa fedha. Lakini mimi naingia katika Kamati ya Uchumi na Mazingira. Je, nini ukweli uliokuwepo hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nilikaa nje tofauti kwa muda mrefu katika kuingia kwenye vikao, naingia tu katika Vikao vya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, bila kiuingia kwenye Kamati. Kwenye Kamati, kila nilipoomba mpaka ilibidi niandike tu barua ya kuingia kwenye Kamati, nikaingia kwenye Kamati. Mbali ya kuingia kwenye Kamati, fedha nilizokuwa nimeahidiwa kwamba nitaweza kulipwa, mpaka Mheshimiwa Naibu Waziri niliweza kumweleza. Akaniambia atafutatilia atawaeleza, lakini bado kumekuwepo na ukimya. Kuna ukiritimba wa hali ya juu na ukiukwaji wa kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tumeambiwa hatuongelei suala la vyama wala la nini. Kwa nini ndani ya Halmashauri zetu za Wilaya, Mwenyekiti wa Halmashauri ambaye alichaguliwa na Wilaya mbili ndiye ambaye sasa anaongoza Wilaya moja, aliwahi kusimama ndani ya Kikao cha Halmashauri na kutamka kwamba hawa wapinzani waoneni hivyo hivyo, lakini sio watu wema. Hao ni maadui.

[MHE. MOZA A. SAIDY]
Je, sisi wa Vyama vya Upinzani tunakuwaje maadui? Sisi wa Vyama vya Upinzani tunaleta maendeleo katika nchi yetu. Kwa hiyo, huu ni ukiukwaji na utovu na wa nidhamu katika Halmashauri. Mwenyekiti anayazungumza, Mkurugenzi wa Halmashauri anayasikia, na wanakuwa lao moja. Ni kwa nini suala kama hii linatokea la kukiuka haki za binadamu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Moza Abedi. Kama nilivyosema mwanzo, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Christina Mughwai na Mheshimikwa Agripina Buyogera ajiandae.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nakushukuru. Nami kama Wabunge wenzangu, kwanza napongeza taarifa zote zilizowasilishwa hapa Bungeni, nasi tunaweza kujadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, naungana na baadhi ya Wabunge pamoja na Taarifa ya Kamati yetu kwamba kwa muda mfupi Kamati ya Bajeti imeweza kusimamia mambo kadhaa na muhimu ya Bajeti ya Serikali. Lakini kama wengine walivyosema, Kamati hii bado inahitaji kuimarishwa kwa kupatiwa ofisi na wataalam ili waweze kutafuta taarifa za kina zaidi ili Wabunge na Bunge kwa ujumla liweze kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Bajeti ya Bunge pamoja na Watumishi wa ofisi hiyo. Lakini hilo litawezekana iwapo Sheria ya Bajeti italetwa hapa Bungeni, na namshukuru Mheshimiwa Spika kwa kukubali tulete hoja ya kuanzisha Sheria ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili lilianzisha utaratibu mpya wa Bajeti ya Serikali. Lengo kubwa la kuanzisha mfumo mpya wa Bajeti ya Serikali ilikuwa ni

kuiwezesha Serikali kuleta fedha za maendeleo katika robo ya kwanza ya mwaka tofauti na miaka iliyopita, kwa maana kwamba Serikali katika robo ya kwanza ilikuwa haipeleki fedha za maendeleo kwa kusema kwamba bajeti yake huwa inachelewa kupitishwa na Bunge. Kwa hiyo, tukaja na utaratibu mpya kwa kushirikiana na Serikali kwamba sasa Bajeti ya Serikali itajadiliwa mwisho tarehe 30 Juni, na kuanzia tarehe 1 Julai ya mwaka mpya wa fedha, Serikali itaweza kupeleka fedha za maendeleo nchini kote ili maendeleo ya wananchi yaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kwamba hili halijaweza kutekelezeka nchini kote. Waheshimiwa Wabunge wamesimama, kila mmoja akilia kwamba fedha za maendeleo hazijapelekwa. Sasa na hii inaondoa mantiki, ni kwa nini basi tulibadilisha *budget site* ikiwa Serikali bado haijaweza kupeleka fedha za maendeleo? Kwa mfano, katika robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha, Serikali Kuu imepeleka asilimia 11 tu ya fedha za maendeleo. Robo nzima, asilimia 11 tu, na fedha za Mikoa ni asilimia 17 tu ndiyo zilizopelekwa katika robo ya kwanza. Sasa ikiwa robo nzima ya mwaka ni asilimia 11% tu zimepelekwa, ukifanya mara nne, maana yake robo za mwaka ziko nne; ni wazi kwamba kwa mwaka huu wa fedha, bajeti ya Serikali haitakifika kiwango cha utekelezaji kwa asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali haitaweza kutimiza bajeti yake kwa asilimia angalau 50, hivi hayo Matokeo Makubwa Sasa yatawezekana? Hiyo *Big Results Now* itawezekanaje kama hela za maendeleo ni asilimia 11? Ndiyo maana nakubaliana na hao watu wanaoiita hii ni *Better Resign Now. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri mpya ya Ikungi na Halmashauri mama yake, Halmashauri ya Singida; Halmashauri ya Ikungi ilitengewa bajeti ya mwaka ya maendeleo ya Shilingi bilioni 3.1, lakini mpaka sasa, maana sasa tuko mwishoni mwa robo ya pili, Halmashauri hii imepelekewa Shilingi bilioni 279 sawa na 9% tu ya maendeleo. Nusu mwaka imepita, Halmashauri mpya ya Ikungi

[MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI]
imepelekewa 9% tu ya fedha ya maendeleo. Matokeo Makubwa Sasa yatawezekana vipi katika Halmashauri hii ya Ikungi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Singida nayo inabidi niisemee maana ni Halmashauri mama ya Halmashauri mpya ya Ikungi. Yenyewe ilitengewa Shilingi bilioni 3.4 ya fedha za maendeleo. Lakini hadi sasa miezi sita, ni asilimia 8.9% ndiyo zimepelekwa. Hivi haya maendeleo yatapatikana kweli? Naiomba Wizara kwamba hizi Halmashauri mpya zilizoanzishwa, kuna mgogoro wa mgawanyo wa fedha za maendeleo zinavyoenda. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI naomba atusaidie. Hizo hela hata kama zinaenda kidogo, bado kuna sintofahamu ya mgawanyo. Halmashauri Mama ya Singida wanalalamikiwa na Halmashauri ya Ikungi kwamba hawawagawii fedha zao za maendeleo ipasavyo. Sasa katika muda huu wa mpito Mheshimiwa Waziri naomba ukatusaidie kuondoa sintofahamu hiyo ili Halmashauri ya Ikungi nayo iweze kusimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo ni moja ya Wizara ambazo ziliongezewa bajeti, na Bunge lililalamika mpaka bajeti yake ikaongezwa. Katika robo hii ya mwaka, Wizara hii ilitarajiwa kutumia Shilingi bilioni 81.04. Lakini katika robo hii ya kwanza, Wizara hii imepewa asilimia 29 tu ya bajeti yake. Ieleweke kwamba Wizara ya Kilimo unapochelewa kuipelekea hela, na sasa hivi ndiyo msimu, fedha hizi zitakapokuja kwenda mwisho wa mwaka wakati kiangazi kimeanza, fedha hizi zitakuwa hazina matumizi. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba inapopeleka fedha katika Wizara ambazo zinategemea misimu, basi ni vizuri watoe kipaumbele. Tunaambiwa kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa nchi hii, sasa kama uti wa mgongo unapelekewa hela asilimia 29 ya bajeti yake, hivi kweli nchi hii itasimama? Mbona huo uti wa mgongo haujaliwi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji nayo imepata sintofahamu hiyo hiyo ya kutokupelekewa bajeti yake kwa wakati. Tunajua kilio cha maji nchi nzima, lakini robo

ya kwanza yote ya mwaka huu ya bajeti ya maendeleo, Wizara hii ilikuwa haijapelekewa hata senti tano. Lakini fedha ya maendeleo imeanza kupelekwa robo ya pili ya mwaka. Sasa vipaumbele vya Serikali viko wapi?

Mimi naomba bajeti ya Serikali pamoja na udogo wake, pamoja na kwamba wameshindwa kukusanya fedha za kutosha za mapato ya ndani, na ulikuwa uzembe wa Serikali yenyewe, mmesema tusiitaje CCM, lakini hii ndiyo Serikali iliyowekwa na Chama cha Mapinduzi. Serikali inashindwa kukusanya mapato, hata hayo madogo wanayoyakusanya hayaendi kwenye maeneo ya vipaumbele. Wizara ya Maji; kilio cha maji nchi nzima, *quarter* ya kwanza inapita *(budget circle)*, hela zake zinaanza kwenda *quarter* ya pili. Hivyo ndivyo tulivyotaarifiwa katika Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie sasa suala la matumizi ya Serikali. Hili nalo limekuwa ni tatizo sugu. Mimi tangu nimeingia Bungeni, nasikia tatizo la matumizi makubwa ya Serikali. Lakini Serikali hii isiyosikia, matumizi yake yameendelea kuwa makubwa zaidi kuliko matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumelalamikia baadhi ya matumizi kama vile safari zisizo na tija, safari za viongozi zinakula hela za Serikali, safari hizi za Viongozi wanaambatana na misafara mirefu sana. Tunaambiwa kwamba bajeti ya safari za viongozi ilikwisha tangu mwezi wa Nane. Bajeti ya Serikali ya safari ilitumika ndani ya miezi miwili tu ya mwanzo ya mwaka wa fedha, na sasa wanasafiri kwa kutumia fungu la dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ndiyo kichekesho. Hivi bajeti ya mwaka mzima iishe ndani ya miezi miwili, na safari zinaendelea kwa kutumia fungu la dharura! Hivi dharura ikitokea, tutakimbilia wapi? Ni kweli wiki iliyopita au mwanzo wa wiki hii, Mheshimiwa Waziri alijibu kwamba safari nyingine zinakuwa hazijatarajiwa. Hili linawezekana, lakini zisitarajiwe kiasi kwamba safari zinakuwa nyingi na bajeti inaisha ndani

ya miezi miwili tu ya mwaka wa bajeti. Hivi tulibajeti sawasawa? Ni safari zisizo na tija, ni misafara mikubwa isiyo ya lazima. Kwa hiyo, naiomba Serikali na Wizara ya Fedha waokoe fedha ya wananchi, tena waache kutumia fungu la dharura. Dharura ikitokea hapa itatuhusu sisi wote, tutakimbilia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya magari. Katika bajeti hii Serikali ilisema kwamba watapunguza gharama za matumzi ya Serikali na hususan upande wa magari. Lakini tuko nusu ya mwaka, mimi sioni dalili yoyote ya kupunguza matumizi ya gharama ya magari. Kuna Waraka wa Serikali unaosema kwamba Watumishi waliokopeshwa magari, wasitumie magari ya Serikali. Lakini naomba Waziri atakapohitimisha, atuambie ni magari mangapi yamewekwa *pool* kwa sababu watumishi waliokuwa wanayatumia isivyo, sasa wanatumia magari yao.

Mhehimiwa Naibu Spika, unamkuta Mtumishi wa Umma amepewa gari, anaishi Dar es Salaam eneo la Bunju, Dereva wake anaishi Mbagala au Gongolamboto. Dereva atatoka Gongolamboto anasafiri kwenda Bunju kumchukua *boss* wake, atampeleka kazini, atamrudisha Bunju jioni; ataondoka na gari kwenda Mbagala au Gongolamboto. Hivi ni mafuta kiasi gani yanatumika? Wakati huo huo huyu ni kiongozi aliyepewa mkopo wa gari. Ni kweli hii Serikali ina nia ya kupunguza matumzi? Mbona mnawabebesha Watanzania mzigo ambao sasa hawawezi kuubeba? Tuone huruma! Oneni huruma! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la matumizi, naomba nimwambie Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, aangalie Marais wenzake; Rais Kagame wa Rwanda alichukua hatua gani mpaka Rwanda hawatumii magari ya anasa? Kenya, Rais wake alifanya nini mpaka sasa hivi Watumishi wa Umma hawatumii magari ya fahari? Nasema ni Rais mwenyewe ndiye mwenye jukumu hili, kwa sababu hutarajii Watendaji hawa wa Serikali ambao ndio wananufaika na ufujaji huu wa fedha za umma, eti ndiyo wachukue hatua ya kuacha kutumia magari ya umma ilihali

[MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI]
hawajui hata bei ya petroli barabani. Ndiyo maana nasema ni Mheshimiwa Rais mwenyewe anatakiwa achukue hatua kama ambavyo Marais wenzake wanafanya.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ooh, Mheshimiwa Christina, ni kengele ya pili. Nakushukuru sana. Mheshimiwa Agripina Buyogera.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika mchanganuo mzuri ulioletwa na Kamati zetu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini, Jimbo linaloongozwa na Kamanda mwanamke Agripina Buyogera, naomba tumshukuru sana Waziri Mkuu kwa kusitisha zoezi ambalo lilikuwa linaendeshwa la kufyeka mahindi na mazao mbalimbali ya wananchi wa Wilaya ya Kasulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo linauma sana kwa sababu kule kwetu sisi tunaamini, mtu anayefyeka mazao, anayemwaga chakula ni mchawi. Kwa hiyo, ninaamini na ninathubutu kusema mbele yako kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutokana na Wawakilishi wake waliopo Wilaya ya Kasulu, wametutendea kitu kibaya sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuchukua hatua za haraka, niliwasiliana na Mkuu wa Mkoa na yeye amesikitika kutokana na kitendo hiki kilichofanyika Kasulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naiomba sana Serikali, nimekuwa nikilalamika tangu nimeingia Bungeni kwa tatizo la wakulima wa Kagera Nkanda. Naomba hii iwe ni mara ya mwisho, Serikali ichukue hatua, tatizo hili lisijirudie tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni matatizo ambayo sisi Wabunge tunakuja kuishauri Serikali kwa nia njema, Serikali haichukui hatua. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ikae,

[MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA]
ifikirie, ni kwa nini Wabunge tuendelee kulalamika humu Bungeni kutokana na watendaji ambao tena wameteuliwa kwa heshima kubwa na Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri wa Tanzania. Inawezekana watu kama akina Dahni Makanga - Mkuu wa Wilaya ya Kasulu anataka kuwachonganisha, kutuondolea imani tuliyonayo kwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete na kutokana na kazi nzuri aliyoifanya kwa Mkoa wa Kigoma? Naomba Serikali iangalie upya, Dahni Makanga ni nani? Kwani ni lazima awe Kasulu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na kuchangia, ninaamini Serikali itakuwa imenisikia, na uzuri leo hii yupo Mheshimiwa Nahodha nakuheshimu sana na Serikali tunakuamini na wananchi. Naomba uishauri Serikali imalize tatizo la Kasulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia kwa Kamati zetu za Bunge. Kwanza, nawapongeza sana kwa kazi nzuri walizozifanya, hususan nianze na Kamati ya Mheshimiwa Andrew Chenge. Kamati ya Mheshimiwa Chenge ni ridhaa ya Bunge lako Tukufu ili tuanzishe Kamati ya Bunge ambayo itakuwa inatusaidia kufuatilia utendaji wa Serikali na kuweza kuchambua taarifa mbalimbali mapema iwezekanavyo kabla ya Bunge la Bajeti kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba ndugu zangu Mawaziri msikilize michango hii na muitafakari na muombe Mungu, wala msiwe na hasira. Ninaamini kwamba hali halisi iliyopo ndani ya nchi yetu, kutokana na udhaifu mkubwa wa Watendaji waliopo Wizarani waliopo kwenye Halmashauri mbalimbali, mlango pekee wa kuisaidia Serikali yetu ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Andrew Chenge tumia nafasi yako vizuri, Kamati yako Bunge tupo tayari kukuunga mkono. Kama kuna mahali ambapo panahitaji kuboreshwa kama hivyo mnatafuta Ofisi, mpatiwe Ofisi ili muwe na meno ya kusaidia Serikali. *(Makofi)*

[MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA]

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya kwa sababu gani? Mimi nimekuwa nikilalamika hapa, kule Jimboni kwangu kuna kitalu cha uwindaji. Kitalu ambacho tumeingia Mkataba na Wawekezaji, mwaka 2013 nilizungumza nikawaambia haiwezekani kitalu kimoja kiwe na wawekezaji watatu. Kitalu kimoja kinakuwa na wawekezaji watatu! Halmashauri Mwekezaji ambaye tumeingia naye Mkataba anatakiwa kutulipa kwa mwaka moja Shilingi milioni 440, lakini tangu ameingia mkataba na Halmashauri ya Kasulu na huyo mwekezaji katika kitalu kile, mpaka leo hii Halmashauri haijapata hata senti moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niongee na Mheshimiwa Andrew Chenge kupitia kwako, nitatoa *documents* hizi ili kuonyesha ugumu na ukubwa wa tatizo hili ambalo nimekuwa nikilizungumzia tangu ninaapishwa kuwa Mbunge, mchango wangu wa kwanza ilikuwa ni Kagera Nkanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *document* nitakukabidhi wewe ili umkabidhi Mheshimiwa Andrew Chenge kwa kuwa nina imani naye; na kwa kuwa najua Kamati yake ina uwezo wa kufuatilia masuala haya, ifuatiliwe Wizara ya Maliasili na Utalii; Shilingi milioni 880 tunazitaka. Naomba mtu aje achukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya kwa uchungu sana. Mkataba mmoja huu ambao tumepitisha Wizara imeweka mwekezaji. Kile kitalu kipo tangu mimi sijazaliwa. Mimi nimezaliwa naikuta Kagera Nkanda. Zamani watu walikuwa wanakula nyama za pori bila kuchunguzwa. Leo hii hakuna kula nyama ya pori kule Kagera Nkanda. Sasa wananchi wa kule wanahitaji wapate mafanikio kutokana na kitalu kile. Lakini leo utashangaa, Shule ya Msingi ya Mvinza haina hata choo wakati tuna kitalu, kwenye hifadhi ile kuna uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi uzuri mwaka 2005/2010 nilikuwa Diwani katika Halmashauri ya Wilaya Kasulu na nilikuwa Mjumbe kwenye Kamati ya Uchumi, Ujenzi na

Mazingira. Nilipata bahati ya kwenda kule kutembelea ile Hifadhi. Tukiwa hapa Serikalini, mkiwa Dar es Salaam, tukiwa hapa Bungeni ninapoongea Waheshimiwa Mawaziri, mnaweza mkafikiri kile ni kitalu kidogo sana. Kumbe ni kitalu kikubwa, kina wanyama wa kutosha, kina tembo wa kutosha, Wizara inatafuna fedha katika kitalu kile. Mkiona ugomvi uliopo, ni wawekezaji kuiwezesha Halmashauri, kumwezesha *DC* kula fedha, wananchi wakiwa wanapigwa, wakiwa wananyanyaswa bila maendeleo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali inisikilize. Tumezoea kuunda Tume. Hii siyo kazi ya Tume. Hii Kamati ya Chenge ikichukua *documents* hizi, ikafuatilia hatua kwa hatua mtagundua ni fedha nyingi zinatafunwa. Wizara imeweka mwekezaji pale, Halmashauri na mimi Mbunge mwenyewe wa eneo husika sijui Wizara yule mwekezaji iliyomweka pale inalipwa Shilingi ngapi? Wizara inachukua Shilingi ngapi? Ambapo kama tungejua inachukua Shilingi ngapi, tungejua katika Halmashauri yetu na sisi ni asilimia ngapi wanatupatia. Hizo fedha hatujui. Lakini hata hizo tunazozijua hizo Shilingi milioni 440 tulizosaini Mkataba na Halmashauri, mpaka leo hata senti moja haijapatikana. Ni vitu vya kushangaza! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo ukiongea hapa jamani, ni nani tumlaumu? Lazima Waziri awajibike. Hatuwezi kumlaumu mtu mwingine zaidi ya hawa walioshindwa kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kengele ya kwanza, naomba niendelee. Niongee kuhusu TAMISEMI juu ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Bunge tumekuwa tunapitisha fedha nyingi hapa ili ziende TAMISEMI kwa maana ya kwenda kwenye Halmashauri kuleta maendeleo, lakini fedha za maendeleo haziendi, mpaka leo Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu haijapata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizungumzie ukaguzi; huu ni mtandao wa wizi kabisa. Mimi nilikuwa Diwani; zile Kamati tulikuwa tunapitisha maombi kwenye bajeti yetu ya

kupewa pesa ya kukagua miradi. Kamati zote za Madiwani tulikuwa tunakwenda kukagua miradi. Kwa sababu kila Kamati ina kazi yake. Lakini leo ule utaratibu wameufuta, wametoa mamlaka kwa Kamati ya Mipango na Fedha ambayo ina Wajumbe wachache. Matokeo yake wakipanga kwenda kukagua miradi, Afisa Mipango, Mkurugenzi kwa sababu wanajua fedha zilipangwa kwenda kukagua miradi, wanawapeleka kwenye ile miradi mizuri ambayo imejengwa kwa ubora. Lakini ile miradi mibovu yote, inabaki huko. Kamati ya watu wachache haiwezi kwenda kukagua miradi kwenye Wilaya nzima kwenye Halmashauri, haiwezekani.

Kwa mfano, Jimbo langu lina Kata 19; sasa Kata 19 hii Kamati itaweza kufahamu miradi iliyopo kwenye vile vitongoji vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Hawa Ghasia hili mliangalie upya. Madiwani wote wana haki ya kuweza kujua miradi iliyoko kwenye Halmashauri yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee maana najua muda karibia unakwisha. Kuna upungufu mkubwa wa Watendaji katika Halmashauri na hasa katika zile Halmashauri mama ambazo wamepunguzwa Watendaji mbalimbali kwenda kuanzisha Halmashauri nyingine. Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, wamehamishwa watendaji waliokuwa pale kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, wamepelekwa kwenye Halmashauri mpya ya Buhigwe. Kazi haziwezi kwenda sawasawa. Ni wakati sasa tuweze kuangalia, tuajiri Watendaji wengine ili waje kuziba zile nafasi ili shughuli za maendeleo ziweze kwenda sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba nimalizie Mpango wa *Big Results Now.* Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, hili nalo naomba Serikali iliangalie vizuri tunapoenda na Matokeo Makubwa Sasa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Najua mtakuwa mmenielewa nataka kusema nini. Miradi ya zamani izingatiwe. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Agripina Buyogera, nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia haututoshi kwa Mbunge mwingine kuweza kuendelea. Tutaendelea na mjadala wetu jioni. Ataanza Mheshimiwa Sabreena Sungura, atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Kawawa na wengine mtafuata.

Baada ya maelezo hayo, naomba basi nisitishe Shughuli za Bunge hadi Saa 11.00 leo jioni.

(Saa 6.49 Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na mchangiaji wetu wa kwanza bila ya kupoteza muda ni Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Vita Kawawa atafuatia na Mheshimiwa Khatib Said Haji.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii adhimu na mimi kupata muda wa kuchangia katika Taarifa zetu tatu; ya Kamati ya Bajeti, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, na Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kupoteza muda naomba niishauri Serikali katika mambo makuu yasiyozidi matano. La kwanza ni suala zima la ukusanyaji wa mapato. Ukiangalia ripoti mbalimbali, mfano ripoti ya Kamati ya Serikali za Mitaa, lakini pia ripoti ya *CAG* kumekuwa kuna upotevu mkubwa wa mapato na upotevu huu mara nyingi umekuwa ukitokana na suala zima la Mikataba katika Halmashauri zetu.

[MHE. SABREENA H. SUNGURA]
Mheshimiwa Naibu Spika, naweza nikasema mpaka dakika hii kwamba Sheria ya Mikataba ambayo inatumika katika Serikali za Mitaa imekuwa ni sheria ambayo haizingatii maslahi ya Halmashauri mbalimbali nchini. Mfano mmojawapo ni kwamba katika sheria hizi Mkurugenzi hajapewa mamlaka katika mapato ambayo yanakusanywa na Mawakala katika Serikali zetu za Mitaa ya kumdhibiti Wakala wa Ukusanyaji wa Mapato pale ambapo anakusanya kiwango ambacho kimezidi ama kiwango kilichotarajiwa.

Sasa katika hali kama hii, kama Wakala anaamibwa akusanye labda takriban Shilingi bilioni mbili, lakini kama atapata Shilingi bilioni 2.5, basi Mkurugenzi sheria haimpi mamlaka ya kumtaka huyu Wakala kiwango hiki cha ziada kiweze kulipwa katika Halmashauri zetu. Katika mazingira kama haya, ni lazima mapato yaendelee kuwa machache katika Halmashauri mbalimbali na hivyo sasa malengo mbalimbali ya Serikali ambayo yanaibuliwa na wananchi yanashindwa kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine ni kuhusu sheria ndogo za Halmashauri na Manispaa kwa ujumla. Serikali ya Serikali za Mtaa yoyote ile haiwezi kukusanya mapato yake bila kuwa na sheria ndogo ambazo zitawezesha kukusanya mapato. Mimi nilikuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo, Kamati ambayo sasa hivi haipo kazini. Lakini hali inasikitisha! Unaweza kukuta Halmashauri moja ina sheria ndogo hata 20 mpaka 25. Lakini kuna Halmashauri zingine zina sheria ndogo za ukusanyaji wa mapato labda mbili, tatu mpaka nne.

Sasa hili suala ni lazima Mheshimiwa Waziri aweze kuangalia lile suala la kuwa umuhimu wa kuwa na *uniform by law* na hii itazisaidia Halmashauri mbalimbali kwa mfano, tunapotoa *uniform by laws* kwa pamoja kwamba ziwe *applied* katika Halmashauri zetu, tunajua kuna tofauti; kuna sehemu nyingine labda hawana uvuvi. Kwa hiyo, Sheria ndogo ya uvuvi haiwezi kuwa *applied* katika Halmashauri hizo. Lakini pia kuna maeneo mengine watu hawafugi na tunaposema tunaweka *uniform by law* itazisaidia sasa

[MHE. SABREENA H. SUNGURA]

Halmashauri zile, kwa sababu suala la mifugo inawezekana mtu leo hafugi, lakini baada ya miaka mitano au sita na kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, eneo hilo watu baadaye wakaweza kuwa wafugaji. Kwa hiyo, sasa itakapotokea, basi ile sheria ndogo itakuwa *applied* katika suala zima la uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi kuna uchimbaji wa mabwawa. Kuna Mikoa ambayo haina mito, bahari wala maziwa, lakini kuna mabwawa yanawekwa kunakuwa kuna samaki. Kwa hiyo, tunavyosema tuwe na *uniform by laws,* ina maana kwamba maeneo hayo itakapofikia hatua sasa ya kuanzisha mabwawa na kupata samaki kwa wingi, sheria hizi zitakuwa *applied*.

Kumekuwa kuna urasimu mkubwa sana wa ucheleweshaji wa ukamilishaji wa sheria ndogo hususan katika *process* ya kuanzia katika Manispaa zetu kwenda mpaka kwa Waziri Mkuu na kurudi, inachukua zaidi ya mwaka mpaka miaka miwili sheria nyingine haijakamilika. Sasa katika mazingira kama haya itakuwa ni vigumu sana kuweza ku-*raise* mapato katika Halmashauri zetu kama hatuna chanzo cha kufanya tukusanye mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo ningependa kuchangia ni udhaifu katika usimamiaji na utekelezaji wa Sheria za Manunuzi. Suala hili limepigiwa kelele karibu Kamati zote mbili ambazo ziliwasilisha ripoti zao; Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kuna udhaifu mkubwa sana katika manunuzi. Hata ripoti ya *CAG* imeonesha kwamba manunuzi mbalimbali ambayo yanaendelea katika nchi yetu, zaidi ya mara mbili mpaka mara tano ya bei ndiyo fedha za Umma zimekuwa zikitumika kufanya manunuzi. Katika mazingira kama haya, kwa kweli hatuwatendei haki Watanzania. Kuna haja ya kurudisha upya Sheria yetu ya Manunuzi Bungeni na kuangalia vipengele ambavyo vitalinda maslahi ya Umma.

[MHE. SABREENA H. SUNGURA]

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye ripoti ya Mwenyekiti wa Mashirika ya Umma inatuelezea kwamba ukaguzi uliofanywa na *PPRA* kwa mwaka 2011/2012 umebaini kwamba kiwango cha uzingativu katika matangazo ya utoaji wa mikataba kwa Wizara, Idara, Mawakala ilikuwa ni asilimia 65. Aidha, zifuatazo ni Wizara, Idara na Wakala zilizokuwa na kiwango kidogo cha uzingativu katika kutangaza utoaji wa mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokwenda kwenye suala la manunuzi, kama hatuzingatii mwanzo katika mchakato wa mikataba, kwa kweli Taifa lazima litakuwa linaingia kwenye hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kwamba kuna Idara ambazo ni nyeti, Idara za Serikali ambazo zinasimamia *legal matters* lakini na zenyewe zimekuwa hazifuati utaratibu katika kuzingatia mikataba ya manunuzi.

Kwenye ripoti hii, jedwali Na. 4 ya Hesabu za Serikali Kuu inaoneshwa kabisa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kiwango cha uzingativu wa mikataba ilikuwa ni sifuri. Hii ni aibu kwa Serikali. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndio Serikali inamtegemea katika masuala mazima ya ushauri, lakini sasa kama kwenye *level* ya mikataba ambayo taasisi yake inaingia, uzingativu wa mikataba kiwango kinakuwa ni sifuri, hii ni aibu kubwa sana kwa Serikali. Lakini pia kuna taasisi nyingine ambayo ni Tume ya Haki za Binadamu.

Hii Tume ni kubwa sana, ni Tume ambayo Watanzania ndio wangetegemea kwamba inalinda maslahi yao kwa ujumla. Lakini kama Tume hii na yenyewe kiwango cha utekelezaji katika kutangaza na utoaji wa mikataba kimekuwa ni 5% tu na 95% ni bure. Kwa kweli hali hii nayo ni mbaya. *The same applied* katika Wizara ya Katiba na Sheria, kiwango cha utekelezaji katika utangazaji na utoaji wa mikataba na wenyewe wana asilimia sifuri. Sasa Taasisi kubwa kama hizi na nyeti katika nchi zinashindwa kuzingatia, hali hii itapelekea Taifa kuingia katika hasara kubwa.

[MHE. SABREENA H. SUNGURA]

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kumekuwa kuna utunzaji mbovu wa kumbukumbu. Nimesikitishwa na Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu inapokwenda kukagua katika Mashirika ya Umma, inakuta majibu kama: "Ukaguzi umebaini kwamba hakuna kumbukumbu za manunuzi ya Umma." Yaani watu wanaamua tu kupotosha kwamba kumbukumbu haziwekwi ofisini, kwa hiyo, watu wanashindwa kujua ukweli ni nini kinaendelea. Lakini pia nyaraka za manunuzi zinakosekana. Hii ni hali ya hatari. Lakini pia kunakosekana orodha ya zabuni, nukuu za bei na mikataba, kusambaa kwa kumbukumbu za manunuzi katika Idara tofauti. Hii ni hali ambayo haileti afya katika uhai na maendeleo ya nchi yetu. Hapa kuna tatizo na kama nchi ni lazima iliangalie kwa umakini na Serikali iweze kulichukulia hatua ambazo zinastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limejitokeza kwenye ripoti mbalimbali za Hesabu za Serikali Kuu na Hesabu za Serikali za Mitaa ilikuwa ni mikopo kwa Watumishi wa Umma. Suala la mikopo limekuwa ni suala nyeti. Pale ambapo watumishi wa Halmashauri mbalimbali wanakopa mpaka kile kiwango kinachohitajika kinapitiliza, hili suala linakuwa ni gumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni zinawataka wasizidishe 2/3 ya mikopo yao, lakini hali halisi ilionekana kwa kutokana na ripoti hizi kwamba watu wanakopa mpaka inabakia *zero balance*. Athari yake ni nini? Mtu anapokopa kwa kiwango hicho, ule muda sasa wa kukaa ofisini, hususan kwa Walimu katika Halmashauri zetu; Mwalimu anapokopa kiwango mpaka kinabakia sifuri hatapata muda wa kukaa chini na aingie darasani awafundishe watoto ili waelewe. Muda mwingi atautumia kwenda kutafuta kipato cha ziada ili mambo yaweze kwenda na familia yake. Sasa lazima Waziri na timu yake wajipange tuhakikishe kwamba mikopo kama hii wanaishughulikia katika *level* mbalimbali za Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine linalosikitisha ni suala la mishahara hewa. Suala hili

limejitokeza kwenye ripoti za Kamati, lakini pia limejitokeza katika ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sampuli ndogo tu iliyofanyika katika Halmashauri mbalimbali, imeonekana kwamba zaidi ya Shilingi milioni 690 na kidogo, zimetumika kwa mishahara hewa. Lakini mbali na Serikali za Mitaa, hata Mashirika ya Umma, Bodi ya Mikopo imelipa katika Chuo Kikuu cha Mkwawa Shilingi milioni 66 kwa wanafunzi hewa.

Kwa hiyo, hili tatizo la hewa Serikalini limekuwa ni tatizo sugu na ni tatizo kubwa. Nami sitaki kuamini kwamba Serikali haina *coordination,* kwamba watu wa *statistics* hawana *coordination* na watu wa Utumishi, hawana *coordination* na watu wa Serikali za Mitaa. Tunavyosema kwamba mtu amefariki, ameachishwa kazi, amestaafu ama yeye mwenyewe ameamua kuacha kazi na bado mishahara inaendelea kulipwa, huu ni udhaifu mkubwa wa Serikali na tatizo hili limekuwa likipigiwa kelele takriban miaka yote, lakini Serikali imeonesha kabisa kushindwa kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala jingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusiana na Madiwani katika Halmashauri mbalimbali kushindwa kuwachukulia hatua watendaji wabovu. Naweza kusema ndiyo Serikali kweli ina udhaifu, lakini na Madiwani katika Manispaa zetu wana *play part* yao inavyotakiwa? Kwa sababu pale Mtendaji anapokuwa amedhulumu Taifa, ameiba na ushahidi upo, kwa nini wanashindwa kumuazimia. Ndiyo, Waziri kwa upande wake anatakiwa aunde Tume kuchunguza Wakuu wa Idara na awachukulie hatua. Kwa hiyo, yeye kwa upande wake anatakiwa a-*deal* na hapo. Lakini kwa upande wa Madiwani, ni lazima tukumbushane nchi nzima, pale ambapo Mtendaji yuko chini ya uwezo wao, wana mamlaka ya kumwazimia, basi wachukue hatua hizo ili tuweze kuondoa Watendaji wabovu na Manispaa zetu ziweze kuendelea katika hali ambayo itasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine katika suala la mapato, sisi tulitembelea na Kamati yetu katika Halmashauri

mbalimbali za Mkoa wa Dar es Salaam, kumekuwa kuna tatizo sugu. Hapo mwanzoni mapato yalikuwa yakikusanywa na watu wa Halmashauri wenyewe, lakini baadaye Serikali iliamua kukaimu suala hili kwa *TRA. TRA* imeshindwa kukusanya kile kilichotakiwa kukusanywa. Mapato ambayo yamekusanywa yamekuwa ni madogo sana hali ambayo imefanya mapato yale yatofautiane na hali halisi ilivyokuwa wakati ya Halmashauri hizo zilipohusika. Mkataba wao wa makusanyo hayo umekwisha toka tarehe 30 Juni, 2013. Sasa ni Mheshimiwa Waziri kuendelea kutoa matamko, nini Manispaa hizi zifanye kutokana na suala zima la ukusanyaji mapato? Kwa sababu muda wa kuangalia watu wa *TRA* umeshapita na hakuna jambo la maana ambalo lilifanyika ili kuhakikisha kwamba mapato haya yanaongezeka hivyo kunusuru uchumi wa nchi.

Suala lingine ni kuhusu fedha za vikundi vya wanawake na vijana. Serikali ya Tanzania imekuwa ikiendelea kuhangaika na suala zima la umaskini. Wanawake vijijini wana hali ngumu sana, vijana na wenyewe hali kadhalika. Kama Taifa linatoa ajira 400,000 lakini Watanzania tuko milioni 45, kwa hiyo, sasa nguvu ya Mtanzania sasa hivi inaangalia katika mitaji midogo midogo ambayo Serikali itawawezesha vijana na akinamama. Lakini inasikitisha kwamba waraka huu ambao ulitolewa na Wizara ya Maendeleo Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwenda kwa TAMISEMI kwamba Watendaji sasa watekeleze kwa kutenga asilimia 10 kwa ajili ya wanawake pamoja na vijana umekuwa haufanyiwi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Taifa hili tunalikomboa katika mazingira ya wapi, kama hata kile ambacho tunajipangia kama sisi kinashindwa kutekelezwa? Tukiangalia siyo kwamba fedha hakuna katika nchi hii, fedha ipo. Fedha mbalimbali zimekuwa zinapotea! Ripoti zinaonesha kwamba takriban Shilingi bilioni 4.46 ambazo zilitakiwa ziwasilishwe kwenye mapato ya Halmashauri zimekuwa hazitolewi kwa muda muafaka, lakini wakati mwingine hata ile mikataba, wakusanyaji wa mapato wamekuwa wakikiuka. Sasa kama fedha nyingi kiasi hiki zinapotea, hatuoni sababu ni kwa nini

[MHE. SABREENA H. SUNGURA]
sasa Serikali inashindwa kutimiza hii azma ya kumkomboa mwanamke na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kuna malalamiko ya rufaa za kodi. Inasikitisha kwamba Ofisi ya *Attorney General* imekuwa inashindwa kujibu barua za malalamiko ya rufaa za kodi kwa takriban mwaka mzima. Sasa katika mazingira kama haya, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ndiyo Ofisi ambayo inategemewa, lakini kama na yenyewe inafeli katika mambo madogo kama haya, kwa kweli suala hili limekuwa ni shida kweli kweli. Kama kwa uwajibikaji huu kama Ofisi ya *Attorney General...*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sabreena Sungura kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Khatib Said Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Kawawa.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami jioni hii kuwa mmoja wa wachangiaji katika taarifa hizi muhimu ambazo ziko mbele yetu. Napenda nichukue nafasi hii ya awali kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote tatu na Kamati zao kwa uwasilishaji mzuri ambao umetoa mwongozo wa namna gani sisi tunaweza kuchangia katika hoja hizi. Hii ni aina na mifano mizuri kwa Kamati zinavyotakiwa kufanya kazi, nazipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianze mchango wangu kwa kugusia hotuba ya Mwenyekiti wa *LAAC* katika ukurasa wa saba wa taarifa yake ambapo ameeleza matatizo sugu ya matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa. Katika ukurasa huo aya 2.15 imeelezwa kwamba:

“Kamati imebaini kuwa bado kuna ubadhirifu, ufisadi na utovu wa nidhamu wa hali ya juu ya matumizi ya fedha za umma na hii inatokana na Wizara husika, TAMISEMI kutosimamia kwa karibu au yenyewe kuhusika moja kwa moja

na ufisadi huo". Ningependa nisome hapo padogo tu ili kuweka msisitizo wa maneno yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyadhifa hizi wanazopewa wenzetu na kula kiapo hapa kwamba watazingatia, watatii na kuiheshimu Katiba katika kutekeleza majukumu yao ni kitu cha msingi kukizingatia katika utendaji wao. Imekuwa sasa kila inapofika wakati wa kusoma taarifa hizi, ni wakati mwingine tena wa sisi Waheshimiwa Wabunge kuendelea kulalamika na kunung'unika. Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanalalamika, Wabunge wa Upinzani wanalalamika, Katibu Mkuu wa CCM analalamika; sasa sote tumekuwa ni Taifa la kulalamika badala ya kuwa Taifa la kuchukua hatua. Kama wananchi waliotutuma wanatusikia sisi tunalalamika kwamba tunayoyasema yanakuwa hayazingatiwi, hii inatufikisha mahali tunatakiwa tujiangalie upya tuone ni nini tufanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Waziri mmoja wa zamani, miongoni mwa Mawaziri Wazungu waliokuwepo hapa, alizungumzia habari ya Taifa gonjwa. Naomba ninukuu maneno yake, alisema: "hadi sasa kuna watu wanaodhani kuwa Waziri au Mkurugenzi Mkuu wa Shirika lolote la Umma, maana yake ni kukaa chini na kula nchi. Hili ndilo linalotatiza maendeleo yetu. Kwa hakika huu ndiyo ugonjwa wa Taifa letu, kwamba wanaoteuliwa kushika nafasi hizi wanadhani ni wakati muafaka wa kukaa chini na kuila nchi. Haya siyo malengo". Waziri huyu aliipa jina la kuita "Taifa Gonjwa." Kwa hiyo, nina wasiwasi sasa kwamba Taifa letu limekuwa gonjwa kwa maneno hayo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khatib, ni nani huyo?

MHE. KHATIB SAID HAJI: Huyo anaitwa Dkt. Stan alitoa maneno haya wakati wa Maazimisho ya Miaka Arobaini mwaka 2001.

NAIBU SPIKA: Ni katika Baraza la Wakoloni au?

MHE. KHATIB SAID HAJI: La Nyerere. *(Makofi/Kicheko)*

[MHE. KHATIBU SAID HAJI]

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 11 wa Taarifa ya Kamati ya *LAAC* kuna Majedwali hapa. Haya Majedwali kuanzia namba nne, tano na sita, yote yananesha ni namna gani mwenendo wa mishahara hewa ilivyolipwa kwa Watumishi waliotoroka, waliostaafu na waliofariki.

Mheshimwa Naibu Spika, kazi yetu sisi ni kuishauri na kuisimamia Serikali. Tumeishauri Serikali mara nyingi kwamba, Watendaji wote wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao, wakiwemo hawa wanaoliibia Taifa hili, wachukuliwe hatua. Mimi naungana sana na Mheshimiwa Mkosamali na hotuba yake aliyosoma asubuhi, sisi hatuwezi kumchukia Waziri. Tunachochelea, kwa mfano, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, mama yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia, sisi hatukuchukii, lakini tunachukia ghasia kuja kutokea kwenye nchi kama mambo haya yataachiwa kuendelea. Ndiyo maana tunaposema haya mambo nia yetu ni kutaka kusaidiana katika kuweka mwongozo sahihi ambao utapelekea Taifa hili kwenye heri.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi imetolewa Taarifa hapa na *Transparency International* wakisema kwamba, Tanzania tumechupa kutoka nafasi ya nne mpaka ya tatu kwa rushwa na matumizi mabaya ya fedha za umma. Tumechupa kutoka ya nne tumekuja ya tatu katika nchi za Afrika Mashariki, yaani ni kupanda. Kuchupa ni kupanda. Kwa hiyo, nina wasiwasi kwamba, upandaji huu na tafiti hizi zinazoonesha kwamba, tunapanda kwenye rushwa badala ya kushuka, hii ni aibu nyingine kwa Serikali inayotawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa pamezungumziwa kuhusu mishahara hewa na fedha ambazo zimeshindwa kutolewa maelezo; kwa mfano, Halmashauri ya Jiji la Tanga pekee imeshindwa kutoa maelezo juu ya shilingi bilioni 2.016. Tunapozungumza kushindwa kutolewa maelezo kwa fedha maana yake hiyo tayari imeliwa. Sisi tutanena kwa sababu ada ya mja hunena, muungwana ni vitendo. Sisi tunanena, waungwana chukueni hatua ya kuonesha matendo haya ya uwajibikaji katika kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali.

[MHE. KHATIBU SAID HAJI]

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sasa ushauri uliotolewa na Wabunge wengi hapa ni vizuri ukazingatiwa kwamba, Mawaziri wote ambao wanaonekana wameongoza katika kufanya vizuri Wizara zao na kusababisha upotevu mkubwa wa fedha za umma, basi ni vizuri wakawajibika. Hili siyo jambo la ajabu; Hayati Baba wa Taifa katika Kitabu chake cha Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania, kuna moja ya aya alisema hivi: "Wala kubadili Waziri Mkuu siyo jambo la ajabu, Ndugu Rashid Mfaume Kawawa, alikuwa Waziri Mkuu wangu kwa muda mrefu, hakuwa amefanya kosa lolote, lakini nilitaka kumbadili na kuteua Waziri Mkuu mwingine. Nilimwita nikamwambia akanielewa, tukashauriana nani anafaa kuziba nafasi yake na tukakubaliana tukafanya hivyo. Najua watu wa aina ya Kawawa ni adimu sana duniani hawazaliwi kila siku." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu aliandika Kitabu hicho mwanzoni wa mwaka 1990, kueleza alivyokerwa kwa namna nchi inavyoendeshwa. Mheshimiwa huyu anasema Mwalimu hakufanya kosa sembuse ninyi mnaosimamia ulaji! Wakati mwingine tunapata tabu maana hapa tumetoa mawaidha mazuri na sisi tunataka tuwe wapole katika kuzungumza ili lugha zetu zisiwe za kuudhi.

Ninashindwa jinsi ya kuliweka vizuri neno mwizi nimwiteje ili asiwe mwizi na hili litatupa tabu kidogo, kwa sababu anayeiba ni mwizi. Wenyeviti wa Halmashauri wanapofanya haya nao ni wezi, wanapata baraka ya Kiongozi anayewasimamia kama hawezi kukemea hapa tusemeje? Tusaidieni ninyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Jiji la Tanga, kwa mfano, ilikadiria kukusanya mapato ya shilingi bilioni sita, lakini ilifanikiwa kukusanya mapato ya shilingi bilioni tatu. Kuna jambo hapa nataka kulieleza; kuna wakati ambapo Halmashauri zinapanga mambo kwa kutaka kujiongezea mapato yao, lakini Mheshimiwa Waziri, naomba

[MHE. KHATIBU SAID HAJI]

utakapokuja kujumuisha hapa na kutoa maelezo unisaidie; kuna jambo linazungumzwa na nimepata taarifa na Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Tanga kwamba, tayari kuna njama za kukichukua Kijiji cha Miaka 21 na kukimilikisha kwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliuliza hili hata Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC* ana taarifa nalo, alikuwepo Tanga. Kwamba, tayari Kijiji hiki ambacho ni mali ya Halmashauri ya Jiji la Tanga, kuna njama za makusudi za kutaka kukimilikisha kwa Chama cha Mapinduzi, badala ya kusikia tu kwamba, Halmashauri ya Jiji la Tanga ilikuwa na mpango wa kuingia ubia na *NSSF* kukiendeleza kijiji kile na kuanzisha Miradi mikubwa ambayo ingesaidia Halmashauri ya Jiji la Tanga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khatibu, hilo lipo ukurasa wa ngapi wa Ripoti?

MHE. KHATIBU SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, hilo halipo kwenye ukurasa, lakini ni Halmashauri katika kujitafutia vyanzo na Halmashauri inapojitafutia vyanzo ni pamoja na kutumia rasilimali zake. Siyo lazima kila kila kitu kiwemo kwenye mstari. *(Makofi)*

T A A R I F A

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Naibu Spika Taarifa.

NAIBU SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Tanga Mjini na Mbunge mwingine.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimwa Naibu Spika, Kijiji cha Miaka 21 kinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi siku nyingi. Hakuna mbinu za kukifanya Kijiji hicho kimilikiwe na Chama cha Mapinduzi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Chiligati nimekuona!

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuongeza taarifa iliyotolewa na Mbunge wa Tanga, kuthibitisha aliyoyasema kwamba, eneo hilo analolisema lilikwishamilikishwa kwa Chama cha Mapinduzi mwaka 2009, mimi nikiwa Waziri wa Ardhi.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: MheshimIwa Naibu Spika ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti wa *LAAC* si utapata nafasi mwishoni kabisa wewe si ndiyo mtoa hoja? Wewe ndiyo mtoa hoja, chukua *notes* tu wakati wako utaendelea.

Mheshimiwa Khatibu endelea!

MHE. KHATIBU SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninazikataa Taarifa zao na hata mimi nataka na wao wathibitishe kwangu kama Kijiji hicho asili yake ni cha Chama cha Mapinduzi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mbele yangu nina *cavity* waliyoweka Madiwani wa Tanga Mjini wa Halmashauri, ambayo imewekwa tarehe 13 Mei, 2011 kuzuia jaribio lolote la kukichukua Kijiji kile na kukifanya Kijiji cha Chama cha Mapinduzi. Ninayo na ninaomba taarifa hii ije Mezani kwako. Ina *sign* ya *registrar* mpya Moshi, asingekubali kupokea *cavity* kama mali hii ilikuwa na uhalali kwamba mali hii ni ya Chama cha Mapinduzi.

Meshimiwa Naibu Spika, hii hapa mchana kweupe nakuwekea. *Cavity* hii imewekwa baada ya Kaimu Katibu Mkuu wa TAMISEMI kupelekewa barua na ikasomwa kwa Kamati ya Fedha, Halmashauri ya Jiji la Tanga kutaka kukubali Kijiji hiki kuwa cha Chama cha Mapinduzi. Walipinga na ndiyo maana yote haya yakatokea. Kwenye Baraza la *Council* wakasomewa tena barua hiyo ya kutaka waridhie Kijiji hiki kitoke Halmashauri na kiwe cha Chama cha Mapinduzi.

[MHE. KHATIBU SAID HAJI]

Mheshimiwa Naibu Spika, mali za Tanzania ni za Watanzania wote. Chama cha Mapinduzi kimejichukilia Viwanja vya Michezo vyote ambavyo sasa wanashindwa kuvihudumia na bado wanaendelea kuchukua hata hizo zilizobakia mali za Halmashauri. Mradi ambao ulikuwa uingiwe na *NSSF* na Halmashauri ya Jiji la Tanga uwanufaishe Wananchi wote wa Tanga. Tayari Chama cha Mapinduzi wameingilia kati na kutaka kufanya Kijiji kile ni mali yao. Hivi ninavyokwambia, kama wanapinga baadhi ya Madiwani wa Jiji la Tanga wapo mbioni kwenda Mahakamani kupinga jaribio lolote la kutaka kuchukua Kijiji kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo yanatuletea tabu sana, kwa sababu kwa kweli ni aibu wakati mwingine. Mali ya Halmashauri ni mali ambayo tija yake inapotokea inawasaidia wahusika Wananchi wote. Mnapoichukua na kuifanya mali ya Chama cha Mapinduzi maana yake mnawabagua wengine wasihusike katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaliyotokea wakati wa kuanzisha Vyama Vingi, mali zote za Chama cha Mapinduzi ambazo walizichukua zilikuwa ni mali za Watanzania wote. Wafanyakazi wote wa Serikali wa nchi hii walikuwa kuna makato wanayokatwa kutokana na kuchangia Chama cha Mapinduzi. Wakati wa Vyama Vingi, urithi ule wote ulikuwa ni wa Chama cha Mapinduzi na haya bado tunayaacha yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Waziri husika jambo hili alitolee maelezo kwa kina, kwa sababu hili jambo lipo na hizo tarehe ambazo zilitolewa kwamba tayari ilikuwa ni mali ya Chama cha Mapinduzi, naomba ulithibitishe hilo hapa Bunge lako liridhike na wale Wananchi wa Tanga waridhike kwamba mali ile kweli haiwahusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, naungana na Wabunge wote waliosimama na kumtaka Waziri Mkuu, achukue hatua juu ya Watendaji wabovu ambao wameisababishia Serikali kupata hasara hasa Viongozi wa Halmashauri. Suala la Wakurugenzi wa

[MHE. KHATIBU SAID HAJI]
Halmashauri kuwa *Returning Officers* linatupa tabu sana. Wakati mwingine huyafanya haya kwa kulipa fadhila tu. Wanakuwa hawawezi hawa Wakubwa wetu kuwakemea wakubwa wetu kwa sababu nadhani kuna masilahi yanayopatikana katika kile kipindi cha shughuli kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba, nakubaliana na wenzangu wote. Wakati wa Wabunge kupiga kelele tukaishia kuondoka umeisha, lazima sasa tuchukue hatua. Mambo haya ya fedha za umma kuendelea kupotea na nchi yetu kupanda daraja na kuwa nchi kinara wa rushwa ni aibu kwa Taifa na ni aibu kwetu sote. Lazima tulikemee kwa nguvu zetu zote ili tuondokane na kadhia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vita Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Omari Juma.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nikushukuru kwa kupata fursa hii ya kutoa mchango wangu kwenye Kamati hizi tatu za Hesabu za Serikali. Kwanza kabisa, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati wote waliowasilisha Taarifa za Kamati zao. Pia naomba nianze kwa kuzipongeza Halmashauri zote zilizofanya vizuri, maana lazima tuwatie moyo Halmashauri zilizofanya kazi vizuri. Siyo Halmashauri zote zilizopata Hati Zisizoridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamelalamika kuhusu utendaji usioridhisha katika Halmashauri zetu kama Ripoti ya *CAG* ilivyoeleza; ni kweli. Naomba niungane nao kwa maana ya maoni waliyotoa kwa Serikali iweze kuyafanyia kazi. Naishauri pia Serikali nayo wafanyie kazi Maoni ya *CAG*. Tunaomba sana tufanyie kazi Maoni ya *CAG.* Ninaamini zile Halmashauri ambazo zilifanya vizuri zote zinatokana na Madiwani wake na Watendaji ambao ni waadilifu. Sisi Wabunge ni moja ya Madiwani.

[MHE. VITA R. KAWAWA]

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na *Memorandum* ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1997 iliyorekebishwa mwaka 2009, Halmashauri zinatakiwa kuandaa kutoa Taarifa ya Fedha ya kila mwezi, robo mwaka, katika Baraza la Madiwani na Ripoti ya Fedha ya Halmashauri hiyo ya Maendeleo kwa *RAS.* Sasa Wabunge ni miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Madiwani. Nasi tujiulize tumeisaidiaje Halmashauri yetu katika upungufu ulioonekana katika Ripoti ya *CAG?* Lazima na sisi tujiulize tusiinyoshee kidole tu Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu ukitazama Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC*, inaeleza katika Kiambatanisho A, B na C. Kiambatanisho A kinaeleza kuwa, kuna vitabu 2,900 vya makusanyo, mapato hayakuwasilishwa. Katika hivyo, kuna Halmashauri 36. Mimi naomba niipongeze Halmashauri yangu ya Namtumbo haimo katika *list* hii, lakini Karatu imo. Karatu inaongozwa na CHADEMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kiambatanisho B kuna maduhuli yaliyokusanywa na Mawakala bila kuwasilishwa ya shilingi bilioni nne. Kuna Halmashauri 56, Halmashauri yangu ya Namtumbo haimo, hapa Karatu haimo. Kuna masurufu yasiyorejeshwa ya shilingi bilioni moja na milioni mia tisa; Halmashauri ya Namtumbo haimo, Karatu imo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza au tunaponyooshea vidole kwamba Serikali iliyopo madarakani tuiondoe mwaka 2015 kwa sababu haikufanya vizuri, lazima tuangalie eneo na sisi tulilopewa dogo tu. Halmashauri hiyo ya Karatu, asilimia karibu 75 ya Madiwani wake inaongozwa na Chama cha CHADEMA, lakini upungufu huo upo. Vilevile ilifanya matumizi nje ya Bajeti ya shilingi milioni kumi, katika Ripoti ya *CAG* imeonesha. Je, Diwani ambaye ni Mbunge alifanyaje kuisaidia Halmashauri hiyo? *(Makofi)*

[MHE. VITA R. KAWAWA]

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa nyuma na *CAG* ya shilingi bilioni 78 kwa jumla Halmashauri zote, kwa maana ya Halmashauri 181 Namtumbo haimo, Karatu imo na milioni 64 ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vita Kawawa hivi Mwakilishi wa Karatu ni nani?

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, wanajijua.

NAIBU SPIKA: Basi endelea. *(Kicheko)*

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii ya shilingi milioni 64 Karatu imo, Namtumbo haimo. Kwa hiyo, wamefanya nini kuisaidia; kwa sababu tumeelezwa kabla taarifa hazijafika Serikali Kuu zinatakiwa zifike kwenye Kikao cha Kamati ya Uongozi na Fedha, Kikao cha Baraza la Madiwani, kwa *RAS* kwa maana pia *RCC.* Sisi wote ni Wajumbe wa Vikao hivyo; tumeisaidiaje Serikali? Halmashauri ya Namtumbo kwenye makosa kama haya sisi tuna Hati Inayoridhisha. Tuemeshawakataa Wakuu wa Idara watano katika kipindi cha miaka mitatu, leo tuna Hati Inayoridhisha. Kwa hiyo, lazima tutazame sisi tunaisaidiaje Serikali.

T A A R I F A

MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji Natse hufungui *pandora's box?* Haya Taarifa!

MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa ndugu yangu taarifa. Ameisema sana Halmashauri ya Karatu na ndiyo ya mfano hata Mheshimiwa Waziri Mkuu aliisifu. Ninataka nimpe taarifa kwamba, Serikali Tawala ni ya CCM; Mkurugenzi, DC, Watendaji, tunapambana nao hata kufikia hapo ashukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vita Kawawa; umeipokea taarifa hiyo?

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei, akajitahidi zaidi na Halmashauri yake kuyapunguza haya maovu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mujibu wa Kanuni ya 118, Nyongeza ya 8 ya Kanuni ya 9, Kamati ya Bajeti katika utekelezaji wa shughuli za Kamati katika kipindi hiki cha Februari hadi Desemba, moja ya kazi zake imetueleza kwamba, imeendelea kufanya utafiti na uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Kamati hii ni kwamba, wasitazame tu vyanzo vya mapato, watazame pia au kuishauri Serikali ikibidi wakati mwingine kwa dharura, ifanye maamuzi ya kuvilinda pia vyanzo hivyo vya mapato. Kamati ya Bajeti, naishauri kuna changamoto nyingi zingine zinatokana na wakati au kwa msimu. Vyanzo vingine vipo tayari lazima visimamiwe na vilindwe. Kwa hiyo, tunaomba kuishauri Kamati hii; kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Spika, kwa kuiunda hii Kamati. *(Makofi)*

Imekuwa *intervention tool* ya kuisaidia Bajeti ya Serikali na kulisaidia Bunge. Kwa hiyo, naomba sana iviangalie vyanzo vya uzalishaji vinavyokwenda kutoa mapato kwa Serikali. Vipo vingi, lakini pia kuna vyanzo vipya vya wataalam, vijana wataalam, ambao tunao, Serikali inawasomesha, vyuo vingine vinawaandaa ili wakawe wajasiriamali, lakini hawana uwezo wa kuendesha shughuli zao. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali au Kamati hii ya Bajeti, isaidie kuona jinsi gani Serikali itaangalia uwezo wa kuwezesha makundi haya ya vijana.

Tumeona mfano, vijana waliokuwa na ujuzi wa teknolojia ya sasa ambao wamepunguza gharama kubwa ya mzigo kwa Serikali kukusanya mapato, pia Wananchi kusumbuka kwenda kwenye vituo vya kukusanya mapato.

[MHE. VITA R. KAWAWA]

Maxi Malipo, teknolojia yao imetusaidia ndani, lakini pia teknolojia yao wanaiuza nje ya nchi. Kwa hiyo, lazima Serikali iwe na uwezo wa kuwaangalia hawa, wapo wa aina nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wahandisi pia lazima tuwaangalie. Wenzetu wa *South East Asia* kule wanachokifanya; mfano Wahandisi Vijana, wanapomaliza Vyuo Vikuu wanawasaidia kuanzisha makampuni na wengine wanawa-*attach* kwenye makampuni makubwa. Hapo hapo makampuni hayo yanaomba kazi nje ya nchi yao wanawapeleka vijana wao. Kuna mfano halisia hapa, Wachina nao wanafanya hivyo. Hapa hapa tuna mradi mkubwa wa dola milioni 300, tulikwenda kuutembelea unatekelezwa na Wachina kwa mkopo wa Benki ya Uchina, lakini unatekelezwa kwetu kwa faida yetu. Mainjinia wale wote ni vijana kabisa *fresh from college,* wapo pale na wote wanatoka China. Sisi mafundi mchundo tu ndiyo wapo kwenye ule Mradi. Maana yake ni nini? Fedha nyingi zinarudi pia China.

Kwa hiyo, naiomba Serikali iwatazame sana vijana na kuwawezesha kuhakikisha wahandisi vijana pia wanajikusanya, wanawawezesha kwa maana ya kimtaji na wanakwenda kufanya kazi za maendeleo katika Halmashauri zetu.

Leo Halmashauri zetu tunapeleka fedha chungu nzima za Miradi mikubwa ya fedha nyingi. Kinachofanyika pale kingine ni kwamba, Wakuu wa Idara au baadhi ya Wakurugenzi wasiokuwa waadilifu, wanakuwa na kampuni wanajificha nyuma ya mgongo, wanazieleza taratibu za manunuzi, wanatoa siri za *rate* ya pale, wanapata kazi, halafu hawana wataalam. Vijana wetu waliomaliza Vyuo Vikuu Wahandisi wanabaki wanatembea mtaani hawana kazi. Kwa hiyo, tuwasaidie, Kamati naomba sana kuishauri hiyo, ione pia uwezo wa kuishauri Serikali. Tuangalie jinsi ya kuwakusanya hawa vijana, wakiwa pamoja wata-*create employment*. Wao watakuwa *consultants*, lakini pia watakuwa na mafundi mchundo na kadhalika na

kadhalika. Kwa hiyo, naomba sana Serikali izingatie ushauri huu.

Vilevile vyanzo vingine vya mapato vya kilimo lazima Serikali iviangalie na ivilinde. Ninapozungumzia suala la tumbaku, nazungumzia uchumi wa mapato ya Dola za Kimarekani kwa mwaka dola milioni 300. Dola milioni hizo zinakuja kwa mauzo ya nje, dola milioni 250 ni kwa ajili ya kuwalipa wakulima tu, lakini zaidi ya bilioni 120 ni *revenue* ya Serikali. Sasa leo tuna matatizo katika tumbaku, Benki mpaka leo hawajatoa mkopo wakulima wapate pembejeo. Niliuliza swali hapa juzi kati, nimetoa taarifa yangu vizuri kwa Waziri wa Kilimo na Waziri Mkuu, naamini wanaifanyia kazi. Nawaombeni sana Serikali, walifanyie kazi suala hili kwa dharura, kwa sababu jambo hili ni la msimu.

Suala hili ni la msimu, mvua zimeshaanza na wakulima hawa wasipopata pembejeo maana yake ni kwamba, Serikali itakosa zaidi ya shilingi bilioni 120 kama *revenue.* Wakulima watakosa zaidi ya dola milioni 250 wanazolipwa kila mwaka kutokana na mauzo hayo na Serikali pia watakosa mauzo ya nje ya dola zaidi ya milioni 300.

Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ifanye jambo hili kwa dharura kuhakikisha wakulima hawa wanapata pembejeo waende shambani. Kama kuna makosa madogo madogo, basi hayo yataangaliwa baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hayo, naomba kuwasilisha mchango wangu. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Riziki Omar Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida!

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi hii niongee machache kuhusiana na Ripoti ambazo zimewasilishwa.

[MHE. RIZIKI OMAR JUMA]

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uwezo na afya iliyo njema, kuweza kusimama hapa muda huu nikachangia machache. Nawapongeza ndugu zangu Mawaziri kwamba, sasa hivi nawaona wamo ndani, ni jambo la kufurahisha na kujipongeza kwamba wamo ndani wanasikia tunayoyazungumza. Zaidi, Mheshimiwa Profesa Mhongo, sijamwona siku nyingi leo yupo nimefurahi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kujikita zaidi kwenye Ripoti ya *CAG.* Nianze na kifungu ambacho kinasema Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuna malipo ya ziada ya ununuzi wa gari Namba *4WD Toyota Land Cruiser* kwa shilingi 56,520,305. Waswahili wanasema, ukila na kipofu usimguse mkono. Jamani hapa kipofu ameguswa mkono. Milioni zote hizi za ziada; haya manunuzi gani ambayo yamefanyika?

Mheshimiwa Hawa Ghasia, ndugu yangu, usipoangalia vizuri watakuweka pabaya. Tunazungumzia kila siku Watumishi ambao siyo waadilifu, hii ni kutokana na kutokuwa na uadilifu wa Watumishi ndiyo mambo kama haya yanajitokeza katika Halmashauri zetu, katika Ofisi zetu na katika Wizara zote. Mambo haya yanajitokeza kutokana na kutokuwa na uadilifu kwa Watumishi wetu na bado Waheshimiwa Wabunge humu ndani tutaendelea kuzungumza.

Tutasema tukimaliza muda tunakunja virago tunarudi majumbani mwetu, tunakwenda Majimboni tunafanya shughuli zetu, tukirudi tunakuja kuzungumzia yale yale. Bila Serikali kuchukua hatua madhubuti kuhusiana na Watumishi hawa wasio waadilifu, basi tutakuwa kila siku tunaimba wimbo ule ule tu mwisho utakuwa ni Wimbo wa Taifa. Ni jambo la kusikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu, ukurasa wa 132, Fungu 49, kuna Watumishi wanne ambao wamestaafu tangu Februari, 2012 waliendelea kulipwa mishahara mpaka fedha hizo zimefikia shilingi 5,811,251. Hivi

[MHE. RIZIKI OMAR JUMA]

jamani hatuoni, ni vipofu, tunafanya makusudi au inakuwaje? Huu ni wizi. Huu ni ufisadi. Jambo ambalo linakemewa kila siku, lakini *still* linaendelea kufanyika siku hadi siku. Naiomba sana Serikali mambo haya iyachukulie hatua za haraka ili kuondoa ulaji huu wa fedha hovyo hovyo huku Wananchi wakiendelea kusota na umaskini.

Katika mashule, vifaa vya kufundishia hakuna, walimu hawana mishahara ya kutosha na hawana makazi mazuri wanaishi katika mazingira magumu, madaftari, hospitalini hamna vifaa vya tiba vya kutosha, lakini fedha zinaliwa na wajanja wachache. Haya ni mambo ya kusikitisha, ni mambo yanayojitokeza katika Halmashauri zetu zote. Naomba sana Serikali ichukue hatua za haraka. Tusifumbie mambo haya.

Leo Ripoti ya *CAG* inasema kwamba, kuna baadhi ya nyaraka ambazo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, ikiwemo taarifa za benki za kipindi cha Januari, 2011 hadi Novemba, 2011, yenye Hundi Namba 812792 yenye thamani ya shilingi 19,800,000. Kwa nini? Ni kwa sababu ipi? Tumhoji nani? Nani atupe jibu sahihi kuhusiana na mambo kama hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mambo ambayo yanasikitisha. Ni mambo ambayo tunayaona kwa sababu hayafanywi kwa siri yanaonekana. Mkaguzi anakwenda ameona hali hii anairipoti kwetu, anaripoti kwa Serikali, hakuna hatua zinazochukuliwa. Je, hawa wanachukuliwa hatua zipi? Hii ni Halmashauri ya Morogoro ambayo naizungumzia kwa kina. Nimejikita zaidi kwa sababu afya yangu ilikuwa hainiruhusu, nikafungua fungua nikaperuzi nikaikuta Halmashauri ya Morogoro, nikagundua vipengele kadhaa ambavyo vimeripotiwa mle kuwa na kasoro fulani fulani, ndiyo hizi ambazo nazizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitabu 40 vya kukusanya mapato havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Tunaelekea wapi? Ukaguzi huu utafanywa saa ngapi? Utafanywa lini? Mahesabu haya yatapatikanaje kama

vitabu vinafichwa na kwa nini vifichwe? Lazima kuna ushirikiano baina ya Halmashauri na Serikali Kuu. Hawezi mtu kuiba bila kuwa na ushirikiano na mtu mwingine. Naomba sana Serikali iwe makini ili Wananchi wasiendelee kutuelewa vibaya na wasiendelee kudhalilika. Hizi ni fedha za Wananchi, tunahitaji tuwasaidie ili maisha yao yaboreke. Sasa ikiwa fedha tunakula sisi wajanja mmoja mmoja Wananchi tunawaweka wapi Mheshimiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri hiyo hiyo ya Morogoro kumekosekana hati za malipo zenye jumla ya shilingi 1,178,916,658; ni fedha nyingi sana. Shuleni hakuna madawati, hospitalini hakuna madawa, fedha zote hizi zinakwenda wapi? Kuna shule hazina maabara na zile ambazo zina maabara ni vyumba tu hakuna vifaa vya sayansi ambavyo vinaweza kuwasaidia vijana wetu na tukapata vijana wazuri watakaotoka na taaluma ya sayansi. Jambo ambalo Wabunge wamekuwa wakilipigia kelele muda mrefu humu ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ndugu zangu, tunaelekea kubaya sana na Serikali yetu haiwezi kuwa na sifa kila siku tutatajwa kwa rushwa. Tutakuwa wa nne, tutakuwa wa tatu, mwakani tutakuwa wa pili, keshokutwa tutakuwa wa tatu; ni jambo la aibu. Mwisho, tutashika nafasi ya kwanza tunaongoza kwa rushwa. Hili ni jambo la aibu, la kusikitisha na linatisha. Ubaya unaposemwa unatakiwa urekebishwe, lakini ubaya ukisemwa sisi tunaendelea kuchomelea mifukoni, inakuwaje? Tunashindilia mifuko yetu tu, Wananchi wanaendelea kudhalilika! Ni kitu cha ajabu, Watanzania tunawafikisha pabaya, tunawaweka pabaya, wanatuangalia sisi. Inaangaliwa Serikali, lakini na sisi Wabunge wanatuangalia, kwa sababu sisi ndiyo wasemaji wao wakubwa. Wametuleta humu ndani ili tuwawakilishe tuwasemee shida zao. Leo kila siku tunasema inakuwa ni wimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi malipo yanafanywa na benki bila hundi? Halmashauri ya Morogoro hiyo, malipo yanafanywa na benki bila hundi, shilingi 156,460,254; ni kitu

[MHE. RIZIKI OMAR JUMA]
cha ajabu na aibu. Fedha hizi ziko wapi? Zinakwenda wapi? Waheshimiwa wananijibu huko lakini sipendi niwasikilize, majibu nitayapata hapa kutokana na waliowasilisha Ripoti.

Ripoti ya *CAG* haya anayotupa yanatakiwa tuyafanyie kazi. Nimesema mwanzoni kwamba, tunaimba humu halafu tunatoka tunarudi mwakani yanayasema haya haya. Hii si mara ya kwanza, kila siku mambo haya yanazidi, upotevu wa fedha unazidi na ulaji wa pesa hovyo hovyo unaongezeka. Matatizo nchini yanaongezeka, hatuna *solution* ya matatizo yetu, kwa sababu ya kazi hii tunayofanya ya ufisadi na wizi wa fedha za mali ya umma. Wizi wa fedha za Serikali, wizi wa fedha za Wananchi, jasho la Wananchi tunawanyonya. Sisi tunaendelea kutanua, Wananchi wanaendelea kudhalilika. Ugonjwa, maradhi na umaskini, utaendelea kutusonga tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mishahara ambayo imelipwa zaidi ya stahili ya Watumishi husika, shilingi 25,146,000,. Mishahara isiyolipwa kutorejeshwa Hazina; kama fedha hizi hazikurejeshwa Hazina ziko wapi? Zimepelekwa wapi? Nani katafuna? Serikali haitaki kuhoji? Serikali Kuu haitaki kuona kama Watumishi hawa wana matatizo?

Lazima wachukuliwe hatua za haraka na hatua siyo kubadilishwa wakapelekwa kwingine wakaibe tena. Hapana, tuchukue hatua za haraka zinazostahili kutokana na matendo yao ya kula fedha za Serikali, fedha za umma, Wananchi wakaendelea kuteseka. Ukijumlisha fedha hizi zote nilizozitaja na zile ambazo sikuzitaja kwenye Halmashauri moja na Halmashauri nyingine ni nyingi sana ambazo zingeweza kutatua tatizo la elimu, zingeweza kutatua tatizo la afya na zingeweza kutatua tatizo la maji japo kwa asilimia fulani. Hatuwezi kumaliza yote kwa pamoja, lakini asilimia fulani ya tatizo hili ingeweza kuondoka kutokana na fedha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo kubwa, lazima Mheshimiwa Waziri Mkuu, achukue hatua ipasavyo. Mimi

[MHE. RIZIKI OMAR JUMA]

nakataa kusema Mawaziri, Mawaziri, *no,* wao wasimamie lakini Makatibu Wakuu ndiyo Watendaji Wakuu jamani, tuwaangalie sana. Katibu Mkuu ni mtu wa mwanzo kumwangalia, yeye ndiye Mtendaji Mkuu, yeye ndiye Afisa Masuuli. Naomba sana tuziangalie kwa kina Halmashauri zetu, tuangalie pesa zinavyotafunwa na wajanja wachache ili tuweze kupata suluhu ya matatizo yetu. Vinginevyo, tutakuja kuimba hapa kila siku hatuna madaftari, hatuna vitabu, hatuna *label,* hatuna hiki na kile, hatuna madaftari, tutaendelea kusota hivi hivi. Madaktari wazuri wanatukimbia, wachache wanatia fedha mfukoni, hawana kazi wanaoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Riziki Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza!

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kunipatia afya njema na mimi kuchangia katika hoja iliyoko Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri miaka ya nyuma nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya *LAAC.* Haya matatizo yaliachwa, hivyo asingiziwe Waziri aliyeko sasa hivi kutaka kutupiwa mzigo, ni mzigo uliaochwa kwa muda mrefu bila kufanyiwa kazi. Huyu aliyekuwepo sasa apambane na matatizo ambayo yako sasa hivi na kwenda mbele. Msimhukumu kwa kitu cha nyuma, kitu cha nyuma kinabidi kitekelezwe na wale waliofanya makosa. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, ninakuja na hoja yangu ambayo inanisikitisha na kuniletea huzuni kubwa ndani ya nafsi yangu. Leo hii Wizara tatu; Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Ardhi na Wizara ya TAMISEMI, zitaiweka Mkoa wa Lindi katika rehani. Mkoa wa Lindi kuna speculators wamegundua kama maeneo yale yana gesi. Hivyo, Wananchi walio kandokando ya bahari sasa hivi

wanatolewa kwa kunyanyaswa. Nimeipeleka hoja yangu kwa Naibu Waziri wa Ardhi, sijaona utekelezaji wake na sasa hivi Waziri wa Nishati na Madini ninamwona hapa; naomba afuatilie kwa makini haya nitakayoyazungumza. Waziri wa TAMISEMI, uko hapa, uyasikilize haya ninayoyazungumza, tukitoka hapa twende Lindi mkasikilize hoja zangu hizi ili msingoje moto baadaye muanze kuuzima. Tunataka tuzime moto sasa hivi, hali ni tete.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Mitwelo ni Kijiji cha asili ya Wananchi wa pale, kipo ndani ya Manispaa ya Lindi. Mradi wa *UTT* umekwenda Mitwelo kutaka kuchukua eneo lile, lakini wanataka kuchukua eneo lile wakati Wizara ya Nishati na Madini wanazungumza, *Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC), Licensing Situation, June, 2013,* eneo hilo wamempatia *Ndovu Resource.* Naomba atupe mwelekeo baadaye ili migogoro ya Wizara hizi mbili na maeneo yale, watu watolewe, halafu baadaye watu wale walioko kule waonekane hawana haki, wajanja wanaokwenda kupimiwa viwanja sasa hivi ndiyo watachukua lile eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaihurumia Serikali yangu, kwa kuwa eneo lile wanatolewa Wananchi eka moja kwa laki nne; ni Manispaa gani katika Tanzania hii imemtoa Mwananchi kwa eka moja laki nne? Huu ni ukandamizaji, huu ni uonevu na si uonevu ni dhambi. Tufike mahali utajiri wetu, ubinafsi wetu, tusiwakandamize Wananchi wenye haki zao za msingi. Tunasema maisha bora kwa kila Mtanzania, hapa hakuna maisha bora, itakuwa ni maisha mabaya kwa Wananchi wa Mitwelo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mitwelo ni eneo ambalo lipo ndani ya Manispaa, sasa hivi wanaenda kupima viwanja kwa bunduki kwa nini? Wananchi wale wenye amani zao kwa nini uchukue bunduki? Wanakandamizwa, eneo la mtu ana eka zake ishirini anapewa shilingi milioni moja na laki moja na haoneshwi anapelekwa wapi, atakwenda kuishi wapi akitolewa pale Mitwelo.

[MHE. RIZIKI S. LULIDA]

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekutana na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ole-Madeye nikamwambia, nikamwandikia na barua. Nimepeleka barua Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini sijaona utekelezaji wake na watu wanaendelea kutumia mabavu na nguvu zao kuhakikisha Wananchi wale wanatolewa kwa nguvu. Ninaomba Serikali isimamishe lile zoezi kwanza haki itendeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, tufike mahali tujiulize Wananchi wa Mkoa wa Lindi walikaa kwa muda mrefu katika mazingira magumu; hawana barabara, hawana elimu, maskini, lakini maeneo yao ya Bahari waliyatunza. Sasa haiwezekani maeneo yao ya Bahari waliyoyatunza miaka mingi wanaambiwa tunataka kuweka mwekezaji hapa tokeni kwa laki nne. Haikubali! Tafuteni ridhaa ya Wananchi wale muwawekee mazingira yao na ipite huruma ndani yake hawafanyi makusudi wanaonewa na hawana mahali pa kukimbilia.

Mimi nimeona nije hapa nijitoe kafara, mimi ni mbuzi wa kafara, kwa wale Wananchi wanaokandamizika nikitoka hapa mkiniambia lini twende Lindi nataka Waziri wa Nishati na Madini, Waziri wa Ardhi, Waziri wa TAMISEMI twende Lindi kuna migogoro mizito, hawawezi watume Kamati zao ziende kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja Wananchi wa Geza, palikuwa na shamba la katani liliachwa toka mwaka 1958, Wananchi wamejenga majumba yao, wamejenga mashule. Sasa hivi wamegundua eneo la Likongo linataka kuingia katika uwekezaji wa gesi, wanaambiwa wale Wananchi wanatolewa kwa bei ya kutupa; watakwenda wapi? Kwa nini mliwaachia mpaka wamejenga nyumba, wamejenga mashule, wameweka mikorosho yao, leo wanaambiwa hili eneo walivamia! Hatuwezi kwenda katika mazingira hayo. Umaskini wao utazidi kuonekana kwa hali inayokwenda sasa hivi.

Naomba kwa heshima na taadhima, sikutakiwa kuchangia sana ila *area* ambayo naiona sasa hivi kwangu

[MHE. RIZIKI S. LULIDA]
ni tatizo na kwao ni tatizo na Serikali ni tatizo. Kwa nini nazungumza hiyo? Kama kweli Wizara ya Nishati na Madini imempata mwekezaji huyu mnyonge ametolewa kwa laki nne; huyo anayeichukua ataiuzia Serikali kwa *billions;* je, Serikali ipo tayari kubeba mzigo mzito kama huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, imefika mahali tujiulize tunakwenda wapi, watu wanataka utajiri wa kutisha, wanataka kuingia kuwatia watu umaskini ili wao waendelee kuwa matajiri. *Gap* la matajiri ni kubwa sana na *gap* la maskini limekuwa la kutisha. Haiwezekani, sina mengi ya kuzungumza, nawaomba Mawaziri hawa wanisikilize na hii kauli itolewe tamko ndani ya Bunge watakuwa tayari kwenda kuangalia tatizo ili angalau liweze kutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ahsanteni sana, nawashukuruni. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Riziki Lulida!

T A A R I F A

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, bahati mbaya, inatakiwa taarifa itolewe wakati mtu anaongea.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kabla hajakaa, alikuwa hajamaliza sentensi ya mwisho na mimi nimewahi kabla hajakaa.

NAIBU SPIKA: Maana yake itabidi nimsimamishe tena ajibu taarifa hiyo kama anaipokea, itakuwa kidogo kiutaratibu imetuletea tabu. Tuvumilie kidogo tukipata nafasi hapo mbele tutafanya hivyo. Samahani sana sikukuona, ilipaswa iwe wakati anaongea.

[NAIBU SPIKA]

Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja zilizopo mbele yetu za Taarifa za Kamati za *LAAC,* Kamati za Hesabu za Serikali pamoja na Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaongelea machache kwa sababu mambo mengi yameshaongelewa na Wabunge, lakini nitarudia mengine kwa kuweka msisitizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na utaratibu wa kulindana pale Watendaji wa Serikali wanapofanya ndivyo sivyo katika utekelezaji wa shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika Halmashauri zetu, Halmashauri zinaundwa na watu wawili; kwanza, ni Watendaji ambayo ni *Executive;* pili, wapo Wanasiasa ambao ni Madiwani pamoja na Wabunge sisi kwa wadhifa wetu ni Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu unakuja pale ambapo sisi Wanasiasa tunapowalaumu Watendaji bila kuona kama sisi kweli tunatimiza wajibu wetu. Ninaomba mnisamehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kukuta Mtendaji amefanya mambo machafu, Kamati zinaenda au sisi Madiwani tunakuwa kule lakini tunafika hatua ya kuomba rushwa ili tuweze kuzima matendo mabaya ya Watendaji. Ninasema hivyo kwa sababu kesi zingine zipo Mahakamani na ninasema kesi hizi zingekuwa CHADEMA ndiyo basi, tungekuwa tunasemwa katika Hadithi za Alfu Lela Ulela, lakini kitendo hata kama kesi ingekuwa moja au ingekuwa nusu, lakini bado ni aibu kwa Bunge.

[MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA]

Mimi nawaomba, Wanasiasa na sisi tuone kama kweli tuko safi katika haya, kama kweli tunakwenda kusimamia Halmashauri ipasavyo na kama kweli tunasimamia matendo machafu ya Wakurugenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji mbovu ni mfumo, hata tungesema tuwe tunabadili Mawaziri kila siku hapa, haiwezi kusaidia kama mfumo ni mbovu, kama mfumo umechoka, kama mfumo ni chakavu kuanzia juu mpaka chini. Hali ni ile ile, nchi hii ilikuwa safi enzi ya Hayati Nyerere lakini baada ya hapo, nchi na mfumo wote umeharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeharibika kwa sababu ajira za Watendaji zinatoka kindugu, zinatoka kirafiki, zinatoka kimtandao, kwa hiyo, hata Mkurugenzi akifanya vibaya hawajibishwi. Hata Madiwani wakati mwingine wakijifunga wakamwajibisha, utakuta anahamishwa na kupewa Halmashauri nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukajiuliza nani anafanya hivyo; ni yule anayewateua na yule anayewaajiri. Kwa hiyo, naomba hili tulione kwamba ni kikwazo katika maendeleo ya nchi yetu. Hatutegemei kuleta mabadiliko yoyote. Tunachopaswa kuangalia ni kufumua mfumo mzima tuone tunatenda kwa ajili ya watu. Tunatenda kwa ajili ya Watanzaia. Maana kama ni mfumo wa rushwa unaingia mpaka kwetu Wanasiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kukuta ndani ya Halmasharui watu ambao wana *tender (contracts),* wenye Makampuni ni Madiwani, Wabunge au Mamea. Kwa hiyo, hata kama Mkurugenzi angependa kufanya mambo mazuri atayafanyaje wakati Wanasiasa wanamkalia kitako hapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Wakurugenzi katika nchi yetu wanafanya kazi vizuri. Nisikilizie basi, Wakurugenzi ambao wanakwenda kwenye Halmashauri wakaziba mianya ya kula, wanashughulikiwa na Wanasiasa. Tumeona katika Halmashauri mbalimbali, nenda Arusha pale uone, wapo *DCs* ni Wanasiasa, wapo *RCs* ni Wanasiasa,

[MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA]
watakwambia hatumtaki Mkurugenzi hatumtaki huyu hana adabu, hana heshima; hana heshima au kaziba mianya ya kula? Wapo Watendaji wazuri, siyo wote ambao ni wabaya. Wakisimama vizuri, sisi Wabunge wenyewe, Madiwani, *RCs,* na *DCs* ndiyo wa kwanza kuwachokonoa na kuomba wahame. *(Makofi)*

Naomba hata hilo tulione, basi kama Mkurugenzi anafanya kazi vizuri tumuunge mkono. Sisi Wanasiasa tutende vizuri ili tuhakikishe tunawasimamia ipasavyo, tuhakikishe kazi inaenda. Tusitoe mikono tu kwa Watendaji peke yao, tujiangalie na sisi Wanasiasa katika nafsi zetu kama tunatenda mambo yaliyo safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye elimu ya Madiwani. Huko nyuma Madiwani walikuwa wanapewa elimu nzuri. Hata mimi mwenyewe nimewahi kuwa Diwani kwenye miaka ya 2000. Kulikuwa na mafunzo ya maboresho ambayo yalikuwa yanawawezesha Madiwani kupewa elimu. Wanajifunza namna ya kusimamia Kamati za Uongozi, wanajifunza hata namna ya kusoma mizania. Ninachotaka kuwaambia ni kwamba, Wakurugenzi wale ni wasomi. *Planning Officers* wana *degree,* unakuta Madiwani wale wanaambiwa ujue kusoma na kuandika. Wanakuletea mizania na taarifa saa saba usiku wakati kesho yake ni kikao. Atasomaje huyo Diwani? Wakielimishwa watajua namna ya kusoma, natajua namna ya kusimamia Sheria za Manunuzi na watajua taratibu zinazowawezesha kuwasimamia Wakurugenzi wao.

Serikali isione kwamba inatumia pesa nyingi, hapana. Tutumie pesa kuwaelimisha, kwa sababu Madiwani wanaojifunza miaka mitano siyo wote wanaorudi, wengine hawarudi wanakuja wapya. Kwa hiyo, wapewe elimu kila baada ya miaka mitano wafundishwe. Madiwani wakifundishwa wataweza kusimamia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani wanasimamia Miradi yenye fedha nyingi, wanalipwa shilingi laki mbili na elfu hamsini. Wao wanafanya kazi tunazozifanya sisi,

[MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA]

wanaombwa hela kama tunavyoombwa sisi Wabunge, wanazika watu, wanatoa mahari, yaani kama sisi tunavyoombwa ndivyo na wao wanavyofanya. Tunawalipa shilingi laki mbili na elfu hamsini, wanafanya kazi wakati sisi tukiwa kwenye Bunge na pia wanasimamia Miradi mikubwa yenye pesa nyingi, watashawishiwa kwa sababu mapato yao ni madogo. Wanasimamia Miradi mikubwa ya mamilioni na mabilioni, watahongwa hawa watu. Tuwawezeshe waongeze kipato kidogo, angalau waweze nao kuwa na ule moyo wa kustahimili hivi vishawishi ambavyo vinaweza kutolewa na Wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye Bajeti. Tunayo Kamati ya Bajeti, tunashukuru kwamba imeanzishwa na tuna matumaini makubwa kwamba, kama mtaweza kufanya kazi inavyotakiwa, basi inawezekana mkaleta mabadiliko makubwa. Ukifuatilia katika Halmashauri hizi, pesa ya mwaka 2012/2013 imepelekwa katika Halmashauri zetu katika *quarter* ya kwanza ya Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, ni pesa nyingi karibu bilioni ishirini na kitu.

Pesa hizi ukienda katika Halmashauri zinaletwa kama bakaa. Hizi bakaa tusipoangalia kimahesabu zinaweza kupelekwa jinsi zilivyo na zikaliwa. Si hivyo tu, zikifika kwa wakati, Serikali na wale walioko kule hawataki kuzirudisha Serikalini, maana watazifanyia warsha na semina.

Semina nyingine ukienda, kuna Kamati moja waliniambia walienda wakaomba hata orodha ya walioingia kwenye semina, walikuta zimesainiwa na mtu mmoja, yaani mwandiko ni wa mtu mmoja, saini ya mtu mmoja, lakini zimelambwa basi. Kwa hiyo, unaweza ukaona Serikali inapopeleka pesa mwishoni kabisa, inawapa ushawishi Watendaji kuhakikisha kwamba, pesa zinatumika katika mambo ambayo sivyo ndivyo ili zisirudi Serikalini.

Hatutegemei kupata *Big Results Now,* kwa sababu Miradi hii haitatekelezwa kwa kuwa pesa zinakwenda. Nakumbuka kuna hii Sheria ya Manunuzi ambayo nayo naomba niiongelee kidogo, ina ukiritimba mkubwa,

[MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA]
inachukua miezi sita na zaidi kabla watu hawajapata Mkandarasi. Hii Sheria ina kitu kinaitwa *quotation.* Kimekuwa kinanipa mashaka mengi, wamesema Wabunge wengi sana hapa. Unaweza kukuta kitu kinauzwa shilingi moja kwenye soko lakini Serikali itakiandika shilingi tatu. Tuelezeni ninyi mna duka wapi?

Maana Serikali mmejipangia yenu na haya mambo ndiyo yanaruhusu watu waweze kuiba na haisemwi kwa sababu sisi wenyewe Wanasiasa, Mawaziri, sijui watu gani, ndiyo tuna mambo, sisi ndiyo Wakandarasi, ndiyo tunapewa *tender* za kununua. Kwa hiyo hii Sheria inakuwa siyo rahisi kuibadilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ametuambia kwamba, Bunge sasa tuangalie namna ya kuleta Muswada sisi wenyewe kama yeye alivyofanya kwenye Bajeti. Naomba Wanasheria mtusaidie na Mheshimiwa Naibu Spika wewe hapo ulipo ni Mwanasheria, kwa hiyo, tuhakikishe tunaleta Muswada sisi wenyewe tunabadili sheria. Serikali haiwezi kuleta kwa sababu wao wenyewe wengine wanahusika katika manunuzi haya na wanafaidika. Huwezi kutegemea kununua kitu mara tatu ya bei ya soko, Mradi hauwezi kukamilika. Utatumia gharama kubwa, gharama zikiwa kubwa basi na Miradi inafanywa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi *quotation* zina mambo ya ajabu, kuna mahali tumeenda wame-*quote* kuweka sinki la shilingi 300,000, lakini tumekwenda kukagua Mradi tumekuta sinki hata mtoto mdogo hawezi kunawa uso pale, lakini Wahandisi wanaruhusu malipo! Unaweza ukajiuliza kupitia Bunge naomba Wahandisi muwe na aibu.

Tanzania tujifunze kupitia nchi nyingine, nchi nyingine zina Umoja wa Wahandisi na hapa Umoja upo unafanya nini? Watoto wetu wanasomeshwa wanaenda kufuata mambo ya hovyo. Mimi nafikiri mtu unapopata elimu hata kama ingekuwa ndogo kiasi gani kule ku-*deliver* ndiyo kunakufanya uwe *proud* na ile elimu yako uliyoipata. Kwa hiyo, naomba hata Wahandisi watusaidie ili waisaidie nchi

hii iweze kwenda mbele. Hatutegemei chochote katika mwendo wa namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea yapi, kama mfumo hauwezi kubadilika, hakuna *quotations* na hakuna usimamizi, hakuna *Big Results Now.* Kwa hiyo, ninachoamini ni kwamba, kama tutajifunga kwa pamoja Wanasiasa pamoja na Watendaji, kweli tukawa na imani hapa na hasa sisi Wanasiasa, turidhike na tunachokipata. Siyo lazima twende kuomba rushwa tu hovyo hovyo huko chini kwa Wakurugenzi mpaka wanatukamata na kuturekodi kwenda kutupeleka Mahakamani, ni mambo ya aibu kabisa.

Kwa hiyo, hiyo inatuonesha sisi Wanasiasa ni dhaifu katika hili, tuhakikishe hatuwanyoshei mikono. Mimi nina uhakika Mheshimiwa Hawa Ghasia, nikikuuliza swali moja hapo ulipo, unaweza kuondoa Mkurugenzi? Kwa sababu Sheria za Kazi za Tanzania zina ukiritimba, mtu anaiba halafu unampa karipio, karipio kali sijui nini, unaweza ukamfukuza kesho akakudai mamilioni ya pesa. Turudie katika Sheria za Kazi kama hizi Sheria zinaruhusu mtu aibe halafu umhamishe au Sheria aibe sijui mpaka umpe karipio, karipio kali, sijui kitu gani, zina ukiritimba mkubwa ambao unafanya hata wale wanaowajibisha washindwe kuwawajibisha.

Kwa hiyo, nazo mzitazame, katika majumuisho Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI utueleze, inawezekana hapa tunakunyooshea vidole lakini huna uwezo wa kuondoa Wakurugenzi wako. Kama unao, maana najua kuna watu wengine wanawekwa na Rais wale wa Majiji labda inawezekana Rais naye mpaka awajibishe.

Inawezekana wa kwako ambao unaweza kuwawajibisha na wewe unalimwa makonzi usiwatoe. Kwa hiyo, naomba hilo eneo utuambie, ujivue msalaba huu Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, maana wewe ni mwanamke, ujisimamie kidete utueleze, kama huna uwezo wa kuwawajibisha Wakurugenzi utueleze wakuondoe katika msalaba huu, wanakunanga sasa hivi. *(Kicheko)*

[MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA]

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niseme Waziri Mkuu, amenangwa nae juzi hapa ajiuzulu na mimi niseme tunampenda lakini amezidi Ukristu. Ninaposema Ukristu unajua sisi tunafundishwa kukubali hata kupigwa kulia na kushoto, kunyenyekea. Kwa hiyo, unyenyekevu umezidi. Awajibishe watu wake. Watu wakiiba unasubiri nini mpaka mwaka mzima mtu unakwenda mpaka sijui karipio, yaani inaniudhi kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaweza kuondolewa kazini wa kuajiriwa wapo. Wapo watoto wetu ambao wamesoma wamekaa benchi, tuna watoto wanamaliza Chuo Kikuu kila mwaka, wamejifunza Utawala, wamejifunza Uhandisi. Kwa nini watu waibe mpaka Wabunge wanakuja kupiga kelele hapa halafu inakuwa *business as usual* hakuna hatua yoyote inayochukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naishia hapa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ukimpa nafasi Mheshimiwa Conshesta Rwamlaza atawamaliza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, atafuata Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay!

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie mjadala huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali isome kwa makini Taarifa za Kamati zote tatu pamoja na michango ya Wabunge wenzangu waliochangia, kwa sababu hali ni mbaya sana. Hili jambo lisiwe siasa, tusifanye siasa kwa sababu fedha zinazokwenda katika Halmashauri zetu na zinazokwenda katika Wizara mbalimbali zinaliwa. *(Makofi)*

Nikiona tunabishana hapa na kutupiana vijembe, kwa kweli hatuko sahihi. Inafaa tuwe makini na tuchukie

[MHE. MICHAEL L. LAIZER]
hali hii kwa sababu Wananchi wetu wanateseka kwa sababu ya Miradi ambayo haitekelezwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niifahamishe Serikali kwamba, Miradi inayojengwa chini ya kiwango ni hasara kubwa kwa Wananchi. Halmashauri ambazo hazipati fedha kwa wakati, kwanza, hiyo ni hujuma. Ningelipenda kuiambia Kamati ya Bajeti, waangalie sana kwa sababu Halmashauri zetu zinatofautiana; kuna Halmashauri zinazopata fedha na kuna Halmashauri ambazo hazipati fedha. Hivi ni kwa nini kunatokea utaratibu huo, Halmashauri ambazo hazipati fedha wana kosa gani? Hii inaleta ubaguzi mkubwa sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana Kamati zote, lakini Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* wamesema jambo muhimu; kuna watumishi hewa wanaolipwa, waliotoroka, waliostaafu na waliofariki. *(Makofi)*

Hivi Serikali haithibitishi hizi fedha za mishahara kweli zote zinakwenda kwa watumishi waliopo? Hapa ninaona Serikali wamefumba macho.

Taarifa za *CAG,* kila mwaka anatoa mabilioni ya fedha zilizoliwa, lakini Serikali inakaa kimya. Ninawashagaa, ninataka nisahihishe jambo moja ambalo sisi Wabunge tunakosea. Tunadhani kwamba, Watendaji hawa walioko katika Halmashauri au walioko katika Serikali ni Makatibu wa CCM; hapana. *(Makofi)*

Hawa asilimia kubwa siyo Wanachama wa CCM, wengine wanaihujumu Serikali hii, lakini ni kosa kwa Serikali kunyamaza kimya. Awe ni wa CCM, awe siyo wa CCM ni mwizi, mwizi hana Chama ni mhalifu. Tusidhani kwamba, wote ni Wana-CCM. Inaonekana kwamba, Watumishi wote walioko Serikalini ni Wana-CCM, hapana, kuna wengine wa vyama mbalimbali nao ni wezi. *(Makofi)*

[MHE. MICHAEL L. LAIZER]

Mheshimiwa Naibu Spika, *BRN* tunayoisema hapa, hatuwezi tukafanikiwa tukiacha wizi huu uendelee. Ianze *Big Reshuffle Now* kupunguza kabisa wezi wote. Ninakubaliana hata kama kuna Mawaziri ambao hawawezi kazi, nao *reshuffle* hiyo iwakumbe. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Naibu Spika, Watendaji wanaweka manunuzi makubwa sana kupita kiwango kinachostahili. Wizi unapita katika manunuzi. Ninaomba Serikali iliangalie jambo hili na isikae kimya katika jambo hili. Ninaomba michango ya Wabunge muifuatilie kwa sababu ni kilio. Ninawashangaa sana Wabunge ambao watatetea jambo hili kwamba siyo kweli. Ninadhani Mawaziri nao wanafahamu kwa sababu hata katika Halmashauri zao mambo haya yanatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi katika Halmashauri zenu Waheshimiwa Mawaziri hakuna wizi? Huu wizi upo katika Halmashauri zote, hakuna Halmashauri ambayo ni salama. Ukitaka kuangalia chukua maboksi yote ya *CAG,* ukichambua Halmashauri yangu haipo hapa, hata ukikutwa katika sehemu moja huo ni wizi. Inawezekana wewe upo katika eneo moja lakini mabilioni ya fedha yamekwenda, sasa hizo ni halali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuzungumzia hilo suala la manunuzi kwamba ni mabaya na inafaa Serikali ichunguze kama kuna matatizo katika mfumo wa manunuzi, sheria iletwe hapa Bungeni tuirekebishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Kamati ya *LAAC* kwamba, kuna mtandao mkubwa sana wa ufisadi unaoendelea kuhujumu Halmashauri. Hawa wamepata nafasi baada ya kuona kwamba, ukiiba sana unapata *promotion.* Kwa hiyo, wengine wameona kumbe ni faida kuiba, anapewa *promotion,* anapandishwa ngazi, badala ya kufukuzwa au kupelekwa Mahakamani. Hii inaonekana ni *promotion* siyo adhabu. *(Kicheko/Makofi)*

[MHE. MICHAEL L. LAIZER]

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumfahamisha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), malalamiko mengi sana yanakwenda TAMISEMI na wanasingiziwa Madiwani ndiyo hawafanyi kazi, hiyo siyo kweli. Malalamiko makubwa katika Halmashauri wakiwalalamikia Watumishi wabovu, ndiyo hawafanyii kazi na Madiwani hawawezi kuwahamisha hao wafanyakazi wabovu na wakiwafukuza wakati mwingine wanarudishwa na TAMISEMI na wakati mwingine wanarudishwa na Mahakama. Sasa Madiwani watafanya nini?

Ninaomba hili suala la wizi Halmashauri na maeneo mbalimbali katika Serikali yetu, Serikali sasa warudi katika kuangalia michango yote ya Wabunge, kuangalia Taarifa ya *CAG* na kuifanyia kazi kwa sababu hali ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Lekule Laizer. Mheshimiwa Mustapha Akunaay!

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu. Nianze kwa kuwapongeza Kamati zote tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hizi tunazozijadili leo ni kwa mujibu wa Kanuni na katika Kamati zote imedhihirika kwamba, mambo mawili ni ya wazi. Kwanza, kitu kinachozungumzwa ni *Financial Reporting* kwa ajili ya uwajibikaji, yaani *Accountability;* pili, kwa ajili ya *Good Governance,* yaani Utawala Bora. Mimi nitaanza na Kamati ya Bajeti.

Nimeisoma Taarifa ya Kamati hii ya Bajeti, ninaipongeza sana pamoja na kwamba ni mara ya kwanza. Ninataka kushauri kuhusu vyanzo vya kodi. Kamati ya Bajeti itakapokuwa inazungumzia vyanzo vya kodi, izingatie sana uchambuzi na utafiti wa vyanzo hivyo kwamba athari yake

[MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY]
ni nini. Mwisho wa yote ni kodi kwa Wananchi. Sasa hivi hapa Tanzania kodi zimekuwa nyingi sana. Kwa hiyo, kama vyanzo vitaongezeka, iwe ni mahali ambapo haijaguswa na kodi yake haijatozwa, lakini siyo vyanzo vilevile na kodi inaanza kuongezwa.

Kwa mfano, Kamati ya Bajeti ilipoweka kodi ya mapato ya shilingi 14,000,000 kwa mwaka kwamba, watumie ile mashine ya *Electronic Fiscal Device (EDF),* pale palichukuliwa kianzio ambacho siyo sahihi. Kwa sababu pesa ile ni kiwango kidogo sana na watu wengi sana watahusishwa kununua mashine ambazo ni za bei ya juu. Ingekuwa wamechukua kiwango ambacho ni cha juu, labda kama ile ya *VAT,* Shilingi 30,000,000 au 40,000,000 kwenda juu, wange-*net* walipa kodi ambao wengekuwa wa maana.

Pili, Wabunge walizungumzia Bajeti, fedha zikaongezeka, ni jambo ambalo lilikuwa haliwezi kuepukika. Nyongeza ilipowekwa baadaye, Wabunge hawakujadili, kwa mfano, katika eneo la simu kutozwa kodi. Sasa baadaye ikaleta matatizo makubwa, kwa hiyo, katika nyakati za baadaye ninashauri Kamati iangalie sana ili isije ikafanya Bajeti ambayo baadaye ikawa chini tena ya makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati ya Bajeti, kuna suala la Kamati yenyewe kutokuwa na Wataalam, hiyo nimeiona. Ninashauri kwamba, Kamati hiyo ipewe *beef-up* ya wataalam ili wafanye utafiti, tuiwezeshe Kamati ifanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumzia sasa Kamati ya Hesabu za Serikali. Katika Kamati hii nimeona mambo mawili, matatu. La kwanza, Deni la Serikali linakua kwa kasi sana, imefikia nusu ya *GDP.* Hiyo ni hatari kwa sababu deni hilo kabla halijakopwa, Wabunge hawajajadili ni kitu gani kitakopwa na malipo yake baadaye riba ni kubwa sana na Wananchi watakuwa wanatozwa wanalipa deni ambalo hawalijui. Kitu kingine ambacho

[MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY]
kimejitokeza katika Kamati hii, kuna kesi nyingi Mahakamani mpaka Shilingi 154,000,000,000 ambazo ni ubishani wa kodi kati ya *TRA* na walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* tuliishauri miaka mingi isiwe inafanya mipango ya kodi ya nguvu ili baadaye Wananchi wafanye ubishano. Mabishano mengi yakichukua muda mrefu Mahakamani, itakula pesa zaidi na mwishoni kama watu hao watashinda itachukua kodi za Wananchi kuwalipa watu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona vilevile kuna dhamana za Serikali ambazo zimedhamini madeni ambayo hayana *guarantee* kubwa, hiyo ni hatari katika uchumi wa nchi. Kwa sababu watu wengi wamezungumzia eneo hili, ninaona nihamie sasa kwenye eneo la Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia hapa Serikali ambayo inaongozwa na Chama cha Mapinduzi. Serikali ya CCM ikifanya kitu kizuri, tunasifu, Wanachama wa CCM na Wabunge wao wanapiga makofi; lakini tukiuliza au tukiwaambia hapa wamefanya makosa wanakasirika na Wabunge wanachukua nafasi ya kuitetea Serikali. Serikali inatakiwa itetewe na Mawaziri. Wabunge wote kazi yao ni kuihoji Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninataka kuwashauri Wabunge hapa ndani ya Bunge hili kwamba, kila mmoja ajue amekuja kufanya nini. Ninataka kutoa mfano kwamba, kuna Halmashauri 71 zenye mahesabu ambazo zilikuwa nyaraka hazionekani, ikatamkwa Halmashauri moja ya Karatu ambayo inaongozwa na CHADEMA. Halmashauri ya CHADEMA, ipo inaongozwa na Serikali ile ile ya Chama cha Mapinduzi, isipokuwa Madiwani pale wengi wao ni wa CHADEMA, lakini *per se* ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ya Mheshimiwa Vita Kawawa, Halmashauri ya Karatu ina

[MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY]
Sekondari katika kila kijiji, ina Zahanati katika kila kijiji na maji imeweka karibu kila kijiji bila kutumia hela ya Serikali. Hiyo ni taarifa tu kwa kifupi, lakini sasa ngoja nizungumzie kwenye Halmashauri yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ngoja nizungumzie kwenye Halmashauri yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mustapha Akunaay, alichohoji Mheshimiwa Vita Kawawa ni zile hoja za Mkaguzi tu. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimeisoma ile Taarifa ya *CAG* vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba nizungumzie Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu. Halmashauri yangu inaingiliwa na Viongozi; kwanza, Mwenyekiti wa Halmashauri ni Mwenyekiti wa CCM; pili, Mkuu wa Wilaya anaingilia kazi ambazo ni za Watendaji. Tumekwama kiasi kwamba, kijiji chochote ambacho wanakijiji wamemwondoa Mwenyekiti, hakuna uchaguzi unaofanywa kwa sababu ya uwoga kwamba labda CCM itashindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), aangalie katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ni vijiji vingapi ambavyo havijafanya uchaguzi kwa zaidi ya miaka miwili. Wananchi hao wamechanga pesa zao za maendeleo, lakini Ofisi za Wenyeviti zimefungwa kwa sababu hakuna uchaguzi unaofanywa. Hili ninampa tu kama *light touch* kwa sababu mambo ni mengi, acha nizungumzie mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri yangu ina matatizo makubwa kwa sababu ya pesa kuchelewa. Pesa za maendeleo zinachelewa, Wananchi wamechanga pesa zao, Miradi yao imekuwa magofu. Kwa zaidi ya miaka

[MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY]
mitatu, pesa nyingi za maendeleo hazikuletwa. Sasa hatuelewi ni kwa sababu Mbunge ni wa CHADEMA au katika Hazina ya Tanzania pesa hazipo!

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii itaendelea tu kama pesa zilizopangwa zitakuja kwa wakati. Labda nizungumzie kwa ujumla, nchi nzima hii Sheria ya Manunuzi ibadilishwe. Haya mambo ya zabuni ni mahali ambapo wizi mkubwa huwa unafanyika. Kitu cha shilingi 3,000,000 katika zabuni kinanunuliwa kwa shilingi 9,000,000. Hii Sheria ibadilishwe, tufanye *procurement* wenyewe na Maafisa Ugavi wanunue wenyewe kwa sababu watakuwa *audited* tutawadhibiti. Jambo lingine ni kwamba, katika Halmashauri nchi nzima kuna *conflict of interest.*

Halmashauri wenyewe, Wafanyakazi wa Halmashauri pamoja na Madiwani, Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri, hao hao ndiyo wanaochukua zabuni. Wanajulikana na hakuna mtu anayewachukulia hatua, mwisho maendeleo ya Wananchi yanarudi nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninataka nizungumzie ni juu ya Ukaguzi wa Ndani. Wakaguzi wa Ndani katika Halmashauri zetu ni kama hawapo. Tunaomba TAMISEMI iiangalie Kada hii. Hii Kada pamoja na Kada ya Wanasheria, aidha, kisomo chao hakitoshi au hawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie jambo la mwisho; Mikataba mingi ya Halmashauri ni mibovu. Hakuna kesi yoyote ambayo Halmashauri ilishitakiwa ikashinda kwa sababu Mikataba iliandikwa na Wanasheria ili Halmashauri ianguke.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba *Contract Management,* wale Wanasheria walioko kwenye Halmashauri wapate hata kozi fupi fupi, kwa maagizo ya TAMISEMI, hata Halmashauri zilipie, lakini waende kwenye mambo ya *Contract Management,* ama wapewe *tution* na Mawakili wa Serikali.

[MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY]

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ninamwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwamba, Wananchi wanakuwa na kesi nyingi Mahakamani katika vijiji vingi lakini Wanasheria wanawaachia. Sasa wale Wanasheria kazi yao pale ni nini iwapo Wenyeviti wa Vijiji wanakwenda Mahakamani lakini Wanasheria hawawasaidii?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay. Mheshimiwa Ezekiah Wenje!

MHE. EZEKIAH D. WENJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na mimi kupata fursa ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuanza kwa kusema kwamba, Waingereza wanasema kwamba; *sometimes it is better to be silent, to be thought a fool than to speak out and clear the doubt.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa sababu asubuhi nilimsikia Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, alivyokuwa anazungumza. Napenda niseme kwenye Bunge lako Tukufu kabla sijaanza kuchangia kuwa, Taarifa ya *CAG* pamoja na Taarifa aliyoiwasilisha Mheshimiwa Zitto Kabwe, hakuna hata sehemu moja ambayo ime-*implicate* Chama changu cha CHADEMA. Mheshimiwa Mgimwa alizungumza *as if* kuna *report* humu ambayo inatu-*implicate* popote pale. Naomba kusema kwenye Bunge lako Tukufu kwamba, hakuna sehemu hata moja ambayo inatu-*implicate* popote pale kwenye Taarifa ambazo ziliwasilishwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kila siku tukizungumza hapa ninyi mnasema Serikali yenu, Serikali yenu, leo *you guys you want to run from your Government, you cannot run from your shadow,* yaani huwezi kukimbia kutoka kwenye *shadow* yako. *(Makofi)*

[MHE. EZEKIAH D. WENJE]

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweke misingi ya hoja yangu sasa. Katika Ripoti ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa *LAAC,* ametupa ripoti za maeneo mengi ambapo Halmashauri zimefanya kazi nzuri, kuna Hati Safi, Hati Chafu na Hati zenye Mashaka. Naomba niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii Halmashauri inayopata Hati Safi na inayopata Hati Chafu na inayopata Hati yenye Mashaka, zote zinalingana tofauti tu ni kwamba, anayepata Hati Safi *is a smart thief, is the innocent thief,* kwa maana kwamba, ni mwizi mjanja anayeweza kuweka *document* sawa na ndiyo maana ukienda kwenye Halmashauri iliyopata Hati Chafu na ile iliyopata Hati Safi kiwango cha maendeleo hakitofautiani. Ukienda kuangalia madarasa waliyojenga ni madarasa ambayo ni *disposable,* yaani wanajenga darasa ambalo baada ya miaka miwili halipo.

Wanajenga darasa ambalo mkiangalia madarasa ninyi wazee mliosoma zamani, kwa mfano, waliosoma *Tabora Boys, Bwiru Girls and Boys* and Mwanza, mpaka leo zile shule zipo na zilijengwa enzi hizo. Leo Shule za Kata zinajengwa na Halmashashauri hizi tunazozisimamia ndani ya miaka miwili hakuna *floor* na shule imechakaa, *under your nose* na ninyi ndiyo mnaangalia hii shughuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmejenga mpaka *disposable roads,* yaani mmejenga barabara ambapo inajengwa barabara ya lami leo inapita hapa na ndani ya miaka miwili ina mashimo matupu ni *disposable roads*, sijawahi kuona popote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema ukirudi Mwanza, juzi Mheshimiwa Rais alikuja kuzindua hospitali ambayo *in the last three years* ilifanya *major renovation*, ikatumika pesa nyingi. Juzi tulipoingia hakuna *floor,* ikabidi watengeneze upya kwa pesa nyingi, Rais amekuja kuzindua. Hizi zote ni *disposable things.* Leo mnajenga *disposable roads, disposable schools, disposable hospitals* na *disposable dispensaries.*

[MHE. EZEKIAH D. WENJE]

Ndugu zangu, nchi haiongozwi kwa kaulimbiu, niliwahi kuwaambia hapa. Mlianza na MKURABITA, MKUKUTA, mkaja na KILIMO KWANZA, ambayo ilikufa siku hiyohiyo na leo mmeibuka na Kiingereza kinaitwa *Big Results Now* ili kupiga Wananchi kamba! Hii nchi haiongozwi kwa kaulimbinu, nchi inaongozwa kwa uadilifu, uwajibikaji na nidhamu, lakini siyo kaulimbiu ndugu zangu nawaambieni!

Ukisoma Ripoti ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa *LAAC*, ukurasa wa 17 na 18, wanapozungumzia kuhamisha watumishi wezi, ngoja nianze na Mwanza. Kamati ya *LAAC* ilikuja Mwanza, Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza alikuwa anaitwa Wilson Kabwe, ni *professional thief*. Sasa Kamati ikaja Mwanza ikagundua, *no, it is true* Kamati ya *LAAC* ilikuja na wakagundua ufisadi walioufanya kwenye fedha za *NSSF* eneo la Bugarika.

NSSF ilikuja kununua viwanja Mwanza, wakalipa *more than one billion* kwamba, Wananchi walipwe *compensation* eneo linaloitwa Bugarika. Wakachukua viwanja, Wananchi wakanyang'anywa viwanja vyao, lakini hakuna faidia waliyopewa. Kamati ilikuja, *the best thing* ambayo Serikali ilifanya ni kumchukua Kabwe kumhamisha kutoka Mwanza akapelekwa Dar es Salaam!

Miongoni mwa watu waliotajwa kwenye Ripoti ya *LAAC* ni Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, wamenyang'anya watu ardhi kila maeneo. Bugarika kuna mgogoro wa ardhi, ukienda Luchelele kuna mgogoro wa ardhi, ukienda kwa Wamachinga mpaka Kabwe alikuwa anawapa bunduki kwenda kuwaua Wamachinga, ana maloloso mengi. Kazi mnayoweza kufanya ni kumhamisha kumtoa Jiji la Mwanza mnapeleka kwenye Jiji kubwa zaidi ili aende akaibe zaidi na ndiyo maana Wabunge wenzangu wanasema kama mnafanya haya, yawezekana basi Waziri anajua na Waziri Mkuu anajua, kwa sababu Mkurugenzi wa Jiji ni *appointee* wa *President*. Mambo gani haya mnayafanya halafu mnaongoza nchi, ni kaulimbiu tu kila siku, Taifa haliongozwi kwa kaulimbiu! *(Makofi)*

[MHE. EZEKIAH D. WENJE]

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wenzangu wamesema, katika mfumo wa *tendering* kwenye Halmashauri, mkifanya leo tathmini mtagundua kwamba, *in the last ten years* kama Taifa, tumepoteza pesa nyingi mno kwenye *tendering process,* kwa sababu wana-*inflate* bei ya hali ya juu. Unakuta maji ambayo yanauzwa shilingi 500 inapoenda kuuziwa Serikali yanauzwa kwa shilingi 3,000; *this business is too much!*

Kwa hiyo, kama tatizo ni hii Sheria ya Manunuzi, haya ni mashinikizo ya *donors*, kama ni vipi *let us go away with this* Sheria, inalifilisi Taifa. Kwa sababu *the most level of devolution* katika nchi yetu ni *Local Government*. Sasa tusipopeleka nguvu ya kuweza ku-*control mechanism* kwenye *Local Government* haki ya mama Taifa hatutaenda popote kwa sababu pesa nyingi zinakwenda kwenye *Local Government* na kule ndiyo madili yanapigwa.

Unakutana na *Engineer* wa Halmashauri ana ghorofa ambalo hata Waziri hana. Unakutana na Mhasibu kwenye Halmashauri ana maghorofa ambayo hata Waziri hana. Unakutana na *Treasurer* wa Halmashauri ana ghorofa ambalo hata Waziri Mkuu hana. *Where do they get all these money*? Ndiyo maana kuna haja ya kuweka *very big control mechanism* ndani ya Halmashauri. Hii ndiyo *last level of devolution in our country, this is the only way to serve the country.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie hoja moja ambayo naomba majibu kutoka Serikalini. Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Sera ya Serikali yenu inasema, Elimu ya Msingi ni bure. Leo wanafunzi wameanza kusajiliwa darasa la kwanza nchi nzima kila kona, lakini ukiangalia usajili wa mwanafunzi anapoingia darasa anaambiwa wanataka pesa ya mlinzi, pesa ya dawati, pesa ya maji, pesa ya nembo na kadhalika. Ukiangalia gharama yote ambayo mzazi anatakiwa alipe mtoto anapoingia darasa la kwanza maeneo mengine inafika mpaka shilingi 60,000, 20,000 au 30,000; *who is fooling who*? Nani anamdanganya nani? Mnawaambia Wananchi kwamba, elimu ni bure

wakati Elimu ya Msingi siyo bure. Tuliuliza mpaka ndani ya Bunge hapa kwamba, toeni tamko ili tujue msimamo wa Serikali.

Sasa hivi tunapoenda kwenye *Christmas, January* darasa la kwanza wanaanza shule, hii ndiyo *pressure all over* kwenye Majimbo yetu sasa. Siyo kwetu tu, hata hawa wenzangu wa CCM hii *pressure* ipo kwenye Majimbo yao wanafunzi wanapoingia darasa la kwanza. Tupeni msimamo wa Serikali, msidanganye Wananchi, mmepiga watu kamba ya kutosha!

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishauri Bungeni kwenye Taarifa mbalimbali kwamba, katika Halmashauri kuna hawa watu wanaitwa Maafisa Ardhi, ukija kwenye Miji kama Mwanza, Dar es Salaam na Arusha, hawa watu ndiyo chanzo cha migogoro ya ardhi kwenye hizi Halmashauri. Tulishauri muda mrefu kwamba, iwepo *reporting line,* wanaweza wakatumia hizi ofisi za Halmshauri, lakini waripoti kwenye Wizara ya Ardhi *direct,* lakini watumie *facilities* za Halmashauri iwepo *doted reporting line*. Hawa watu ni chanzo cha migogoro. Mimi kila siku nasema, tatizo tulilonalo Mwanza kubwa kuliko yote ni migogoro ya ardhi. Ule mji unakua kwa kasi Barani Afrika kuliko miji mingine yote. Sasa Mji unapokua kwa kasi na thamani ya ardhi inakua kwa kasi hiyohiyo. Kwa hiyo, ardhi Mwanza imekuwa dili.

Leo nimekaa hapa kuna Wananchi wa eneo moja linaitwa Sawa, wananipigia simu kuna watu wamekwenda wanataka kuchukua ardhi, Eneo la Isebanda watu wanataka kuchukua ardhi. Luchelele tuna migogoro ya kudumu na Bugarika tuna mgogoro aliouanzisha Kabwe. Hebu chukueni ushauri wetu basi, la sivyo tunazungumza hapa tunafanya nini? Mnatuleta hapa tuzungumze ili iwe *formality* kwamba tulizungumza au tunazungumza *seriously* mchukue mawazo tunayowapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kusema msamaha wa kodi nchi hii tumesema mara nyingi sana na tozo za *line* za simu kwa

[MHE. EZEKIAH D. WENJE]

mfano, ililetwa tu na Serikali kwa sababu imefikia wakati Serikali ina-*feel* haioni mapato yanayotoka kwenye *Telecom Sector.* Tumezungumza mara nyingi kwamba, leteni *traffic monitoring system,* ni danadana tu kwamba, ooh, inakuja, inakuja; imekuwa mvua hiyo? Wekeni *traffic monitoring system* na mkileta mta-*realise* mapato makubwa sana. Hata hizi tozo kwenye *line* za simu ambazo mmewaingizia Wananchi hata kama Wananchi hawataki, yaani mnalazimisha tu, Wananchi hawataki hii tozo mmeiweka kwa nguvu, kwa sababu ni udhaifu wa mifumo yenu ya kazi ambayo hamuwezi mkadhibiti au hamna *traffic monitoring system.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kila Mbunge amesema, wasomi mbalimbali wamesema kwamba, nchi hii misahama mbalimbali ya kodi kwenye mafuta kwa mfano, tulisema hapa kwamba, mafuta yote yanayokwenda kwenye migodi ni *tax free.* Sasa kama mafuta ni *tax free* halafu mama ambaye yuko kijijini anatumia *kerosene* ninyi mnamtoza kodi, mnamsaidia nani; mnawasaidia Makaburu wanaokuja kuwekeza au mnawasaidia Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Peter Msigwa!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami nianze kwa kuzungumzia Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu, Bunge la mwaka 2011 la Bajeti, nilitoa takwimu ambazo zilitolewa na Wizara ya Afya kwamba, 42% ya watoto wanaozaliwa Tanzania, wanadumaa na mtu anayedumaa maana yake hawezi kufikiri, hawezi kuhoji wala hawezi kudadisi. Kwa kutumia takwimu hizi hizi na kwa sababu takwimu hizi zilianza tangu nyuma, nina wasiwasi kwamba, katika Baraza la Mawaziri ambao wapo 56, kuna

uwezekano 40% wamedumaa na zaidi kwa sababu ya changamoto tunazozipata katika Bunge hili.

Pia, ninaipenda ile nukuu ambayo niliisema na ninaomba niirudie tena, kwa sababu hatujaja hapa kucheza. Naomba mnisikilize ni wakati wangu, anayekunja uso na akunje tu, lakini *I have to speak, this is my right,* kama hujadumaa shauri yako, kama hujadumaa *deliver*. *(Makofi)*

Insanity is doing the same thing in the same way and expecting different results. Narudia tena haya maneno kwa sababu inaonekana haijaeleweka. Wabunge wenzangu wote wamezungumza hapa kwamba, kila mwaka tunarudi tunazungumza yaleyale. *CAG* anapokuja yeye ni kioo cha Serikali, anakuja hapa kutusaidia kutuelekeza ili tujirekebishe. Tunapopata majibu yaleyale watu hawabadiliki, maana yake *there is something wrong in our mind* na hili ni Baraza la Mawaziri ambalo lipo tunategemea li-*deliver*.

Kwa hiyo, tunapozungumzia matatizo tunayoyapata katika nchi hii na wizi wa fedha ni tatizo kubwa ambalo ni lazima tupate ufumbuzi. Haiwezekani watu wazima kila siku tunasema hayohayo, matokeo yaleyale, tunatumia mbinu hizohizo, tunategemea turudie kusema hivyohiyo, halafu tukiwasema watu mnakunja uso, hatuwezi kunyamaza! Inaonekana baada ya kusema sasa hivi Baraza la Mawaziri limeongezeka kidogo limesogea, kwa hiyo, kumbe kusemasema inasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa na *mental problem you have to offer mental solution*. Sasa hapa inawezekana inawezekana tuna *mental problem* halafu tuna-*offer economical solutions;* na hili ndiyo tatizo. Labda tu-*deal* na *mental problem* tupate *mental solution,* kwa sababu haiwezekani tuwe tunazungumza mambo hayohayo kila siku halafu hayabadiliki.

[MHE. MCH. PETER S. MSIGWA]

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza suala la pesa zinazoliwa kwenye Serikali zetu za Mitaa. Huku kwenye Halmashauri kuna matatizo mengi na niseme kwamba, juzi nilizungumza hapa wakati nachangia kwamba, kwenye fikra za watu mawazo bado hayajabadilika. Tupo kwenye Mfumo wa Vyama Vingi, ipo kwenye vitabu lakini kwenye fikra za watu wengi bado wanadhani tupo kwenye Mfumo wa Chama Kimoja. Natoa mfano kwa nini kuna matatizo kama haya.

Kwa mfano, kwenye Halmashauri yangu, Meya na Madiwani wanaweza wakawa chanzo cha ubadhirifu wa fedha. Kwa mfano, utakuta magari ya Manispaa, magari ya Halmashauri, yanatumika kwenye shughuli za Chama cha Mapinduzi, wakati tupo kwenye Mfumo wa Chama Kimoja, ambapo ni kinyume kabisa na utaratibu. Utakuta Mkurugenzi analazimishwa na Madiwani na Wakurugenzi eti waende uwanja wa ndege kumpokea Nape na Kinana kwenye shughuli za Chama cha Mapinduzi kwa kutumia magari ya Manispaa ambayo ni ya Serikali. Huu ni ubadhirifu na haikubaliki! *(Makofi)*

Waziri yupo, Waziri Mkuu yupo, huu ni uvunjaji kabisa wa kanuni na uendeshaji wa nchi yetu, ambapo tumeamua kabisa kwamba, sasa hivi tupo kwenye Mfumo wa Vyama Vingi. Vyama Vingi hivi vinapata ruzuku yake kutoka kwa Msajili wa Vyama na vinajua namna ya kujiendesha. Kutumia magari ya Serikali na kutumia rasilimali za umma kwenye shughuli za vyama ni utovu wa nidhamu. Huku ni kutokuwa na *ethics* katika utendaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hawa Ghasia, naomba hawa watu ambao wapo chini yako, hii tabia waiache kwa sababu ni kukosa nidhamu.

Ukisoma katika Kitabu hiki cha Mwenyekiti wa *LAAC,* nirudie kama alivyosoma rafiki yangu anasema; hata hivyo, Kamati imebaini kuwa bado kuna ubadhirifu, ufisadi na utovu wa nidhamu wa hali ya juu wa matumizi ya fedha za umma. Hii ni pamoja na utovu wa hali ya juu wa kutokufuata

taratibu. Wabunge wenzangu wengi wamezungumza hapa, ukiona Meya ni rafiki sana wa Mkurugenzi, basi hapo kuna dili wanapiga na ukiona Mkurugenzi anasimamia pesa vizuri, utasikia huyu Mkurugenzini CHADEMA. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuna matatizo makubwa sana kati ya Mameya na Madiwani ambao wengine wanafanya dili, wanawasumbua hata Watendaji wa Idara kwenda kuwaomba pesa za mafuta, kuwalazimisha Wakurugenzi wapate mafuta na Wabunge wengine wanaomba pesa kwa Wakurugenzi. Wabunge wengine kweli wapo humu ndani, vikao vikiendelea kule wanakwenda kuchukua fedha tena wanapata *double payment.* Hiyo ni lazima tuikemee! Hii ni laana mbele za Mungu, kwa sababu tunawaibia Wananchi. *(Makofi)*

Haya ni mambo kama tunataka tuwe na *discipline* na wengine wanamchukia *CAG*. Nilizungumza siku moja kwamba ni sawa na gari lako, hizi *sight mirror* zinapokuonesha kwamba kuna gari linarudi nyuma unachukia nini si uendeshe gari lako vizuri? Kama tunavyowaambia sasa kwamba hamko sawasawa na ninashukuru ufalme wenu umeanza kufitirika.

Tumezungumza miaka mitatu iliyopita hapa kwamba, kuna wizi kwenye Halmashauri, kuna Mawaziri ni mzigo, lakini hii sauti imesikika sasa mpaka Katibu wenu wa Chama anasema hadharani kwamba, watu wengine wanafunga tai tu ni mzigo, kazi yao ni kufunga tai na kutembea mjini. Haya ni maneno ya Katibu Mkuu wa Chama chenu. Amefika mahali anakiri ... (*Makofi*)

MJUMBE FULANI: Kitaje Chama!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Ni Chama cha Mapinduzi, kwani ni chama cha magamba.

Anasema ni mzigo. Alipokuwa Mbeya Mjini, bahati nzuri hakusogea Iringa, amekiri amesema niwaombe radhi Wananchi wa Mbeya na siyo awaombe radhi Wananchi

[MHE. MCH. PETER S. MSIGWA]

wa Mbeya tu, awaombe radhi Watanzania. *For three solid years we have been telling you guys you don't listen*. Sasa mnaongea lugha yetu kwamba kuna wezi, katikati yenu kuna Mawaziri mzigo, mnaanza kucheza muziki wetu, mmeambiwa ni mzigo.

Huu ufisadi ambao kwa miaka mitatu zaidi tumezungumza toka tumeingia Bungeni tukaambiwa wengine Wachungaji wa Nguruwe, tukaambiwa waongo, isipokuwa mkiambizana wenyewe ndiyo mnakubaliana. Wakati umefika kwamba, ni lazima kila mtu abebe mzigo wake. Lazima turudishe Taifa kwenye nidhamu, kila mtu atimize wajibu wake. Taifa limekuwa halina nidhamu, hakuna *ethics* wala hakuna kujali.

Mmeondoka na *big results* anayozungumza Mheshimiwa Wenje hapa, kuna shule moja Iringa mwaka juzi alipita Mheshimiwa Mwanri, bahati mbaya hayupo hapa, alikuta shule wameijenga chini ya kiwango imebomoka kabisa yote. Wananchi wa Ipogolo waliandamana wakaja wamechukia, shule ikabomolewa tukalalamika, ile shule imejengwa tena hatujui pesa zimetoka wapi, lakini hakuna hata mtu mmoja aliyechukuliwa hatua, halafu tunakuja hapa na *Big Results.* Ukienda kwenye Halmashauri saa hizi mmebandika makaratisi *"Big Results, Big Results"* watu wame-*claim* kama kasuku; *do they really understand meaning of Big Results? (Kicheko)*

Do we really understand the meaning of Big Results au ni masuala tu tume-*copy* na ku-*paste* tunataka tuwahadae Watanzania? *What is big result real mean?* Tuko *seriously* kwamba, tunataka tuwe na mabadiliko ya kweli, watu hatujawaandaa, watu ni wale wale, wanafikiri vilevile, wanawaza vilevile, wanatenda vilevile, *Big Result Now.*

Ndugu zangu, Wabunge wenzangu wamezungumza sana, tutaonekana kichekesho kwa Wananchi ambao wametuamini. Hebu tuchukue hatua basi kwa sababu kila

[MHE. MCH. PETER S. MSIGWA]

mtu analalamika hapa, sasa tutaondokaje. Wizara ya TAMISEMI, Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa sababu wewe ndiyo uko hapa, Wizara yako inabeba shutuma nyingi na lazima tuibebeshe. Ukienda kwa mfano Wizara ya Mazingira, tunalalamika labda miji yetu michafu, lakini Wizara yako ndiyo ina watu, wewe ndiyo una watu, kwa hiyo, lazima mzigo mkubwa tukubebeshe wewe. Wale watu kule chini wasipofanya kazi tutakufuata wewe.

Turudi tena kama alivyosema Mheshimiwa Leticia Nyerere, labda tuna tatizo la rasilimali watu hata tukisema tukutoe wewe tutamuweka nani maana yake ni yale yale?

Sasa na mimi niwaombe Watanzania, muda mwafaka umefika, hiki Chama ni chakavu, kimechoka, ni vizuri tukaleta Chama mbadala kwa ajili ya kuliokoa Taifa hili. Kwa sababu kama ni Baraza la Mawaziri limebadilishwa mara kibao, lakini hakuna tija, tunafanya yale yale. Kwa hiyo, hata tukisema Hawa Ghasia uondoke tunakuonea, tukisema Waziri Mkuu aondoke tunamwonea, alikuwepo Waziri Mkuu mwingine akaondoka mambo yako vilevile.

Tukamleta Waziri wa Maliasili tukamtoa Maige, naona tulimwonea, amekuja mwingine mambo yako vilevile; sasa tufanyeje? Watanzania nawasihi na Ngeleja kaondoka umeme na mgao uko vilevile; sasa tufanyeje jamani? Tuliambiwa nguzo za umeme zinatoka South Africa mtanunua hapa hapa sasa mnanunua huko huko nje; *what can we do* na bei ipo vilevile? Hizi ni kamba anazosema Wenje hapa tufanyeje? *(Makofi)*

Niwasihi tu Watanzania, muda umefika, hii nchi ni yetu sote, siyo ya Wanasiasa peke yao walioko humu ndani. Watanzania mnaotusikia huko nje, *is time to make some changes for this Government,* ni wakati wa ku-*vote out* hiki Chama kimeshindwa kutuongoza kwa sababu kuna ubadhirifu mwingi watu mpaka wanamchukia *CAG* kwa kosa gani yeye anatusaidia! *(Makofi)*

[MHE. MCH. PETER S. MSIGWA]

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni yetu ya 64 (1), narudia tena kuvumilia kwa sababu si mimi tu Watanzania wote wamemvumilia wanamjua. Pamoja na kumjua Mheshimiwa Msigwa Mchungaji kwamba ndiyo maneno yake ya siku zote, lakini nilitaka afute hii kauli ambayo ameitumia, imekiuka Kanuni ya 64(1)(g). Kanuni yetu humu ndani inakataza kutumia lugha ya kuudhi.

Mimi nataka kuamini kwamba, amewaudhi Wana-CCM waliomo humu ndani kwa kusema Chama cha Mapinduzi ni Chama chakavu. Vyama vyote 21 vilivyosajiliwa, vyote vina hati inayofanana na vyote vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria na ukisoma ile hati hakuna ambayo imeandikwa tofauti na nyingine.

Sasa nataka athibitishe hapa, kwenye Hati ya Chama cha Mapinduzi kuna maneno imeandikwa tofauti na hati nyingine kwamba Chama cha Mapinduzi ni Chama Chakavu au afute kauli yake na awaombe radhi Wabunge wa CCM kwa sababu Chama cha Mapinduzi ni Chama imara, Chama chenye nguvu, Chama ambacho kimeingiza Wabunge humu ndani zaidi ya asilimia 75. Chama ambacho hivi sasa Serikali hii inatekeleza Sera yake. Chama ambacho kinasimamia utekelezaji wa Ilani lakini kinasimamia maendeleo ya nchi hii ikiwa ni pamoja na mshahara wa Mheshimiwa Mchungaji. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wana-CCM hawa, Wabunge waliopo hapa, lugha hii ni ya kuudhi wala bila mzaha. Maneno yote aliyotukana tunajua ni tabia yake, lakini hii ya kuudhi ya Chama chakavu, naomba afute. Kwa niaba ya Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, afute lugha hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, una dakika moja!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naona ni tatizo la uelewa tu, kitu chakavu kinaweza kikawa kimechakaa, kina umri mrefu, haki-*deliver*. Sasa Chama cha Mapinduzi kinashindwa ku-*deliver,* kwa hiyo, siwezi kufuta kwa sababu sijatumia maneno ya kuudhi, labda ni uelewa tu wa kuelewa, uchakavu kikiwa na umri mrefu, mzee akiwa ana umri mrefu amechakaa. Sasa Chama cha Mapinduzi kina umri mrefu kimechakaa, kwa hiyo, sijatumia maneno ya maudhi. *(Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Nitatolea baadaye kidogo ufafanuzi kuhusu jambo hili. Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Keissy ajiandae!

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami nichangie katika ajenda iliyoko mbele yetu inayohusu Kamati ya Bajeti, Kamati ya *PAC* na *LAAC.*

Ninayo shukrani mbele za Mungu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili nami niweze kusema machache kuhusu namna gani tunatakiwa kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaongea mengi, nataka niweke mambo sawasawa, kuna watu wamediriki kusema kwamba, Waziri Mkuu ajiuzulu, sijui Chama cha CCM ni chakavu, sijui hiki Chama hakiwezi! Nashauri tu kwamba, Chama cha CHADEMA Mheshimiwa Mbowe ajiuzulu. Kwa nini nasema hivyo?

Tangu amechukua Chama hiki kutoka kwa Baba Mkwe wake, hajawahi kufanya Uchaguzi ndani ya nchi hii kuwaruhusu watu wengine waweze kuchukua nafasi. Chama ambacho Mwenyekiti ana zaidi ya miaka 15, ni Chama ambacho kipo kama cha ujima au cha ukoo. *(Makofi)*

[MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA]

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. Kwa kuthibitisha hayo, Mheshimwa Kabwe amediriki kusema kila siku jamani tufanye ukaguzi, ruzuku zinaenda na hivi na vile, wamempiga chini Uongozi kwa sababu anataka mambo yaende sawa. *(Makofi)*

Wabunge wote walioko katika Chama cha CHADEMA waliokuwa katika nafasi za Waziri Vivuli walipohoji ruzuku wamepigwa chini, leo siyo Mawaziri Vivuli. Halafu hawa watu wanataka kupewa nchi, kama ruzuku yenyewe imekuwa mgogoro bajeti ya nchi mtaiweza? *(Makofi)*

Nataka niulize kama hawa ni waadilifu ni namna gani Wabunge wa Viti Maalum wanaingia katika Bunge hili; uchaguzi unafanyika vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wanadhani hatujui, kuna mgogoro katika Chama chao. Mtu unajikopesha milioni 100 halafu unasema nimejikopesha milioni 20 unatoa kwenye Ruzuku lakini unasema unataka kuongoza nchi. Mimi nasema kwamba, CCM ni halali na tutaendelea kuongoza. Ninaona tunaendelea vizuri na mwaka 2015 tutakuwa nao walioko huku kama Leticia Nyerere; unatafuta nini huko wewe ni mtoto wa CCM rudi katika nafasi yako! Kuna watu makini mpo huko, rudini mchukue nafasi, hamna haja ya kukaa kupoteza wakati, wakati wa CCM kushika hatamu umefika mara mbili yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mengi kuhusu Chama hiki lakini hebu niache wataendelea kusoma nyakati na Mheshimiwa Zitto Kabwe, endelea kuulizia ruzuku ili tujue hizo hela zinaenda wapi, ndipo baadaye waseme wanataka kutawala nchi. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, niende kwenye masuala mengine ambayo nitaongelea hata Jimbo langu la Nkenge. Nichangie kwenye hoja ya msingi, naomba niongelee Wizara ya Nishati. Ukiangalia katika Kitabu hiki au katika Taarifa ya *PAC,* ukurasa namba 18, ukaangalia Jedwali

[MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA]
Namba 8, utaona utaratibu ulivyokuwa umeenda wa namna wanavyopokea fedha kwenye *REA*. Mwaka 2012/ 2013 utaona wamepokea fedha kiasi cha asilimia 31 na hii 69 haijapelekwa na hatuelewi itapelekwa lini.

Niombe tu kuwasihi watu wanaosimamia masuala haya, masuala ya umeme siyo jambo la mchezo, watu wengi wanategemea umeme kwa ajili ya kuendeleza maisha yao. Kwa hiyo, naiomba Wizara ilione hili ni la msingi kabisa na badala ya fedha za maendeleo kwenda *percent* kubwa ipeleke fedha za matumizi, zinaenda nyingi kuliko fedha za maendeleo, matokeo yake matumizi ni makubwa kuliko mambo ya maendeleo. Kwa hiyo, naomba sana sana hebu tuangalie maendeleo kuliko matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Rais alipoutembelea Mkoa wa Kagera, alitembelea na Jimbo la Nkenge na alipolitembelea Mheshimiwa Muhongo alisimama, akawaambia Wana wa Kagera na Misenyi hasa Misenyi kwamba, tarehe 25 Desemba, 2013, Mtukura umeme utakuwa unawaka. Wale Wananchi wakaenda wakafanya *wiring* nyumba zao, tayari wanangoja kusherehekea Christmas kwa umeme, lakini mpaka leo hata nguzo hatujaziona!

Sasa wamenituma, sikiliza niwaambie ninyi mnaweza? Mmeshindwa hebu niwaache, ninyi ndiyo ambao mnapeana kwa undugu vyeo siyo, basi hebu niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haimaanishi kwamba, Chama cha Mapinduzi hakiwezi, ngoja niwaulize; Wabunge kama mambo haya hatutakiwi kuongea wala kuongezea tukae nyumbani tuchaguliwe tuje mara moja na tukae nyumbani. Tuko hapa Bungeni kila mara kwa ajili ya kueleza mambo yasonge mbele. Haina maana kama kitu hakijafanyika tusiongee kwa sababu hatuwezi, tunamaliza moja tunaenda jambo linguine. La sivyo, tuwe tunahudhuria Bunge mara moja na mambo tunayaacha

yanaendelea peke yake, lakini utaratibu tunapokuja tunakuja kueleza mambo yapate kusonga mbele.

Umenielewa sina sababu ya kusema mtu hawezi hata wewe mwenyewe huwezi. Naomba atakapokuja Mheshimiwa atueleze Christmas itakuwaje kwa sababu yeye mwenyewe alitamka au hapo baadaye anapoeleza anaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine muhimu ambalo linatusumbua sasa hivi ni uagizaji wa sukari ambapo kibali kinatokea katika Wizara ya Kilimo. Naomba niseme jambo moja, hivi Serikali inaonaje kuamua kutoa hicho kibali kwa mtu ambaye ana mzigo wala hana *mandate* ya kuleta sukari; kwa nini hicho kibali kinachotolewa kisitolewe kwa wale walio na lile jukumu la kuleta sukari mfano; wawekezaji ambao wamewekeza kwenye viwanda vya sukari? Sasa hivi sukari zao zipo nyumbani, zipo kwenye magodown wameshindwa kupata soko zuri kwa sababu ya kuingiza sukari kutoka nje.

Ninaomba na nitaleta hoja yangu binafsi ya kuonesha ni namna gani uingizaji wa sukari holela unaweza kuharibu viwanda vya ndani na kuharibu Sera yetu ambayo tumesema tunalinda viwanda vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekutana na mwenye Kiwanda cha Kagera Sugar, ameniambia ifikapo Desemba tarehe 31, ataondoa watu 3,000 kutoka kiwandani kwake kama Serikali haitadhibiti uingizwaji wa sukari. Kwa hiyo, nashauri Serikali hebu tuwape wale wenye viwanda jukumu la kuhakikisha tuna sukari na Bodi ya Sukari ihakikishe tunapata sukari kuliko kuwapa watu wengine ambao wanafanya biashara. Matokeo yake viwanda vinasimama na Mwekezaji amesema Mtibwa ataondoa wafanyakazi 4,000. Niambie wafanyakazi 7,000 wakikosa kazi itakuwa haisaidii. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu kwamba, ni wakati mzuri sasa wa kuangalia na kuvilinda viwanda vyetu vya ndani ili wale waliowekeza mikopo yao waweze kulipa vizuri.

[MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA]

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani bado nina muda kidogo, ninapenda niongelee jambo lingine. Ukiangalia katika matumizi ya Serikali, kawaida matumizi yoyote mtu lazima utumie kulingana na unavyopata; tatizo letu sasa hivi linalotukumba tunatumia zaidi ya mapato tunayopata.

Kwa hiyo, hebu tufanye kitu kimoja na nasema nipo katika Kamati ya Bajeti, tunatakiwa kuangalia ni kiwango gani tunaingiza na kiwango gani tunatakiwa kutumia ndipo tuweze kuweka bajeti na kuweka matumizi yetu. Ni aibu kubwa ukakuta una shilingi 300,000 umeandaa matumizi ya shilingi 500,000, ukitegemea jirani utamwomba shilingi 100,000, ukitegemea jirani mwingine utamwomba shilingi 50,000. Matokeo yake ile shilingi 50,000 na shilingi 100,000 ukikosa unapata *deficit*. Kwa hiyo, ili tuepukane nayo tuandae vitu kulingana na tulichonacho.

Tukiwa nacho mkononi ndiyo tuandae bajeti, tukisema barabara tatu ni tatu, hakuna haja ya kutandaza barabara 100 wakati unaweza kulipia barabara tatu. Tukisema visima vitano ndiyo nguvu yetu tuweke visima vitano, kuliko unasema visima kumi unatangaza mpaka unaleta makaratasi, kama suala la umeme tulipeleka makaratasi kila Kata kwamba, ninyi mtapata mpaka leo hatujapata.

Ninaomba tubajeti kitu kulingana na uwezo wetu. Siku moja nilishauri kuwa na *Capital Budget*. Hii inamaanisha kwamba, unajua utatumia milioni 800, unazo milioni 500, unakopa 300 kwanza unaiweka kwenye mfuko wako. Ukiwa nayo sasa unabajeti ndiyo inaitwa *Capital Budget,* lakini ukisema *Cash Budget* ina maana ukusanye, utoze ushuru, wengine wanagoma, matokeo yake hatuwezi kufika. Hebu tuanze na kitu mkononi, una milioni 500 unabajeti kwa milioni 500, kuliko kubajeti 800 wakati unayo 500. Nafikiri tukifanya hivyo hata wale ambao wanataka kutusaidia, wasipoleta kwa wakati tutaweza kufika na tutaweza kufanya.

Nimalizie kwa kusema kwamba, wakati umefika wa watu wote ambao ninawaomba Watanzania mlionisikiliza

[MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA]

leo mnaweza kupima pumba na mchele ni upi. Mkikaa mkapima hivyo vichochezi vya kusema tumechakaa ndiyo kwanza tumesimama imara achaneni navyo. Chama cha Mapinduzi kimesimama na kimepita Taifa zima Tanzania, watu wamekipa kura kuliko vyote. Hata ninyi mnaosikiliza, wanaowaambia wameanza kuchanana, wamefukuzana. Wenyeviti wanatoka, anayeuliza hiki anaambiwa toka, wanataka mtu ambaye akiona ananyamaza, lakini arefushe mkono kwa upande mwingine. Sasa na sisi tunaona hatunyamazi tunawaeleza Watanzania wapate kuelewa.

Katika haya machache, naomba Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Wenje, kwa sababu muda ni mdogo sana, nakuombeni sana tuwe na uvumilivu. Mwishoni nikipata dakika mbili, tatu, nitawaruhusu.

Mheshimiwa Keissy!

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Cha muhimu kabisa, sisi wote hapa ni Madiwani. Wabunge wote ni Madiwani. Mambo yanapoharibika katika Halmashauri tusiwasingizie Madiwani, pamoja na sisi. Siyo TAMISEMI peke yake, wote ni Madiwani tunahusika. *(Makofi)*

Jambo la pili, ubadhirifu mkubwa, pamoja na Madiwani, Wabunge wenzetu hapa; kuna baadhi ya Wabunge wanapewa pesa za safari, tunasafiri kwenda nje au kwenda mikoani, hawasafiri na pesa hawarudishi. Namwomba *CAG* na TAKUKURU, wafuatilie kila Mbunge aliyepewa hela za safari hakusafiri; huu ni wizi apelekwe Mahakamani moja kwa moja. Hizi hela za walipa kodi, Wabunge wamo humu. Juzi juzi mtu mmoja mkubwa wa Chama, kamrudisha mke wake alikuwa anakwenda Dominica, kamrudishia New York arudi Dubai. Pesa za Bunge, za Serikali, za walipa kodi.

WABUNGE FULANI: Mtaje!

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Atatajwa na *CAG* na TAKUKURU anajulikana. Sasa huu unakuwa ni ubadhirifu. *(Kicheko/Makofi)*

Ninyi mnasema mizigo ni Mawaziri na Wabunge ni mizigo zaidi. Huu ni wizi, tena ni wizi kabisa. Bora mvunja majumba, Mbunge mzima, posho yako nzuri, mshahara mzuri, unapewa pesa kwa ajili ya kwenda kukagua Miradi, unachukua posho unakaa Dar es Salaam. Wewe ni Mbunge kweli, una uchungu na nchi yako? Unapewa pesa zaidi ya milioni tano, milioni sita, kwenda nje huendi nje na Tiketi ya *Business Class* inapotea! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili naomba Waziri Mkuu au Mheshimiwa Rais ampe *CAG* pesa akague Wabunge wote mmoja baada ya mwingine. Wote ambao hawakusafiri, wamechukua posho, wawajibike wapelekwe Mahakamani. Hawa ni wezi wakubwa. Watatajwa wanajulikana. Wanajijua wamo wote humu, kama hawamo wako nje.

Baadhi ya Wabunge wanawalazimisha Wakurugenzi kuchukua mafuta wakati tunapewa posho za mafuta, wanajulikana.

Baadhi ya Wabunge wapo huku, Vikao vya Halmashauri vinatendeka kule, wanasafiri wanakwenda kuchukua posho. Wabunge hao, lakini hapo hapo wanachongoa mdomo wanasema ooh, CCM, CCM. Ndugu zangu Wabunge tujichunguze, Wabunge wote wabadhirifu sasa kimoto kimefika kitawabana. *CAG,* TAKUKURU watawabana, hamna msalie Mtume. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naanza kuchangia hoja. Sikuwepo muda mrefu. Kuhusu leseni za magari, Serikali haipati kitu, ni Kampuni ya Israeli ndiyo inachukua, yaani hamna chochote inachopata Serikali. Serikali inaambulia

[MHE. ALLY KEISSY MOHAMED]

dola nane, ina wafanyakazi, inatumia umeme na kila kitu, ile kampuni imekaa inachukua dola 22. Sasa hii inakuwa haina faida na kila baada ya miaka mitatu anakata leseni nyingine. Naomba sana, Serikali ifikirie mambo ya leseni, iwe miaka mitano na hiyo kampuni ipigwe marufuku, waifanye *TRA* wenyewe hizo leseni. Hatuna faida kabisa na hizo leseni. Serikali haipati kitu, inaitajirisha Kampuni ya Israeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Utangazaji *TBC*; Ripoti ya Hesabu za Serikali inaonesha kuwa, Shirika lipo *ICU,* linadaiwa zaidi ya shilingi bilioni mbili. Shirika letu litakufa kama *ATC.* Sasa hili ndiyo Shirika letu la kutegemea habari, tutashindwaje na Mashirika mengine madogo madogo? Serikali iliangalie upya hili Shirika, iwape matangazo yote ya Serikali, siyo kunyima matangazo ya Serikali. Matangazo yote yaende *TBC* ili Shirika lijitegemee na yeyote mwenye *TV* alipie leseni, pesa ziende *TBC*.

Waingereza ndiyo wafadhili wetu, lakini Uingereza ukienda leo *Television* zote zinalipiwa. Sisi hapa kila kitu bure, tutafika wapi nchi maskini? Waingereza wanaotufadhili wanalipia *Television* na hela zote zinakwenda *BBC;* ndiyo sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri kupata Hati Chafu, inaadhibiwa haipelekewi hela za maendeleo. Mnashindwa kuwakamata mnawaadhibu Wananchi? Kwa mfano, Halmashauri ya Nkansi imepata Hati Chafu, pesa za Miradi hazikwenda. Za umwagiliaji kule Lwanfi wamewanyima Wananchi wasilime mpunga. Wakati wezi wanajulikana, ninyi mnawaadhibu Wananchi maana yake nini? Huu ni udhaifu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi ya simu; tumeambiwa kila siku hapa kwamba, hawa jamaa wana promosheni za ajabu, mabajaji, mameseji ya ajabu ajabu yanaingiza pesa usiku na mchana; lakini hakuna mtambo wa ku-*control* mawasiliano. Angalieni barabara, kwa mfano, barabara inapojengwa na mizani tayari kudhibiti mizigo.

[MHE. ALLY KEISSY MOHAMED]
Mnashindwaje pale pale mwanzoni kupata mtambo kudhibiti ili tupate kodi? Tunashindwa na Rwanda, wana pesa nyingi za mawasiliano kuliko nchi kubwa kama Tanzania! Huu mtambo ni muhimu, promosheni za simu zimezidi, wanatuletea meseji kila siku, bahati nasibu wanachezesha, hatujui kodi yake inakwenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pesa za harambee; unakuta mtu anafanya harambee shilingi milioni mia mbili, mia tatu, amelipa kodi? Hizo pesa zimelipiwa kodi? Harambee ya harusi ilipiwe kodi, harambee ya Msikiti ilipiwe kodi, harambee ya Kanisa ilipiwe kodi. Sasa tunafanya maharambee, siku hizi ndiyo imekuwa mtindo; lakini kodi hakuna. Harambee yako wewe fanya, lakini tupatie kodi yetu, wewe nenda zako na harambee zako. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliodhaminiwa na Serikali yetu zaidi ya trilioni 1.2, wamestarehe na wake zao na watoto wao, sisi tuwalipie Wananchi wetu. Tuwalipie hawa waliodhaminiwa na Serikali mabilioni ya hela, sisi tuwalipie. Wamejifilisi wengine kijanja kijanja, sisi tuwalipie maana yake nini? Hao watu wanaoingia mikataba kuwapa mikopo hao jamaa kuwadhamini; wachukuliwe hatua si wapo.

Leo ukienda Benki kukopa, masharti kibao; sasa wao walikopaje hizo pesa bila masharti? Mnawadhamini wenye Viwanda vya Sukari, Migodi ya Kiwira, wenye mashamba makubwa; lakini hakuna waliolipa. Wamestarehe na wake zao na watoto zao. Wananchi wanyonge waendelee kunyongwa kuwalipia hayo madeni ya mabilioni ya hela. Lazima wafuatwe jamaa wote waliowadhamini mikataba kihuni kihuni, walipiwe hizo hela.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika Marehemu Hayati *ATC,* Mikataba ya ajabu ajabu iliwekwa, twende kulipia madeni ya ajabu ajabu, wenyewe wapo wamestarehe na wake zao. Nchi hii ndugu zangu, tutapiga kelele hapa Bungeni kama watoto wadogo, bila kubadilisha sheria ziwe kali kama za Kichina za kuwakatakata hawa jamaa,

hatuwezi kufika. Narudia kila mara, hawa adhabu yao ni kifo na kunyang'anya mali yao. Hakuna msalie Mtume. *(Kicheko)*

Hawa jamaa wamekaa wamestarehe wanatucheka. Wakienda Mahakamani wanafungwa miaka miwili. Wewe umeiba kuku au ng'ombe, miaka saba, anayeiba mabilioni ya hela, miaka miaka miwili. Inatia uchungu sana nchi hii. Mfano tu kule kwangu Namanyele, Bwana Samaki, alitumia mafuta lita 4,500 badala ya lita 400; akashinda kesi. Ndugu zangu, tunakwenda wapi? Mawakili hawaendi Mahakamani, wanapeleka washitakiwa Mahakamani. Serikali, wale Mawakili hawaendi Mahakamani, inasomwa kesi hawana habari wanakunywa pombe mpaka kesi inafutwa, hana habari. Siku kesi inafutwa ndiyo anashituka, aah, anakunywa pombe tu. Hawa Wanasheria wanaajiriwa kula mishahara bure tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hapa inasema pesa, haziendi Wilayani ndugu zangu. Haziendi kabisa kabisa ni asilimia kumi au kumi na mbili na wakati mwingine hakuna kabisa. Maendeleo yatakuja bila pesa? Hayo mnayoyasema, mnamsifu Mandela alikuwa na msamaha amesamehe, hakusamehe wezi. Hataki kusamehe wezi. Mandela alisamehe na wezi wasamehewe? Hakuna msamaha. Tunaanzia hapa Wabunge wezi wanaopewa pesa hawasafiri ni wezi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuendi kwa kupendeleana, hapa ni vyama vyote vinahusika. Tunachongoa midomo hapa tunazungumza, wapo wakubwa wa vyama wanajulikana, mtu anakwenda Dominica, anarudia New York, anakwenda kustarehe Dubai. Anapewa hela za kwenda London na hela nyingi mzee; dola 420 kwa siku, siku kumi, dola 4500 za walipa kodi, *Business Class*, mnakaa Dar es Salaam ndugu zangu. Halafu mnasema Waziri mzigo, Waziri mzigo! *(Kicheko/Makofi)*

[MHE. ALLY KEISSY MOHAMED]

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Kilimo nimemfuata mimi, hajapewa hela za kulipa mfano mahindi Rukwa. Nimemwendea Waziri wa Fedha anasema hela hatuna. Waziri achukue hela za mfukoni kwake apeleke Rukwa? Unasema mzigo wewe, achukue hela za mfukoni apeleke Rukwa? Mimi nakujibu wewe unayesema mzigo wakati na ninyi vilevile mnapewa pesa, hamwendi safari. Chama chako, umekwenda kukaguliwa umekataa kukaguliwa, unachukua pesa unakwenda kununua nyumba Dubai. Wewe huyaoni hayo? Hela za bendera unaongezea hukohuko, kontena la bendera liko wapi! Liko wapi kontena la bendera hapa? *(Kicheko/Makofi)*

Usipige mawe wewe unakimbilia kwenye nyumba ya vioo, lete hesabu zikaguliwe kama ruzuku imenunua ya Dubai itaonesha. Hatuna maelewano hapa. Siyo kusema CCM tu, sijui Waziri Mkuu na nini, sijui namna hii, wakati wakikuchunguza wewe umechukua pesa za *imprest* hukwenda popote! *(Kicheko/Makofi)*

Unachukua pesa za Serikali, za walala hoi, unapewa safari ya siku kumi, ukifika kule siku mbili umesharudi. Siku nane, umerudisha pesa za siku nane? Unasingizia mtoto mgonjwa au mama mgonjwa. Watatajwa na *CAG.* Tunawajua, mimi sitaki kuwataja majina hapa. Wote mmo, mna cha Chama hapa wote mno. Tutafuatilia mpaka hoteli kama hamkulala, *boarding pass,* kama ulilala na tiketi utazionesha. Kazi ndogo kuwakamata hawa. Waache kuwaambia Mawaziri mizigo. Waziri yuko hapa kule Nkansi wanaiba, Waziri Hawa Ghasia atajua? Wewe Mbunge ni kazi yako, ni Diwani, kushughulikia Wilaya yako kudhibiti wezi. Kazi yako nini wewe Mbunge? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi nimemkamata Mtendaji, hela za mchango milioni 18 anaweka kwenye akaunti yake badala ya akaunti ya kijiji, nikamkamata. Kihoro, akakimbia kufika Dar es Salaam akagongwa na gari akafa.

MBUNGE FULANI: Umemuua wewe! *(Kicheko)*

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Amejiua kwa kihoro. Anachukua hela za michango anaweka kwenye akaunti yake. Mimi nikamkamata kwenye Kikao cha *Ward C,* twende Benki, kwenda Benki hakuna hela, nikamwambia nitakupeleka Polisi. Huku na huku, hela kaweka kwenye akaunti yake, kumbana bado milioni nne, katoroka. Kufika Dar es Salaam, Mungu si Athumani, gari ikamgonga kafa na deni la Wananchi. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa wewe kama Mbunge umechukua hatua gani kwenye Wilaya yako kudhibiti wizi au kazi yenu kwenda kuchukua posho kwenye Vikao vya Halmashauri au umekaa hapa kwa ajili ya kuchukua posho? Dhibiti wizi kwenye Halmashauri yako. Wewe ni Diwani, ndiyo kazi yetu sisi. Siyo unafika pale kazi yako kupiga makofi na kwenda kwa Mkurugenzi kuomba pesa ya mafuta. Hiyo siyo kazi yako wewe, kazi yako ni kudhibiti Halmashauri yako. Wewe ndiyo mkubwa pale, katika Madiwani wewe Mbunge ndiyo Diwani mkubwa. Kila Halmashauri ina Mbunge, pamoja Viti Maalum tumo mle mna kazi gani? Tena wanasema Mbunge wa Mkoa. Mbunge wa Mkoa ingia kwenye Vikao vya Halmashauri, angalia wizi, pita pita chunguza, siyo kazi yako kupokea ripoti tu. *(Makofi)*

Wewe kaa kwenye vijiwe, utajua nani kaiba na nani hakuiba, siyo unavaa suti tu unakaa baa. Hiyo siyo kazi ya Mbunge. Kazi ya Mbunge ni kufuatilia kila kitu katika Wilaya yako. Siyo unavaa suti unakwenda kuwatisha mimi Mbunge, mimi Mheshimiwa; Mheshimiwa gani wewe? Mheshimiwa dhibiti wizi. Nawaambia Wabunge wote, Wilaya zote zina matatizo pamoja na Mbozi Mashariki. *(Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Keissy, tunakushukuru.

MHE. ALLY KEISSY MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba pesa itolewe kwa *CAG,* akague Wabunge wote waliopewa *imprest* za safari kama walitumia zile hela kihalali. Siwezi kuacha, nitamwambia hata *President Kikwete* atoe hizo pesa. *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Keissy. Kwa dakika nilizonazo, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, unaweza kuzitumia?

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba niseme tu kwamba, nitazungumza kwa kifupi sana.

Kwanza, naomba nizipongeze Kamati zote kwa kazi kubwa na nzuri waliyofanya. La pili, naomba kulifahamisha na Bunge lako Tukufu kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC,* nimekagua mahesabu na pia nimetembelea baadhi ya Halmashauri. Kwa kifupi sana, taarifa iliyotolewa na Kamati ni taarifa halisi, ni taarifa ya kweli inayoonesha hali ilivyo kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana kulitokea mazingira ya namna hii hii kwa Mheshimiwa Mkuchika, akiwa Waziri kwenye Wizara hii. Ninaomba sana kwamba, umefika wakati sasa tutafute namna ya kubadilisha mifumo iliyoko. Sidhani kama Waziri kama Waziri anaweza akawa ni *solution,* kama walivyosema wengine, mimi si-*recommend* sana suala la kumwajibisha Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo kubwa sana la mifumo kule chini kwenye Halmashauri zetu. Cha kwanza ambacho tunapaswa kukielewa ni kwamba, Bunge dogo kwenye Wilaya ni Baraza la Madiwani. Madiwani ambao ndiyo wanasimamia hizi fedha, ni watu muhimu sana katika kufanya kazi. Tukitaka kutatua matatizo haya, tuhahitaji tuanzie na wao.

Katika kutatua matatizo ya Madiwani, cha kwanza kikubwa Madiwani wanatakiwa wajengewe uwezo. Uwezo wa Madiwani kitaaluma ni mdogo sana. Haiwezekani katika mazingira niliyoyaona kwenye Halmashauri zilizo nyingi, Diwani ambaye uwezo wake na elimu yake ni ndogo, aweze kukagua Miradi. Baya zaidi, pia hata utaratibu uliowekwa, Madiwani hawaruhusiwi kukagua Miradi.

[MHE. EZEKIEL M. MAIGE]

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka kwenye mkutano mmoja wa *LART* Arusha, tulizungumza na Waziri Mkuu na mimi nilikuwepo, moja ya mambo yaliyoazimiwa ni kuwaomba Madiwani waunde Kamati kama ilivyo Kamati ya *LAAC,* kama ilivyo Kamati ya *PAC*, kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa Miradi kwenye Halmashauri zao. Jambo hili lilikubaliwa, bahati mbaya halijatekelezwa.

Ninaomba sana jambo hili litazamwe na litekelezwe, ili Madiwani kupitia Kamati ndogo ndogo hizi, waweze kufanya ziara ya kukagua Miradi. Kamati ya *LAAC* inakagua Miradi kwenye Halmashauri zaidi ya 160. Haiwezi ikakagua Miradi yote na haiwezi ikakagua Halmashauri zote. Wawakilishi wa Watanzania kwenye Halmashauri ni Madiwani. Madiwani wajengewe uwezo wa kuweza kukagua Miradi na kwa kiasi kikubwa wataweza kusaidia kutatua matatizo katika hatua za awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo linahitaji kutatuliwa la Madiwani ni mapato yao. Mapato ya Madiwani ni kidogo sana. Wanakuwa *very venerable* na rushwa. Katika mazingira ambayo Diwani analipwa kiasi kidogo namna hiyo, anafanya kazi kwa kujitolea na unakuta anakuwa na *Full Council* labda mara moja kwa miezi mitatu au zaidi ya hapo hakuna vikao vyovyote wala shughuli zozote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikwenda kwenye Halmashauri moja tukakuta kuna ugomvi mkubwa sana baina ya Madiwani na Mkurugenzi. Baada ya uchunguzi tuligundua kwamba, ugomvi uliopo ni kwa sababu tu yule Mkurugenzi eti analaumiwa kwamba ana roho mbaya, anawabania Madiwani, hawapi safari, hawapi mafunzo, hafanyi hiki. Kwa uelewa wa Madiwani wale walikuwa wanadhani Mkurugenzi yule anayafanya yale kwa matashi yake, lakini ndivyo utaratibu ulivyo. Kwa hiyo, naomba sana mapato ya Madiwani yaboreshwe ili waweze kufanya kazi vizuri.

[MHE. EZEKIEL M. MAIGE]

Tusipofanya hivyo, kwa maana ya kuwajengea uwezo wa kiuchumi, wakafanya kazi kwa moyo, wakaacha kufanya kazi kwa kujitolea kama ilivyo hivi sasa; bado matatizo yataendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nadhani ni muhimu likatazamwa ni Idara ya Ukaguzi wa Ndani. Idara hii nayo ni muhimu sana ili kutoa viashiria vya awali kwa Mkurugenzi, ili kuona maeneo ambayo yana upungufu. Idara hizi kwenye Halmashauri nyingi hazina uwezo kabisa, hazina Watumishi wala vitendea kazi; ni Idara muhimu sana, zinahitaji kuwezeshwa ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuishauri Serikali, pengine kuweka *control* kwenye Wizara, yaani Katibu Mkuu wa TAMISEMI awe ndiye Msimamizi wa Halmashauri zote na ndiyo mamlaka ya nidhamu ya Wakurugenzi wote; nadhani inaweza ikawa si jambo zuri sana. Kwa kuwa tunazungumzia *D by D,* nadhani ni muda muhimu na ni jambo zuri, tukiweka uwezekano au kuangalia utaratibu wa kuwawezesha Ma-*RAS* katika mikoa wawe ndiyo mamlaka za nidhamu na kuweza kusimamia Wakurugenzi wote kwenye mikoa yao.

Kwa kufanya hivyo, itakuwa ni rahisi sana kwa sababu Mkurugenzi atakuwa anawajibika kwa mtu ambaye yuko karibu naye. Kwa hivi sasa sidhani kama Katibu wa TAMISEMI ana uwezo kweli wa kujua kinachoendelea *on daily basis* kwa Mkurugenzi aliyeko Nkansi, Mkurugenzi aliyeko Kahama au sehemu nyingine yoyote. Kwa hiyo, Sekretarieti za Mikoa zijengewe uwezo na zikasimiwe baadhi ya madaraka ambayo kwa sasa yapo kwenye Wizara ili ziweze kusimamia Halmashauri hizi kwa ukaribu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la Sheria, Wabunge wengi wamelizungumzia. Sheria ya Utumishi wa Umma imelinda sana Watumishi wa Umma. Ni mara

nyingi sana tunalalamika hapa, kumwajibisha Mtumishi wa Umma *is almost impossible*. *(Makofi)*

Nakumbuka kuna nyakati fulani Viongozi hapa Mawaziri waliwahi kuchukua hatua. Kuna kesi nyingi tu lakini wakienda kwenye Tume ya Utumishi wa Umma wanashinda kesi ili kumfikisha hatua ya kumfukuza kazi ni jambo gumu sana. Hata sasa hivi nikimwuliza Waziri katika kipindi cha mwaka mmoja ni Wakurugenzi wangapi waliofukuzwa kazi, kwa maana ya kufukuzwa katika wizi huu tuliouona, hakuna. Zaidi yake ushahidi unakosekana, taratibu haziwezeshi mtu yule kufukuzwa, inalazimika kumhamisha au kufanya kitu kingine cha namna hiyo. Kwa hiyo, Sheria ya Utumishi wa Umma ni vizuri sana ikatazamwa ili kuwezesha hatua za nidhamu kuchukuliwa kwa urahisi.

Jambo lingine ambalo nadhani ni la muhimu, tumekuwa tukilisema sana kwenye Kamati yetu; Kamati ya *LAAC* kwa mfano, inakwenda inakagua Miradi na inakuta mazingira ya dhahiri kabisa kwamba matumizi mabaya ya fedha yamefanyika. Kamati ile hairuhusiwi kuchukua hatua za kushirikisha vyombo vyenye uwezo wa kufanya hayo. Tumekuwa tukisema mara kwa mara kwamba, hivi kama mtu unakuta kaiba au kajenga jengo vibaya na ushahidi uko wazi; kuna ubaya gani Kamati hii ikawa inafanya kazi kwa karibu sana na Jeshi la Polisi na TAKUKURU ili inapotokea mazingira ya namna hiyo mara moja watu hawa wakabidhiwe?

Sasa hivi kila tukiwaambia mnatuambia sio jukumu letu nendeni mkamwambie Waziri. Mnamwambia Waziri mwaka unapita, mwaka wa pili, matokeo yake anahamisha yule mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba eneo hili nalo ni vizuri tukalitazama, Kamati iwe na uwezo ili pale inapobaini jambo na kuna ulazimu wa kuokoa muda, basi iweze kufanya kazi kwa ukaribu na vyombo hivi, *Law Enforcement Agencies,* ili waweze kuwa wanawakabidhi watu hawa kwa mamlaka zinazohusika na uchunguzi. Kamati ya *LAAC* haina

uwezo wa kuchunguza suala la rushwa, Kamati ya *LAAC* haina uwezo wa kuchunguza suala la jinai kwa maana ya wizi, lakini pale ambapo inabaini jambo hilo iwe ni halali kwa Kamati kuikabidhi TAKUKURU, iwe ni halali kwa Kamati kuikabidhi Polisi *instantly* ili hatua ziweze kuchukuliwa. Kwa kufanya hivyo, ninaamini walau kutakuwa na matukio baadhi ambayo Kamati itaweza kuyafikia yatakayoweza kudhibitiwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda kuwa umekwenda sana na ninaona dakika zimekuwa si nyingi sana, naomba niishie hapo. Niseme tu kwa mara nyingine kwamba, tujaribu kubadilisha mifumo kwenye Serikali za Mitaa kwa kuimarisha uwezo wa Madiwani, kwa kubadilisha Sheria, kwa kukasimu baadhi ya madaraka kutoka kwa Katibu Mkuu TAMISEMI yaende kwa *RAS* katika mikoa ili angalau hatua za haraka ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru naomba kuishia hapo. *(Makofi)*

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Wenje, nusu dakika, kifupi sana muda haupo upande wetu.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 64(1) (a), (b) na (g).

Mheshimiwa Naibu Spika, alipokuwa anazungumza Mchungaji Assumpter, Mchungaji ninayemheshimu sana, ila nasikitika tu kwamba, kama Wachungaji nao wanadanganya basi sijui tutakimbilia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ieleweke. Mheshimiwa Assumpter Mshama, amesema kwamba, Mheshimiwa Zitto amevuliwa uongozi kwenye chama chetu kwa sababu ya ruzuku, ambapo siyo kweli. *That is number one*. Kwa hiyo, amesema uongo na hawezi kuthibitisha hilo.

Amesema kuna wengine wamejikopesha shilingi milioni mia ambayo ni uongo.

MHE. NAIBU SPIKA: Kwamba amesema ruzuku imefanyaje Mheshimiwa?

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) pamoja na 64(1)(a), (b) na (g) ambayo kwanza, inakataza mtu kusema uongo Bungeni na pili, inakataza mtu kusema, naomba nisome *just a minute.*

NAIBU SPIKA: Endelea tu na *issue* yenyewe, nakuelewa nasema tu amesema uongo, kile alichosema uongo kifafanue vizuri.

MHE. EZEKIA D. WENJE: *Number one,* amesema uongo kwamba, Mheshimiwa Zitto amevuliwa Uongozi CHADEMA kwa sababu ya ruzuku.

Pili, amesema kuna watu wanajikopesha shilingi milioni mia huku anaandika milioni ishirini, ni uongo.

Tatu, anasema CHADEMA haijawahi kufanya uchaguzi chini ya Mbowe, ni uongo.

Nne, anasema waliohoji ruzuku kwenye Baraza Kivuli la CHADEMA waliondolewa, ni uongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kisheria mtu anayetoa *allegations* ana wajibu wa *ku-substantiate allegations* anazotoa. Inasikitisha kama Wachungaji wanasema uongo ndani ya Bunge, Taifa hili tutaenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wote wawili, nawaomba Mheshimiwa *Chief Whip* na Mheshimiwa Silinde, mkitazama muda kwa kweli haupo upande wetu hata kidogo. Hatuna hata dakika moja ya kuweza kuendelea.

Ninachotaka kukisemea kwa ujumla katika mambo haya ni kwamba, tuwe na uvumilivu. Waheshimiwa Wabunge, tuwe na uvumilivu. Sisi wote ni Wanasiasa hapa na Mwanasiasa ukipigwa lazima ujibu mapigo. Kwa kweli ndiyo Mwanasiasa. Ukiwa Mwanasiasa ninyi CCM mnakaa hapa mnapigwapigwa mmekaakaa tu hapa basi ninyi siyo Wanasiasa au ninyi Wapinzani mmekaakaa hapa mnapigwa mnaangalia tu, katika siasa mimi ukinipiga Job Ndugai nakujibu kesho asubuhi, yaani hiyo haina wasiwasi kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Tena nakujibu kwa *media* ileile, lakini sitatukana, sitafanya hivi na tungependa Bunge letu liwe hivyo. Pale tunapojibiwa tuwe na ngozi ngumu kidogo kuvumilia. Maana habari zinazosemwa kila watu wanaokotaokota kwenye vyombo vya habari, huyu anasoma gazeti hili, huyu anasoma lile, huyu anapigiwa simu, lakini kwa ujumla tuvumiliane, tuwe na lugha za staha. *(Makofi)*

Tukiwa na kiasi tutajikuta wote hatuumiiumii hivi, lakini tukipitiliza, mtu mmoja tu akipitiliza, anafungulia ile niliyosema asubuhi. Sasa ikishafunguka kidogo; kwa hiyo, namwona Mheshimiwa Wenje hawezi kukaa chini, lazima uwe Mwanasiasa. Mwanasiasa ni pamoja na kuvumilia kupigwa kidogo halafu baadaye unatafuta namna gani utajibu mapigo.

Baada ya maelezo hayo, nawaombeni Waheshimiwa Wabunge, tunachokiongea hapa ni kwa nia njema ya kujenga nchi yetu. Yeyote aliyeiba hela za Serikali siyo kwa sababu yeye ni Mwanachama wa Chama chochote cha Siasa. Hatuna Chama katika nchi yetu mpaka sasa ambacho Sera yake ni kupalilia wizi. Inawezekana kabisa, kwa sababu Wafanyakazi wa Serikali wanaruhusiwa kuwa Wanachama wa Chama isipokuwa

[NAIBU SPIKA]
kutokuwa Viongozi, anaweza kuwa ni Mwanachama wa Chama chako. Sasa wewe ukafikiri kwa sababu tu ni Mfanyakazi wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo, kila Mtumishi ni wa CCM au mambo ya namna hiyo; siyo kweli hata kidogo. Kwa hiyo, tushughulikie tatizo lilipo, tusiposhughulikia tatizo lilipo tutajikuta tumepanua wigo halafu tutakuwa hatujashughulikia chochote kile katika ufumbuzi wa jambo hili.

Mwisho, nami niwaombe sana, Waheshimiwa Wabunge, sisi sote ni Madiwani kwenye Halmashauri zetu, itasaidia sana tukihudhuria vikao, itasaidia sana tukifuatilia mambo na tukawasiliana na Waheshimiwa Mawaziri husika katika maeneo ambayo tunadhani yana upungufu, tuone namna gani ya kusaidiana na Serikali katika kutatua matatizo, maana nchi hii ni kubwa na mambo ni mengi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi na Mheshimiwa Mturano atakuwa ndiyo mchangiaji wa kwanza.

(Saa 1.45 jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 11 Desemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)